

## BUNGE LA TANZANIA

---

### MAJADILIANO YA BUNGE

---

### MKUTANO WA KUMI NA TANO

**Kikao cha Nne -Tarehe 5 Aprili, 2019**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

### D U A

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae. Katibu!

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:**

### MASWALI NA MAJIBU

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, maswali, tutaanza na Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni, sasa aulize swali lake.

Na 24

**Idadi ya Watu Wenye Ulemavu Nchini**

**MHE. MAULID S. MTULIA** aliuliza:-

Walemvu wana mahitaji maalum ukilinganisha na watu wasiokuwa na Ulemavu na idadi ya walemvu imekua ikiongezeka siku hadi siku kutokana na ajali za barabarani hasa zitokanazo na usafiri wa bodaboda:-

(a) Je, Serikali inaweza kutoa orodha ya idadi ya watu wenye ulemavu nchini kwa kuzingatia makundi yao kwa asilimia?

(b) Je, Serikali ina mpango gani mahususi wa kuwajengea uwezo wa kujitegemea watu wenyewe ulemavu hasa Vijana, Watoto na Wanawake ili kuondoa utamaduni wa kuendesha maisha yao kwa kuombaomba?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Stella Ikupa Alex, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, naomba kujibu swalil Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Sensa ya Taifa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2012 iliyotolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu, idadi ya Watu wenyewe Ulemavu kwa kuzingatia makundi yao na kwa asilimia ni kama ifuatavyo:-

Watu wenyewe Ualbino ni 16,477 sawa na 0.04%; walemauvu wasioona ni 848,530, sawa na 1.93%; walemauvu ambaao ni viziwi ni 425,322, swan a 0.97%; walemauvu wa viungo ni 525,019, sawa na 1.19%; walemauvu wa kumbukumbu ni 401,931, sawa na 0.91%; walemauvu wa kujihudumia ni 324,725, sawa na 0.74%; na Ulemavu mwingine, yaani kwa ujumla wake ni 99,798, sawa na 0.23%. Kulinganisha na takwimu hizo jumla ya watu wenyewe ulemavu, kwa mujibu wa Sensa ya mwaka 2012 ni watu 2,641,802.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali hivi sasa inakamilisha zoezi la uanzishwaji wa regista ambayo itasaidia kupata takwimu sahihi ya watu wenyewe ulemavu katika maeneo yote ya mijini na vijijini. Faida nyingine ya kuanzisha regista hizi zitatusaidia pia kutambua sababu za kuongezeka kwa ulemavu katika kila eneo na changamoto zinazowakabili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha watu wote wenye ulemavu hasa vijana, watoto na wanawake hawaachwi nyuma kiuchumi, Serikali inaendelea kuwajengea uwezo kuhakikisha watoto wote ikiwa ni pamoja na wenye ulemavu wanapata elimu ya msingi na sekondari ili kuwajengea uwezo wa kujitegemea. Pia inatoa elimu na mafunzo ya ufundi stadi kwa makundi ya vijana na wanawake wenye ulemavu kupitia vyuo vya watu wenye ulemavu na programu ya kukuza ujizi hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, ili kuhakikisha watu wenye ulemavu wanawezeshwa kiuchumi, Serikali inatoa mkopo wa fedha ya asilimia mbili (2%) zinazotokana na mapato ya ndani ya Halmashauri. Hata hivyo, mipango yote ya uvezeshaji kiuchumi nchini ni jumuishi ikiwajumuisha pia watu wenye ulemavu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, swalii la nyongeza.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii adhimu ya kuuliza swalii la nyongeza. Kwanza, niipongeze Serikali kwa majibu mazuri ya kitakwimu na naamini kwa majibu haya na kuonesha kwamba tuna walemovu zaidi ya milioni mbili, itasaidia Serikali yetu kuja na mpango mkakati wa namna gani ya kuwasaidia. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa, hapo Dar es Salaam Mkuu wetu wa Mkoa alileta mpango kuleta vifaa vya kuwasaidia walemovu na walemovu wengi sana wakajitokeza, ikionesha kwamba kuna shida hiyo. Je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuhakikisha inawajengea uwezo walemovu, kwa maana wa viungo kuwaletea viungo ili wawe na uwezo wa kujitegemea wenyewe na wale wa kusikia wapate viungo vya kusikia ili waweze kujitegemea wenyewe na walemovu wengine? Pia, je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea uwezo ili kupunguza athali ya ulemavu kwa kutumia viungo bandia?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa mbona umeuliza kwa nini mbili hapo, kuna swali lingine tena! Maswali ni mawili tu na umeshataja kwa nini mbili, kwa hiyo maana yake maswali yako mawili, maana nisje nikakosea kanuni hapa itakuwa balaa. Mheshimiwa Ikupa Stella Alex, majibu!

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Maulid Said Mtulia, Mbunge wa Kinondoni kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeza Mheshimiwa Maulid Mtulia kwa jinsi ambavyo anafuutilia masuala ya watu wenyе ulemavu. Pia naomba niweze kumjibu Mheshimiwa Mbunge, kwamba Serikali imekuwa na mipango mingi kwa upande wa uwezeshaji kwa watu wenyе ulemavu, ikiwemo kuwapatia vifaa saidizi. Kwa sababu tunafahamu kwamba, mtu mwenye ulemavu, kulingana na aina yake ya ulemavu, asipowezeshwa kwa upande wa vifaa visaidizi, hawezi kujimudu. Kwa kuliangalia hilo, Serikali imekuwa ikitenga bajeti, lakini pia kwa kushirikiana na wadau mbalimbali, tumekuwa tukigawa vifaa visaidizi kwa watu wenyе ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kwa kundi hili la watu wenyе ulemavu, ili kuhakikisha kwamba wanaweza kufanya vizuri kama ambavyo nimeongea kwenye jibu langu la msingi, ni kwamba tumekuwa tukihakikisha kwamba tunawajengea uwezo kwa kuwawezesha katika maeneo mbalimbali, ikiwemo kuhakikisha kwamba pia hata *programmes* ambazo tunakuwa tunaziandaa zinakuwa ni jumuishi kwa watu wenyе ulemavu. Kwa hiyo, suala la vifaa kwa watu wenyе ulemavu, tumekuwa tukilifanya kama Serikali. Tunaona hata katika shule zetu, tumekuwa tukitenga bajeti ambayo tunanunua vifaa visaidizi na kuvigawa kwenye shule zetu, lakini haviishii tu kwenye shule, tunavipeleka hata kwa watu ambao siyo wanafunzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu ya nyongeza.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri, nataka niongezee kidogo katika majibu hayo. Kwanza Serikali imeondoa kodi katika baadhi ya vifaa saidizi kwa kutambua kwamba kuna kikundi ndani ya nchi yetu ambacho wanavihitaji vile vifaa na vinaweza vikawasaidia kuwa na maisha bora, kodi hizo katika baadhi ya vifaa zimeondolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nilikuwa nataka niwape taarifa tu Waheshimiwa Wabunge, kuanzia mwezi huu wa Aprili, Hospitali ya Mifupa *MOI*, wataanza zoezi la kufanya upimaji pamoja na kutoa vifaa, viungo bandia kwa baadhi ya wale walemavu ambao wanavihitaji. Kwa hiyo, naomba kupitia Waheshimiwa Wabunge kutoa taarifa kwa watu hawa ambao wanahitaji viungo bandia, basi kufika katika Hospitali ya Taifa, *MOI* kwa ajili ya kuweza kupata vifaa hivyo. Hata hivyo, katika masuala ya vifaa vyatya usikivu tumekuwa tunaendelea na kampeni katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili vyatya kupandikiza vifaa vyatya usikivu, lakini vilevile kutoa vifaa saidizi kwa wale watoto ambao wanahitaji vifaa hivyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anthony Komu, swalii la nyongeza.

**MHE. ANTHONY C. KOMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swalii dogo moja la nyongeza. Kwa kutambua mahitaji makubwa ya walemavu wananchi wa Moshi Vijijiini kwa kushirikiana na Padri Apolnarys Ngao ambaye anaishi Ujerumanii na marafiki zake kule Ujerumanii, tunajenga kituo kikubwa cha walemavu kule Parokia ya Mawela. Naomba kumuuliza Waziri kama atakuwa tayari kuja kuona hii jitihada, kuitambua na kuhamasisha michango zaidi ili kuweza kufanikishi hii nia njema? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, unaomba kwenda huko kwa Mheshimiwa Anthony Komu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Anthony Komu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa ameomba niweze kwenda kwenye hicho kituo ambacho kinaandaliwa sasa hivi, kwanza niwapongeze kwa hilo wazo jema kwa kundi hili la watu wenye walemavu. Mimi nikiwa kama Naibu Waziri mwenye dhamana hiyo, naomba niseme kwamba niko tayari.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Venance Mwamoto, Balozi wa Watu Wenye Ulemavu Nchini, swali.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri ambazo zinafanya na Serikali, kundi la watu wenye ulemavu limeongezeka na ni walemavu wa tofauti. Je, sasa Mheshimiwa Naibu Waziri atakubali kukutana na makundi hayo ili iwe rahisi kuwasaidia kwa sababu wana changamoto zinazotofautiana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (WATU WENYE ULEMAVU):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo, Balozi wa Watu Wenye Ulemavu, lakini pia babu yangu kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mwamoto, hajaanza leo kuhakikisha kwamba masuala ya watu wenye ulemavu yanakaa sawa, toka akiwa *DCanafanya* hivyo. Nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, nimefanya ziara nyngi hapa Tanzania kwenye mikoa mingi na katika zile ziara zangu, ni lazima nikutane na makundi ya watu wenye ulemavu. Kwa

hiyo, nimhakikishie tu kwamba, niko tayari kwa hilo ambalo amelizungumza.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tutaendelea, lakini Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya amesema Serikali imeondoa kodi kwenye baadhi ya vifaa vya watu wenye ulemavu. (*Makofii*)

Sasa badala ya kuwa na lile neno baadhi, madam vifaa ni vya watu wenye ulemavu, ni vizuri kwa kuwa sasa tunajadili, tuko kipindi cha bajeti ni vizuri kuhakikisha vifaa vinavyohitajika na watu wenye ulemavu vyote vinaondolewa kodi badala ya baadhi ya vifaa. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge tunaendela na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, Mbunge wa Viti Maalum, sasa alulize swali lake.

Na. 25

### **Mradi wa Maji katika Manispaa ya Morogoro**

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA** aliuliza:-

Serikali inajitahidi sana kukabiliana na tatizo la maji katika Manispaa ya Morogoro, lakini tatizo hilo lipo kwenye baadhi ya Kata:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya makusudi ya kumaliza tatizo hili katika Manispaa ya Morogoro?

### **NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Christine Gabriel Ishengoma, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuitia Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Morogoro (*MORUWASA*) inaendelea na uboreshaji wa huduma ya maji katika

Manispaa ya Morogoro kwa mipango ya muda mfupi na muda mrefu. Katika mipango ya muda mfupi, katika mwaka wa fedha 2018/2019, *MORUWASA* imetekeleza mradi wa uboreshaji wa huduma ya maji katika Kata za Kihonda na Mkundi. Mradi huo umegharimu kiasi cha shilingi bilioni 1.9 na umewanufaisha wakazi wapatao 17,000 wanaoishi maeneo ya Kihonda Kilimanjaro, Yespa, Kiegea na Kihonda Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mpango wa muda mrefu, Serikali kwa kushirikiana na Serikali ya Ufaransa kuitia Shirika la Maendeleo la *AFD* itatekeleza mradi wa kuboresha huduma ya majisafi katika Manispaa ya Morogoro. Kazi zitakazotekelawa ni kuongeza kina cha bwawa la Mindu, ujenzi wa mtambo wenye uwezo wa kusafisha na kutibu maji, upanuzi wa mtambo wa kusambaza maji, ukarabati wa mabwawa ya majitaka kwa gharama ya *Euro* milioni 70. Kwa sasa Wizara inasubiri kusainiwa kwa mkataba wa kifedha kati ya Wizara ya Fedha na Shirika la Maendeleo la Ufaransa la *AFD* kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Nashukuru sana kwa majibu ya Naibu Waziri, ni kweli muda mfupi umeanza ambao ni mzuri sana, ambao wanaweza wakatoa maji kwenye kata mbalimbali, lakini kuna Kata ya Magadu ambao waliahidiwa maji, ambao hakuna maji kabisa na ilikuwa wachimbiwe kisima cha muda mfupi angalau waweze kupata maji, lakini mpaka sasa hivi Kata ya Magadu wana shida sana ya maji. Je, ni lini wataweza kupatiwa hicho kisima au kuchimbiwa maji wakaweza wakapata maji?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, mradi huu ambao unafadhiliwa kwa *Euro* milioni 70 umechukua muda mrefu na tukiwa tunasubiri kwa muda mrefu wa miaka zaidi ya mitatu sasa tunaambiwa kuwa imebaki kusainiwa; je, kwa sababu wananchi wa Morogoro Manispaa wanategemea

maji yao kutoka bwawa la Mindu, kuna mkakati gani wa muda mfupi ambao Serikali inaweza ikafanya kukarabati bwawa la Mindu?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Aweso majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge, mama yangu, Mheshimiwa Christine Ishengoma, kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika kuhakikisha anawasemea wananchi wake wa Mkoa wa Morogoro. Kubwa ni kuhusu suala zima la maji katika Kata ya Magadu. Nimuagize tu Mhandisi wa Maji wa Mkoa, sisi ni Wizara ya Maji, siyo Wizara ya ukame, ahakikishe anasimamia suala hilli la uchimbaji wa kisima wananchi wa Magadu waweze kupata maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu suala zima la mradi huu mkubwa wa *Euro* milioni 70. Tunapozungumzia maji, ni rasilimali muhimu sana, lakini sasa hivi Morogoro kumekuwa na uhitaji mkubwa sana, uzalishaji wetu sisi ni lita milioni 30 lakini kutohana na ongezeko la watu pamoja na taasisi na viwanda, kumekuwa na uhitaji wa zaidi ya lita milioni 59 na ndio maana sisi kama Serikali tukaona haja sasa ya kuwekeza kwa maana ya kuongeza bwawa la Mindu, katika kuhakikisha kwamba linakuwa na uzalishaji mkubwa ili wananchi wa Morogoro waweze kupata maji safi, salama na kuweza kukuza uchumi wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kilio hiki cha muda mrefu, lakini kubwa nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, utekelezaji wa miradi ya maji unategemeana na fedha, kwa hiyo, pamoja na utoaji huu wa fedha lazima tufuate utaratibu. Nataka nimtie moyo kwamba wawe na subira, subira yavuta heri na heri itapatikana katika upatikanaji wa maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Roman Selasini, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Jimbo la Rombo lina shida kubwa sana ya maji, pamoja na hayo Serikali ina jitihada inazofanya kama za kupata maji katika Ziwa Chala, kupanua lile bomba kubwa linalotoa maji Marangu kuleta Rombo na kadhalika. Hata hivyo, shida hii inakuzwa sana na jinsi *KILIWATER* (Taasisi ya Wananchi) inavyogawa maji kule Rombo, inagawa kwa upendeleo, inagawa kwa baadhi ya watu, haifungii watu mita na kadhalika. Baraza la Madiwani...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selasini uliza swali tafadhali.

**MHE. JOSEPH R. SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Sasa kwa kuwa tulishaazimia taasisi hii iondolewe na Serikali ilishakubali; je, Mheshimiwa Naibu Waziri, yuko tayari kwa muda wake twende Rombo ili akakague shughuli za hii taasisi na kuipa amri ya kugawa maji kwa haki wakati hizo hatua nyingine zikiendelea kuchukuliwa na Serikali?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake zuri, lakini kubwa tunapozungumzia suala la maji, maji ni uhai na maji hayana mbadala na hakuna sababu ya kutoa maji kwa upendeleo. Nimwahidi niko tayari kuongozana na yeze katika kuhakikisha kama ipo changamoto hiyo tuweze kuitatua kwa haraka ili wananchi wa Jimbo la Rombo waweze kupata maji safi na salama. Ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Shukuru Kawambwa, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. SHUKURU J. KAWAMBWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza, pamoja na shukrani nyingi za wananchi wa Bagamoyo kwa Serikali kwa kuwajenye tanki kubwa la maji lita milioni sita Bagamoyo Mjini, naomba kuuliza swali la nyongeza kwamba, sasa ni lini shughuli ya mradi wa kusambaza au kulaza mabomba, mtandao huu mpya wa mabomba ya maji katika Mji wa Bagamoyo na Kata zinazozunguka Mji wa Bagamoyo utaanza kwa sababu tanki lile sasa hivi haliletii tija ya kutosha kwa wananchi wa Bagamoyo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua changamoto kubwa sana ya maji katika eneo la Dar es Salaam pamoja na Pwani kwa maana ya Bagamoyo, Serikali imewekeza zaidi ya dola milioni 32 katika kuhakikisha wananchi wa maeneo haya wanapata maji. Nimhakikishie, hii ni hatua ya kwanza na tunamwagiza Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Salama Dar es Salaam kuhakikisha mradi huu unaanza haraka ili wananchi wa Bagamoyo waweze kupata maji safi na salama.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada nzuri za Serikali kuwapatia wananchi maji, kuna mradi mmoja wa KfW wa tangu mwaka 2008 ambao ulikuwa uhudumie Mikoa saba ya Manyara, Babati, Mtwara, Kigoma, Lindi na maeneo mengine. Mikoa mingine mitano ilishapatiwa huduma ya maji bado Babati na Mtwara na tulikuwa tumepanganya shilingi bilioni 20 na kila mkoa shilingi bilioni 10. Mpaka sasa mradi huu haujasainiwa na wenzetu wa Ujerumani pamoja na

Serikali ya Tanzania. Naomba nifahamu ni lini mradi huu sasa utasainiwa kwa sababu tunahitaji hizo shilingi bilioni 10 zitusaidie kuondoa tatizo la maji Babati na Mtwara ambako kumesalia.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge wa Babati na mimi nilishafika Babati pamoja na huu mradi mkubwa lakini zipo jitihada pale za utekelezaji wa mradi wa maji. Nataka nimhakikishie, kama tulivyoahidi tutatekeleza lakini tutalifanya hili jambo kwa haraka ili wananchi wake wa Babati waweze kupata maji safi na salama. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, swali la nyongeza.

**MHE. DKT. MARY M. NAGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ilivyo Morogoro naishukuru sana Serikali kuona tatizo la Mji Mkuu wa Wilaya ya Hanang na kuweza kuwapangia zaidi ya shilingi bilioni 2. Naomba kuuliza naona kama speed ni ndogo, je, mradi ule utafikisha maji kata 20 kwa sababu wanachotaka kuona wananchi wanakunywa maji na wanatumia maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge mama yangu Mheshimiwa Dkt. Mary Nagu, maeneo yenye changamoto kubwa sana ni katika jimbo lake lakini sisi kama Serikali tuna mradi mkubwa sana pale ambao tumeuwekeza kwa ajili ya kutatua tatizo la maji Hanang. Nataka nimhakikishie sisi kama Wizara na viongozi wa Wizara hii tunamwagiza mkandarasi lazima afanye kazi usiku na mchana, kama atashindwa

kufanya kazi ile kwa haraka sisi tutamwondoa tutamweka mkandarasi ambaye anaweza kufanya ile na kuweza kukamilisha mradi kwa mujibu wa mkataba kama ulivyopangwa. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Kilimo, Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, sasa aulize swali lake.

Na. 26

**Changamoto Zinazowakabili Wakulima wa  
Zao la Tumbaku**

**MHE. MARGARET S. SITTA** aliuliza:-

Moja kati ya changamoto zinazowakabili wakulima wa tumbaku katika Wilaya ya Urambo ni madeni yanayotokana na mikopo ya pembejeo ikiwemo mbolea:

(a) Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuwasaidia wakulima kuepukana na changamoto hii?

(b) Je, Serikali ina mkakati gani wa kushusha bei ya pembejeo ili kumsaidia mkulima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu wa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L.  
BASHUNGWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Margaret S. Sitta, lenye vipengele (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kuanzia mwaka 2008, Serikali imeboresha mfumo wa upatikanaji wa pembejeo za zao la tumbaku kwa wakulima kupata pembejeo kuitia vyama vya ushirika tofauti na ilivyokuwa

kabla ya mwaka 2008 ambapo pembejeo za tumbaku zilitolewa kuitia kampuni zinazonunua tumbaku kwa kuwakopesha wakulima na kuwakata wakati wa mauzo. Utaratibu huo ulikuwa na changamoto kadhaa ikiwa ni pamoja na riba kubwa isiyo na tija kwa mkulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuondokana na madeni yatokanayo na riba za mkopo wa pembejeo, Serikali imewahamasisha wakulima kuitia vyama vyao vya ushirika kuainisha mahitaji ya pembejeo mapema na wamekubali kukatwa kiasi cha fedha kutokana na mauzo ya tumbaku ili kuagiza pembejeo hizo kwa wakati. Mfano Chama cha Msingi cha Kahama (KACU) wamekubaliana kukatwa Sh.60 kwa kila kilo kwa lengo la kukusanya takribani shilingi bilioni 3 zitakazotosheleza kuagiza asilimia 75 ya mahitaji ya pembejeo. Utaratibu huo unafanyika kwa vyama vyote ambapo wakulima watanufaika kwa kupata bei ndogo kullko ile ya kukopa.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Mfumo wa uagizaji Mbolea kwa Pamoja (*Bulk Procurement System - BPS*) ulianzishwa kwa lengo la kupunguza gharama au kodi kwa wakulima. Hata hivyo, mfumo huo unategemea bei ya mbolea iliyopo katika soko la dunia kwa wakati huo. Kutokana na changamoto za ongezeko la bei ya mbolea katika soko la dunia, Serikali inasimamia Mfumo wa Uagizaji wa Mbolea kwa pamoja ili kuhakikisha kuwa wakulima wakiwemo wa zao la tumbaku wanapata pembejeo kwa wakati na kwa bei nafuu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Margaret Sitta, swali la nyongeza.

**MHE. MARGARET S. SITTA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza, naomba uniruhusu nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa jitihada kubwa ambazo amechukua kusaidia zao la tumbaku kwa kuja kila wakati katika Mkoa wa Tabora. Pili, naomba nimshukruu pia Naibu Waziri kwa jibu zuri kwamba wataagiza mbolea kwa pamoja yaani *bulk*

*procurement ili kusaidia kupunguza bei lakini kufika kwa wakati. (Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza, upatikanaji au uagizaji wa mbolea kwa wakati unategemea sana makisio. Je, Serikali inachukua hatua gani ili kuhakikisha kwamba makisio yanatolewa mapema ili mbolea iweze kuagizwa mapema na imfikie mkulima kabla ya mwezi Agosti?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, mkulima anapata moyo wa kulima kutokana na bei anayotegemea kupata. Je, Serikali ina mkakati gani wa kupata wanunuzi wengi zaidi ili soko lipatikane kwa wakati na kwa ushindani ili angalau mkulima apate bei inayoweza kumsaidia kumudu maisha na kazi kubwa anayoifanya ya kulima tumbaku? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta, Mbunge wa Urambo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niwapongeze wananchi wa Urambo kwa kuchagua Mbunge jembe. Mheshimiwa Mama Sitta anawahangaikia sana. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia namwagiza Mrajisi wa Tume ya Maendeleo ya Ushirika afike Urambo haraka iwezekanavyo acae na Mkuu wa Wilaya ili waangalie namna bora ya kuratibu utaratibu wa kukusanya madeni kwa wakulima wa tumbaku hasahaha wale wakulima ambao wanadaiwa lakini wanaendelea na kilimo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ni kuhusu kufanya makisio mapema. Naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge mama Sitta pamoja na wananchi wake kwamba Serikali tumejipanga kuhakikisha makisio ya wanunuzi yanafanyika mapema ili wakulima waweze kujua ni kiasi gani cha mbolea wanatakiwa kuagiza na mbolea iwafikie kabla ya mwezi Agosti, kama alivyoomba Mheshimiwa Mbunge. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ni kuhusu mkakati wa kuongeza wanunuzi. Naomba niwajulishe Waheshimiwa Wabunge na wakulima wetu kwamba kwa upande wa zao la tumbaku tayari Serikali tumekaa na wanunuzi waliopo na kuangalia changamoto zao ambazo tukizitatua zitawawezesha kununua tumbaku zaidi lakini tunaendelea kuongea na nchi ambazo zina mahitaji ya tumbaku ikiwemo China na Misri. Kwa hiyo, kwa mikakati hiyo Serikali itaweza kuwasaidia wakulima wa tumbaku kupata soko la uhakika na zaidi na kwa kufanya hivyo tutakuwa tumewasiaidia kuhakikisha tumbaku yao inatakiwa na inagombaniwa na wahitaji na kufanya hivyo kutasaidia kuchochaea bei kupanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Paschal Haonga, swali la nyongeza.

**MHE. PASCHAL Y. HAONGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Changamoto za zao la tumbaku zinafanana kabisa na changamoto zinazokabili zao la kahawa. Suala hili la pembejeo hasa mbolea imekuwa ni tatizo kubwa sana kwa sababu wakulima wa kahama wengi wanashindwa kulima kahawa vizuri, wanashindwa kuhudumia mashamba ya kahawa kwa sababu ya bei kubwa ya mbolea. Licha kwamba Serikali inatumia Mfumo wa Ununuzi wa Mbolea wa Pamoja lakini bado hajawa suluhi kwa wakulima wa zao la kahawa. Je, ni lini sasa Serikali itajenga viwanda vyta mbolea nchini ili angalau sasa mbolea iweze kushuka bei na wakulima

wa kahawa waweze kunufaika na uzalishaji uweze kuongezeka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Haonga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie nafasi hii kumkaribisha Mheshimiwa Haonga pamoja na Wabunge wengine, leo tuna kikao cha wadau wa kahawa kinafanyika hapa Dodoma, kimeanza saa mbili na nusu. Kwa hiyo, baada ya maswali na majibu tunawakaribisha Waheshimiwa Wabunge kushiriki kikao hiki na tuweze kupata maoni yenu ili kuboresha mfumo wa ununuzi wa kahawa hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la Mheshimiwa Haonga la lini Serikali itajenga viwanda vya mbolea, majibu ya Serikali ni kwamba inaendelea kufanya kila jitihada kuhakikisha tunajenga viwanda vya mbolea hapa nchini ikiwemo utumiaji wa gesi asilia ambayo tumeigundua ili kutengeneza mbolea na kusaidia wakulima wetu waweze kupata mbolea hapa hapa nchini na kwa bei nafuu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Almas Maige, swali la nyongeza.

**MHE. ALMAS A. MAIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kuniruhusu na mimi niulize swali moja la nyongeza kuhusu tumbaku kwa sababu tumbaku Tabora ndio siasa yenye. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vyama vingi vya msingi vimekufa au vimesinzia au havifanyi kazi kutokana na mfumo wa zamani uliokuwepo na hasahaha utoroshaji wa tumbaku, kukwepa madeni kuititia vyama vya IF. Sasa mfumo mzuri umewekwa na kwamba madeni yamedhibitiwa. Je, Serikali kuititia Benki ya Kilimo haiwezi kuwadhamini wanachama

hawa wa vyama sinzia ili vilime tumbaku kwa mkakati wa kulipa madeni? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Almas Maige, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze kwa ufatiliaji wake wa karibu wakulima wake wa tumbaku. Swalii la Mheshimiwa Maige ni kwamba *TADB* inawasaidiaje wakulima kupitia vyama vya msingi. Jibu ni kwamba Serikali inaendelea kufanya jitihada kwanza ya kufufua vyama vya msingi viweze kuzingatia utawala bora (*good governance*) kwani kwa kipindi cha nyuma vyama vya msingi baadhi ya viongozi walikuwa siyo waadilifu kwa hiyo fedha nyingi zilikuwa zinapotea kwa njia hiyo kwa sababu walishindwa kuzisimamia vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mkakati wa Serikali wa kuboresha ushirika na kuhakikisha vyama vya msingi vinakuwa na viongozi waadilifu basi tumhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tutakaa na *TADB* na kuangalia ni namna gani tunaweza tukaratibu jambo hili ili wakulima kupitia vyama vya msingi waweze kupata mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, swalii la nyongeza.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Bado narudi kwenye swalii la msingi la Mheshimiwa Margaret Simwanza Sitta kuhusu tumbaku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama alivyojibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwenye kalenda ya Bodi ya Tumbaku ili pembejeo zifike nchini mwezi Agosti na Septemba,

makisio hutolewa tarehe 31 Machi, ndiyo *deadline*. Sasa makisio yametolewa kwa makampuni matatu ambayo yanafanya biashara hapa nchini; kampuni moja hajatoa makisio, hiyo ina maana wakulima wa Tabora, Chunya, Ruvuma, Mpanda watakosa kulima tumbaku msimu ujao. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari kuitisha kikao cha dhararu kati ya Bodi ya Tumbaku na Wabunge wanaolima tumbaku ili kutatua tatizo hilo? (*Makofi*)

**MBUNGE FULANI:** Yes. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwambalaswa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nakubaliana na ye ye kwamba kukaa na wanunuzi kufanya makisio mapema iwezekanavyo ikiwezekana mapema mwezi Machi, ni jambo la msingi kwani litasaidia wakulima wetu kujuu ni kiasi gani wanahitaji kuagiza kupitia *bulk procurement system*.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali ni kwamba tuko tayari kukaa na huyu mnunuzi mmoja ambaye bado hajatoa makisio? Jibu ni kwamba Mheshimiwa Mwambalaswa niko tayari na baada ya hapa nitatafuta namba zao na kuwapigia simu na kuona kwa nini mpaka sasa hawajatoa makisio kwa wakulima wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk Mbunge wa Tanga Mjini, kwa niaba yake Mheshimiwa Sonia uliza swali.

Na. 27

### **Hitaji la Soko la Muhogo**

**MHE. SONIA J. MAGOGO (K.n.y. MHE. MUSSA B. MBAROUK)** aliuliza:-

Wakazi wa Kata ya Kirare, Tongoni, Mzizima, Chongoleani, Mabokweni na Pongwe Wilayani Tanga Mjini ni wazalisaji wakubwa wa zao la muhogo lakini hawana soko la uhakika:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani wa kutafuta soko la uhakika wa zao la muhogo ndani na nje ya nchi?

(b) Zipo mashine za kuchakata muhogo lakini bei zake ni kubwa na hivyo wakulima hawana uwezo wa kununua; je, Serikali haioni haja ya kuondoa kodi katika mashine hizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu wa swali hilo.

### **WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mussa Bakari Mbarouk, Mbunge wa Tanga Mjini, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, imeweka vipaumbele vitatu ambavyo ndivyo tunavyoviwekea msisitizo wa uwekezaji kwenye sekta ya viwanda. Vipaumbele hivyo ni viwanda vyatya kusindika mazao ya kilimo ili kuongeza thamani sambamba na kulinda jasho la mkulima; viwanda vyatya kutengeneza bidhaa za majumbanii kama vyakula, nguo, mafuta ya kula, samani na kadhalika na bidhaa tegemezi kwenye sekta ya ujenzi kama sementi, mabati na kadhalika ili kuharakisha ubora wa maisha na maendeleo; viwanda vinavyoajiri watu wengi kwa ajili ya kuhakikisha ajira kwa vijana.

Mheshimiwa Naibu Spika, zao la muhogo ambalo ni maarufu kwenye mikoa ya Dar es Salaam, Tanga, Pwani, Lindi, Mtwara na maeneo mengi ya nchi hadi Kigoma kwa sasa limepewa kipaumbele maalum duniani. Kutokana na ukweli kwamba muhogo hausindikwi kutengeneza unga wa ugali au uji au mkate au biskuti peke yake bali unga wa muhogo unatumika kwa sasa kwenye uunganishaji wa chuma, mbao, kutengeneza gundi na matumizi mengine mengi sana. Soko la muhogo Ulaya, Marekani na China ni kubwa sana kwa sasa. China peke yake inahitaji tani milioni mbili na nusu za muhogo kwa mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ukweli huo, kasi ya ujenzi wa viwanda vya kusindika muhogo ni kubwa. Mwaka huu peke yake ukiacha viwanda vitano vinavyonunua muhogo wa mkullma kwa sasa kikiwemo kile Kilichopo Handeni, viwanda viwili vipyta vitakuwa vimefunguliwa kabla ya Juni, 2019 kimoja Lindi na Kingine Pwani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bei kubwa za mitambo kutoka nje, nawashauri wawekezaji wa ndani watembelee *SIDO* na *TEMDO* kwanza maana ni taasisi za ndani ambapo mionganoni mwa majukumu yake ni kubuni na kutengeneza mitambo na mashine za kusindika mazao zenyen garama nafuu. Endapo italazimika kuagiza nje ya nchi, italazimu kufuata Sheria ya Fedha iliyopo au kusubiri mapendelekezo yaliyopelekwa kwenye Kikosi Kazi cha kutathmini mapendelekezo ya marekebisho ya kodi yatakayojadiliwa wakati wa kujadili rasimu itakayoletwa na Serikali Bungeni Juni, 2019.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sonia Magogo, swalii la nyongeza.

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyogeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza, kwa kuwa wakulima wengi wa mihogo ni wadogowadogo na hawana mitaji na wamehamasishwa na wawekezaji kulima zao hili kwa wingi, je, Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia wakulima hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, vilevile napenda kujua Serikali ina mpango gani wa kuwasaidia elimu wakulima hawa ili waweze kuzalisha zao hili kwa wingi na kwa kiwango kinachohitajika?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Sonia Magogo, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza kwamba wakulima wengi ni wadogo, hawana mitaji, kwa kweli hilo sio kwenye sekta ya kilimo cha muhogo peke yake bali wakulima wetu wengi hapa Tanzania hasa hawa wadogowadogo wanalima kilimo cha kawaida, kilimo cha kutegemea mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la muhimu zaidi ni pale alipouliza katika sehemu ya pili ya swalii lake kuhusu elimu, hilo ndilo jambo la muhimu zaidi kwa sababu elimu itahusu kilimo bora cha muhogo, utafiti na kutumia mbegu bora. Kwa hiyo, tunashirikiana kwa karibu sana sisi mapacha, Wizara ya Kilimo na Wizara ya Viwanda kuhakikisha kwamba mkulima anaongeza uzalishaji kutokana na ile elimu atakayopata kutoka kwa Maafisa Ugani walioko kwenye kata na vijiji. Hilo ndiyo jambo la msingi sana. Waziri wa Kilimo ameshaagiza Maafisa Kilimo wote nchini wale ambao hawajayajua vizuri mazao fulani kwenye maeneo yao wanatakiwa wapatiwe mafunzo wao wenye kwanza kabla hawajaenda kuwapatia wakulima. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf, swalii la nyongeza.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf swali la nyongeza.

**MHE. YUSSUF SALIM HUSSEIN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na jitihada za Serikali kuona inainua kilimo hiki au zao hili la muhogo ambalo ni tegemeo kubwa hususan kwa watu wa Mikoa ya Kanda ya Mashariki, lakini zao la muhogo linakabiliwa na magojwa ya *Cassava Mill Bags*. Je, nini kauli ya Serikali kukabiliana na wadudu hawa ambao wanaathiri sana zao la muhogo ambalo linawarudisha nyuma wakulima wanaolima zao hili? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Yussuf hilo ni swali la Wizara nydingine ndiyo maana naona Mheshimiwa Waziri anageuka nyuma kuona Mheshimiwa Waziri wa Kilimo yuko wapi amsaidie kujibu. Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Alichokisema ni kweli kabisa na haya masuala ya magonjwa ya mazao siyo kwamba yapo kwenye kilimo cha muhogo peke yake, bali mazao mengi yamekuwa yakiathiriwa sana na wadudu. Mheshimiwa Waziri wa Kilimo ameshatoa msisitizo na ametoa maagizo kwamba viuatilifu ambavyo ni feki visitumike kwenye mazao. Yeyote ambaye atakamatwa anauza au anampatia mkulima viuatilifu feki ambavyo havisaidii kupambana na magonjwa na wadudu atachukuliwa hatua kali na Serikali. Kwa hiyo, hiyo ni elimu mojawapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imechukua hatua za makusudi kabisa na kupitia vituo vya utafiti kikiwemo Kituo cha Utafiti cha Naliendele na kituo cha utafiti ambacho kipo chini ya Wizara ya Kilimo cha pale Dar es Salaam wamefanya utafiti mzuri wa mbegu ambayo inahimili magonjwa kama hayo. Kwa hiyo, msisitizo ni kutumia mbegu ambazo zinahimili matatizo hayo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Justine Monko, swali la nyongeza.

**MHE. JUSTIN J. MONKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo walilonalo wananchi wa Tanga linafanana sana na tatizo walilonalo wananchi wa Mkoa wa Singida. Jimbo la Singida Kaskazini na Mkoa wa Singida kwa ujumla ni wakulima wakubwa sana wa vitunguu pamoja na alizeti. Hivi tunavyozungumza, soko la kitunguu gunia moja linauzwa kati ya shilingi 10,000/= mpaka shilingi 40,000/=, badala ya shilingi 80,000/= mpaka shilingi 120,000/= ilipokuwa katika msimu wa mwaka uliopita. (*Makofii*)

Je, Serikali iko tayari kuingilia kati suala hili na kuwanusuru wananchi ambao wanaendelea kupata hasara kutokana na kazi kubwa waliyofanya?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli alichokisema. Kwanza tunatoa tahadhari kwa Watanzania, wakulima pamoja na wafanyabiashara, lipo tatizo hapa nchini ambalo ni kubwa, watu wanakuja katika vijiji kununua, wengine wananunua kwenye mashamba bila kufuata utaratibu. Hilo tunashirikiana na Wizara ya Kilimo na tunashirikiana na Shirika la Vipimo kuhakikisha kwamba utaratibu wa kisheria unafuatwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hao watu ambao wamekuwa wananunua halafu wanasafrisha nje ya nchi bila kuwa na vifungashio vinavyokubalika kisheria, hao wanakiuka sheria na kwa kweli itabidi tuchukue hatua kali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuingilia kati suala la bei, namuahidi Mheshimiwa Mbunge kwamba tutaingilia kati na tutatoa maagizo kwa maandishi kuanzia leo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, hiyo hoja ya vifungashio ipo kwenye mazao mengi. Unaona Wabunge wamesimama hapa, wengine wangesimama kuhusu vifungashio vya viazi kwao. Kwa hiyo, mliangalie kwa ujumla wake na pia watu wenu wa vipimo mwongee nao kwa sababu kuna mazao yanaharibikia kwenye yale maeneo ambayo wameweka sehemu za kupimia hivyo vifungashio. (*Makof*)

Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, sasa aulize swalilake.

Na. 28

### **Barabara ya Isandula (Magu) hadi Hungumalwa**

**MHE. RICHARD M. NDASSA** aliuliza:-

Usanifu wa kina wa barabara ya Isandula (Magu) – Bukwimba *Station* – Ngudu hadi Hungumalwa ambayo ni kilometra 74 umeshakamilika:-

Je, ni lini barabara hiyo itaingizwa kwenye bajeti ili ijengwe kwa kiwango cha lami?

### **NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalilake Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, Mbunge wa Sumve, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Isandula hadi Hungumalwa yenye urefu wa kilometra 71 ni Barabara ya

Mkoa inayohudumiwa na Wizara yangu kuititia Wakala wa Barabara Nchini (*TANROADS*). Barabara hii inapita katika Mji wa Bukwimba, Nyambiti na Ngudu na ni barabara muhimu katika kukuza uchumi wa Wilaya za Magu, Sumve na Ngudu. Barabara hii pia ni kiungo katika ya barabara kuu ya Mwanza – Sirari na Mwanza – Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua umuhimu huo, Wizara yangu inaifanya upembuzi yakinifu na usanifu wa kina barabara hiyo kwa lengo la kuijenga kwa kiwango cha lami. Kazi ya usanifu wa kina inatarajiwa kukamilika mwezi Mei, 2019. Baada ya usanifu huo kukamilika na gharama kujulikana, barabara hiyo itaingizwa kwenye mpango wa ujenzi kwa kiwango cha lami kutegemeana na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati ujenzi huo wa kiwango cha lami ukisubiriwa, Wizara yangu kuititia Wakala wa Barabara Nchini (*TANROADS*) itaendelea kuifanya matengenezo barabara hiyo kuhakikisha kuwa inapitika majira yote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, swali la nyongeza.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na maelezo mazuri sana ya Serikali, barabara hii imekuwa na maelezo ya muda mrefu kwa maana ya kwamba kuna ahadi ya Mheshimiwa Rais wa Awamu ya Nne na Rais wa Awamu ya Tano kwamba barabara hiyo itatengenezwa kwa kiwango cha lami. Kwa maelezo ya Mheshimiwa Waziri anasema kwamba usanifu wa kina utakamilika Mei, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Barabara Mkoa wa Mwanza. Usanifu wa kina umeshakamilika na baada ya usanifu wa kina kukamilika nilienda kwa Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, ofisini kwake, akaniahidi kwamba ataiiingiza kwenye bajeti ya mwaka huu kwa maana ya 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nataka kuuliza, kwa maelezo haya, Barabara ya Isandula – Hungumalwa itaingizwa kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha 2019/2020? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili. Kama ahadi inatolewa na Mheshimiwa Rais na Serikali imekiri kwamba barabara hii ni muhimu na ni kiungo kikubwa kwa Sirari, Mwanza na Shinyanga: Je, Serikali sasa kwa umuhimu huo, iko tayari barabara hii ambayo ni muhimu kuingiza kwenye bajeti ya mwaka huu wa fedha? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza unipe ruhusa nimpongeze sana Mheshimiwa Richard Ndassa, Senator huyu, amekuwa akiifuatilia sana barabara hii na ni kweli barabara hii imeahidiwa muda mrefu na ni kweli kabisa Mheshimiwa Mbunge amekuwa akiifuatilia sana barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa umuhimu huo, tumesimamia vizuri kuhakikisha kwamba usanifu unakamilika. Tulipokea rasimu ya kwanza ya usanifu wa barabara hii ambayo angalau *ime-indicate* kwamba barabara hii inaweza ikawa na gharama gani. Kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Ndassa avute subira na kwa sababu jambo hili tumelishika na turnedhamiria kujenga barabara hii na sisi tunaitazama barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika swalii lake la pili amezungumza juu ya bajeti, niseme tu kwamba asiwahishe shughuli, tunaitazama vizuri barabara hii, na Mungu akijaalia tunaweza tukaja na mapendekezo ya kujenga barabara hii. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Ndassa pamoja na wananchi wa Isandula, Bukwimba, Nyambiti, Ngudu, Nyamilama, Hungumalwa (Magu), Sumve na Ngudu kwa ujumla kwamba tunaona umuhimu wa kujenga barabara

hii. Tukipata fedha na bajeti ikeruhusu tutaijenga barabara hii kwa kiwango cha lami. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joyce Sokombi, swali la nyongeza.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii ya kuuliza swali la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mara kuna tatizo kubwa sana la barabara hasa barabara ya Wanyele – Kitario. Barabara hii imekatika, hakuna mawasiliano. Barabara ile inahitaji kujengewa daraja na barabara hiyo pia ilishaua watoto zaidi ya 20:-

Je, ni lini Serikali itaweka mkakati wa kipaumbele kuhakikisha inajenga daraja na tukichukulia kwamba kipindi cha masika kinakaribia? Ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inao utaratibu wa kutenga fedha kushughulikia maeneo korofi kama hayo ambayo Mheshimiwa Mbunge anayataja. Namwomba tu Mheshimiwa Mbunge, labda tuwasiliane baadaye kwa sababu ni eneo limekuwa mahsus na kwa wakati huu tuone kama lipo tatizo kwa kuititia utaratibu ambao tupo nao wa kushughulikia maeneo korofi na kuhakikisha wananchi wanapata huduma ya barabara wakati wote, tuweze kushughulikia eneo hili. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge ili niipate sawasawa tuweze kushughulikia eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Na. 29

## **Kukamilika Ujenzi wa Barabara ya Kyaka hadi Benako**

**MHE. OLIVER D. SEMUGURUKA** aliuliza:-

Barabara ya Kyaka – Kasulu hadi Benako Ngara  
imeishia Bugene:-

Je, ni lini barabara hiyo ya lami itajengwa hadi  
Benako?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Oliver Daniel Semguruka, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (Buneko) yenye urefu wa kilometra 178 ni barabara kuu na inahudumiwa na Wakala wa Barabara Nchini (*TANROADS*) Mkoa wa Kagera.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua umuhimu wa barabara hii kiuchumi na kijamii iliamua kujenga barabara hii kwa kiwango cha lami kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Awamu ya kwanza ilihuisha sehemu ya barabara toka Kyaka hadi Bugene (Nyakahanga) yenye urefu wa kilometra 59.1. Sehemu hiyo tayari imekamilika kujengwa kwa kiwango la lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, awamu ya pili inahusisha sehemu ya barabara kutoka Bugene hadi Kasulo (Benako) yenye urefu wa kilometra 118.9. Sehemu hii kwa sasa inafanyiwa upembizi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Kazi hii ipo katika hatua za mwisho chini ya Mhandisi Mshauri *LEA International Ltd* ya Canada ikishirikiana na *LEA*

*International Ltd ya Asia Kusini. Kazi hii inagharamiwa na Jumuiya ya Nchi za Afrika Mashariki na itajengwa kuititia mradi huo.*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati sehemu hiyo ikitubiriwa kujengwa kwa kiwango cha lami, Wizara itaendelea kutenga fedha kwa ajili ya kufanya matengenezo mbalimbali ili kuhakikisha kuwa barabara hii inapitika vizuri majira yote. Katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya shilingi milioni 650.371 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo mbalimbali ya barabara hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Daniel Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. OLIVER D. SEMGURUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi. Ninayo maswali mawili ya nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali, wananchi wamesubiria fidia kwa muda mrefu sana na kabla ya ujenzi wa lami, fidia huwa inatangulia. Sasa Serikali inawaambiaje wananchi wangu wanaoishi kwenye hii barabara kuanzia Nyakahanga, Nyaishozi, Nyakasindi hadi Benako Ngara? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Bugene kuititia Nkwenda – Kaisho - Mlongo ni barabara muhimu sana kwa wananchi wa Karagwe, Kyerwa na Misenyi. Je, ni lini Serikali itajenga barabara hii muhimu kwa uchumi wa Wilaya hizi na Taifa kwa ujumla. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimwia Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu kwa maswali hayo.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO  
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) :** Mheshimiwa Naibu Spika, ni utaratibu wa Serikali kulipa fidia kwanza kabla ya kuanza ujenzi. Kwa hiyo, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba wananchi wa maeneo haya ambapo mradi utapita watalipwa fidia zao kabla ujenzi haujaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia nimpongeze sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia mambo mbalimbali ya maendeleo katika eneo lake lakini pia niwapongeze wananchi kwa kupisha mradi; kwa maana hiyo kwamba kutoa ushirikiano kwa Serikali kwa ajili ya maendeleo yetu kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swalı lake la pili, amezungumza juu ya barabara hii ambayo inakwenda Mrushaka – Mlongo kilometra 125. Mimi nimetembelea eneo hili, ni eneo muhimu sana sasa kuunganishwa kwa sababu ni sera ya Serikali kuunganisha nchi yetu na nchi za jirani. Barabara hii Mheshimiwa Mbunge anaitaja inatuunganisha sisi Tanzania na Uganda. Kwa hiyo, tunayo mipango ya kuijenga kwa kiwango cha lami lakini namwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira, asiwhishe shughuli na ikiwezekana tunaweza kuteta ili ajue mpango wa Serikali juu ya kuijenga barabara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, tunaendelea kuihudumia hii barabara na maeneo ambayo ni korofi. Kwa mfano, ile milima, maeneo ya Rwabunuka kuna mipangilio ya milima ambayo ni mikali sana. Tumetenga fedha kwa ajili ya kuanza kushughulikia maeneo korofi wakati tunajiendaa kuiboresha hii barabara katika kiwango cha lami.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge na wananchi wa maeneo haya wavute subira, tumejipanga vizuri na tunafahamu maeneo haya ni muhimu sana kwa uchumi. Tutashughulikia barabara hii muhimu. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Goodluck Mlinga, swalı la nyongeza.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalı langu linahusu barabara ya Kidatu – Ifakara; barabara yenye urefu wa

kilometa 69.9. Mradi wake wenyе thamani ya shilingi bilioni 109 ambaо unafadhiliwa na *DFID* na *European Union*.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ilifunguliwa tarehe 5 Mei, 2018. Wakati inafunguliwa vifaa viliwekwa vingi na Mheshimiwa Rais lakini Mheshimiwa Rais alipoondoka na Mkandarasi akaondoa vifaa vyake. (*Kicheko*)

Je, Serikali inatuambia nini kuhusu barabara hii? Ina maana ndiyo tumepigwa changa la macho sisi pamoja na Mheshimiwa Rais?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) :** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze sana Mheshimiwa Mlinga kwa sababu mara zote amekuwa ukifuatilia sana ujenzi wa barabara hii. Niseme tu kwamba tunawaambia nini wananchi na Watanzania kwa ujumla kuhusu barabara hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tulivyoanza ujenzi wa barabara hii kulikuwa na changamoto kuhusu vifaa na *materiаl* kwenye ujenzi wa barabara hii. Hii ilitokana na mabadiliko ya Sheria ya VAT, kwa hiyo, tulichelewa kidogo. Niwaambie wananchi na Mheshimiwa Mbunge kwamba baada ya changamoto hizi kutatuliwa, sasa Mkandarasi atakwenda kwa kasi kubwa na wananchi wategemee kupata barabara ya lami, bora na itakayowahudumia wananchi wa maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante (*Makofи*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swalı lake.

Na. 30

### **Kukithiri kwa Vitendo vya Ukatili kwa Watoto**

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR** aliuliza:-

Vitendo vya ukatili kwa watoto vimezidi kuendelea kwa kasi siku hadi siku kama vile ubakaji, kunajisiwa kwa watoto wa kiume na kuingiliwa kinyume na maumbile watoto wa kike:-

Je, ni lini Serikali italeta Muswada wa Sheria Bungeni ili kurekebisha sheria hiyo iwe kali zaidi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla sheria zilizopo zinajitosheleza kabisa kuwashughulikia wale wote wanaokutwa na hatia katika makosa ya ubakaji, kunajisi watoto wa kiume na wa kike. Sheria ya Makosa ya Jinai ya mwaka 1985, kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002, imeelekeza adhabu kali kwa yejote atakayebainika kutenda kosa la kumdhahilisha mtoto au kumbaka mtoto ikiwemo kifungo cha miaka 30.

Hata hivyo, imekuwa vigumu kuwatia hatiani wakosaji hawa kwa sababu wengi wanatoka ndani ya familia na kwa kukosekana ushahidi ikizingatiwa matukio mengi hufanywa na watu walio karibu na familia. Wengi wao wanaogopa kutoa ushahidi kutokana na hofu ya kupoteza mmoja wa wanafamilia kutokana na adhabu za vifungo vya maisha.

Aidha, kutokana na mtazamo hasi wa jamii, familia nyingi huhofia kudhalilika na kunyanyapaliwa baada ya kubainika mkosaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inajitahidi kuweka mikakati ya kusaidia kupunguza au kumaliza kabisa tatizo hili, lakini bila ushirikiano katika ngazi zote kuanzia familia haitakuwa rahisi. Serikali inatoa rai kwa jamii kutomaliza masuala ya ukatili wa kijinsia ndani ya familia na badala yake ishirikiane na Serikali ili sheria ichukue mkondo wake.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar, swali la nyongeza.

**MHE. ZAINAB MUSSA BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa maswali mawili ya nyongeza. Swali langu la kwanza; Serikali wamesema wameweka mikakati, nataka kujua ni mikakati ipi ambayo wameweka ili kupunguza ama kumaliza tatizo hili?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili ni kwamba; kwa kuwa tatizo hili ni kubwa sana na kesi mbalimbali zinapelekwa mahakamani na baadhi ya kesi watuhumiwa wanashinda kutokana na kwamba kuna vitu ambavyo vinakosekana kama vile shahawa ama majimaji ambayo yanalingana na yule mwanaume ambaye amembaka au kumnajisi mtoto, je, Wizara ya Afya imeshusha mwongozo gani kuwashushia Madaktari ili kuwaongoza waweze kupima vitu kama hivyo ili wananchi wasikate tamaa kupeleka kesi zao mahakamani na kushindwa? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu kwa swali hilo muhimu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Zainab Mussa Bakar kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kubaini ukubwa wa tatizo na nianze kwa kutoa takwimu tu kwamba kati ya Januari mpaka Desemba, 2017 tulikuwa na matukio 41 ya ukatili wa kijinsia na kati ya hayo, 13,000 yalikuwa ni masuala ya ukatili dhidi ya watoto. Sisi kama Serikali tumeandaa mpango mkakati wa kuzuia ukatili wa jinsia dhidi ya wanawake na watoto ambao unaithwa MTAKUWA wa mwaka 2017/2018 ambao unaisha mwaka 2021/2022. Katika mkakati huu tumejielekeza katika maeneo makubwa yafuatayo:-

Moja, kuanzisha Kamati za Ulinzi na Usalama wa Wanawake na watoto ambapo mpaka sasa hivi kuna kamati zaidi ya 10,000 tumezianzisha katika ngazi mbalimbali kuanzia Taifa, Mikoa, Wilaya na katika ngazi ya Halmashauri hadi katika Kata; kuanzisha madawati ya jinsia ndani ya Jeshi la Polisi zaidi ya madawati 400 tumeshaanzisha. Sambamba na hilo, kumekuwa na kuanzhwa na mahakama maalum za watoto ili mashauri ya watoto yaweze kukaa na kusikilizwa. Tunaendelea kushauriana na Wizara ya Elimu kuhakikisha kwamba kunakwa na Walimu walezi ambao wanaweza wakatoa ushauri nasaha na kupokea baadhi ya mashauri kwa watoto ule ukatili ambao wanafanyiwa wakiwa majumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu kama nilivyoeleza katika jibu la msingi ni kwamba mashauri mengi tunashindwa kuyafikisha mwisho kwa sababu wanaofanya ukatili huu ni watu ambao wako ndani ya familia. Kwa hiyo, nami nitoe rai kwa jamii kwamba tusiyamalize mashauri haya kifamilia na badala yake turuhusu mkondo wa kisheria uweze kuchukua nafasi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalilake la pili, ameelezea kwamba kushindwa kwa baadhi ya kesi kwa sababu ya ushahidi wa kitaalam kutoka kwa wataalam wetu wa afya. Hili tumeshalitolea maelekezo kwa wataalam wetu wote wa afya na tumeweka msisitizo mkubwa sana kwamba mtu ye yote katika Sekta ya Afya ambaye amepewa jukumu la kuthibitisha vipimo ambaye atakwenda kinyume na misingi

na miiko ya maadili ya taaluma hatutasita kumfungia na kumfutia leseni ya Udaktari.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Rose Tweve, swali la nyongeza.

**MHE. ROSE C. TWEVE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Tatizo la ubakaji na ulawiti kwa watoto bado ni changamoto kubwa sana, hasa kwa Mkao wetu wa Iringa. Sasa wenzetu wa Chuo cha Mkwawa na *RUCO* walifanya utafiti na walibaini kuwa wazazi na walezi wamekuwa wanaachwa na mzigo mkubwa sana kugharamia matibabu ya watoto hao.

Je, Serikali haioni umuhimu sasa kuweka utaratibu maalum kwa matibabu, ukizingatia hawa watoto huwa wanaachwa na *physical damage* na *psychological damage* kubwa ili waweze kuwalea watoto hawa?

Mheshimiwa Nabu Spika, nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Rose Tweve kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto tulishalitolea tamko suala hili kwamba wahanga wote wa ukatili wa kijinsia Serikali itatoa matibabu bure.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 31

## **Hitaji la Madaktari Hospitali ya Mkoa ya Mtwara**

**MHE. TUNZA I. MALAPO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka Madaktari wa kutibu magonjwa mbalimbali katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara ya Ligula?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Tunza Issa Malapo, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto imeajiri Madaktari 11 katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mtwara katika ajira mpya za mwezi Julai, 2018. Kwa sasa hospitali imeshapokea Madaktari nane na kufanya jumla ya Madaktari wa kada kuwa 17. Sanjari na hilo, katika kupunguza tatizo la uhaba wa Madaktari Bingwa, Hospitali ya Ligula kwa kupitia utaratibu wa kuendeleza watumishi wake inatarajia kumpokea Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Koo, Pua na Maskio (*ENT Surgeon*) ambaye anatarajija kumaliza mwezi Oktoba, 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2017/2018, Wizara iliwapeleka Madaktari Bingwa wa fani ya Upasuaji wa Kawaida na Mifupa (*General Surgeon na Orthopaedic Surgeon*) katika Chuo cha Muhimbili ambapo wanatarajia kumaliza katika kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021. Aidha, Wizara itaendelea kutenga bajeti ya kuwasomesha Madaktari Bingwa wa fani mbalimbali ili

kufikia azma ya Serikali na kuhakikisha kwamba hospitali zote za rufaa za mikoa zinakuwa na Madaktari Bingwa wa kutosha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Musukuma, swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimeomba swali la 31.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Tunza Malapo, samahani, swali la nyongeza.

**MHE. TUNZA I. MALAPO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mimi nina maswali mawili madogo ya nyongeza. Swali langu la kwanza; nataka tu kujua katika ile Hospitali ya Mkoa ya Ligula kuna Madaktari Bingwa wangapi na wanatibu magonjwa gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa hospitali ile ni ya mkoa, maana yake inahudumia mkoa mzima na ni ya rufaa na sisi hatuna hospitali ya kanda, Kanda ya Kusini, bado haijaanza kufanya kazi.

Katika jibu lake la msingi amesema Madaktari wa kufanya upasuaji wa kawaida na mifupa bado wapo masomoni wanasona na ukizingatia kuna ajali nyingi zinazotokea, anawaambia nini vijana, wananchi wa Mtwara ambao wanapata matatizo, wanataka tiba ya upasuaji wa kawaida na mifupa; wasubiri mpaka mwaka 2021? (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Tunza Malapo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya Mtwara, Ligula tuna Daktari Bingwa

mmoja katika Magonjwa ya Akinamama, lakini tunatambua kwamba tunahitaji huduma za Madaktari Bingwa katika hospitali zetu za rufaa za mikoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sasa tulitangaza nafasi hizi Madaktari hawa hawako mtaani na ndiyo maana sisi kama Serikali tumewekeza katika kuhakikisha kwamba tunatoa mafunzo kwa Madaktari Bingwa wengi iwezekanavyo na tumeendelea sasa hata kufanya mabadiliko ya mifumo ya kufundisha Madaktari ili tuweze kupata Madaktari Bingwa wengi kwa utaratibu wa *fellowship* ambao na sisi ndani ya Wizara tunakwenda nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo, kwa lengo la kutibu changamoto ambazo tunazo Serikali imekuwa inafanya kambi mbalimbali za kutoa Madaktari Bingwa kutoka sehemu moja kwenda kwenye sehemu mbalimbali na hii tumekuwa tunafanya kwa kushirikiana na Bima ya Afya na kwenda katika kambi katika mikoa mbalimbali kuhakikisha kwamba zile huduma za dharura ambazo zinahitaji upasujaji nazo zinaweza zikafanyiwa kazi wakati tunasubiria kujenga uwezo wa kuwa na Madaktari Bingwa wengi zaidi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumalizie swalii la mwisho Wizara ya Madini...

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ulinitamka.

**NAIBU SPIKA:** Umesema sio swalii hili Mheshimiwa Musukuma.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo hili alikuwa anauliza mwenye swalii la msingi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer Christopher Kajoro Chiza*, Mbunge wa Buyungu.

Na. 32

## **Utafiti Juu ya Uwepo wa Madini – Wilaya ya Kakonko**

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA** aliuliza:-

Katika Wilaya ya Kakonko kuna wachimbaji wadogo wa madini aina ya dhahabu katika Vijiji vya Myamwilonge, Nyakayenzi, Ruhuru na kuna dalili za kuwepo madini hayo katika sehemu nyingine. Aidha, kuna madini ya chokaa katika Milima ya Nkongogwa ambayo yana matumizi mengine ya viwandani:-

Je, Serikali imejipangaje kufanya utafiti wa uwepo wa madini na kuwasaidia wachimbaji ili wayachimbe na kujipatia kipato?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Madini, napenda sasa nijibu swali la Mheshimiwa *Engineer Christopher Kajoro Chiza*, Mbunge wa Buyungu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Taasisi ya Jiolojia na Utafiti wa Madini Tanzania ilifanya tafiti zifuatazo:-

(i) Upimaji na utafiti wa jiolojia ulifanyika mwaka 1960 na kuchora ramani ya jiolojia ya *QDS (Quarter Degree Sheet)* namba 43 pale Kakonko.

(ii) Utafiti wa pili ulifanyika mwaka 1978 – 1980 Serikali ilifanya utafiti wa jiofizikia kwa kutumia ndege na kufanya uchakataji wa takwimu zilizochukuliwa na hatimaye kuainisha maeneo yenye mipasuko ya miamba inayoashiria uwepo wa madini mbalimbali katika maeneo ya Kakonko na taarifa hizo zipo katika Ofisi ya *GST (Geological Survey of Tanzania)*.

(iii) Utafiti wa tatu ulifanywa kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo ikiwemo Mradi wa *Nordic Fund*, Kampuni ya *Beak Consultants* ya Ujerumanu na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kati ya mwaka 2003 na 2014 walifanya utafiti wa jiosayansi na kubainisha yafuatayo:-

- (a) Uwepo wa madini ya dhahabu katika Kata ya Muhange, Kijiji cha Mwiluzi, Nyamtukuza, Nyamwilonge, Msekwa/ Galama, Kasela na Kata ya Kasuga katika Kijiji cha Nyakayenzi; na;
- (b) Madini ya *agate* katika Kata za Kasanda, Kijiji cha Nkuba, Kata ya Gwanumpu katika Kijiji cha Kabingo na Kata ya Nyamtukuza katika Vijiji vya Nyamwilonge na Kasela.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara kupitia *Geological Survey of Tanzania* inakamilisha uandaaji wa kitabu cha madini yapatikanayo katika toleo la nne ambacho kinaonesha uwepo wa madini katika mikoa, wilaya na vijiji, hivyo kitasaidia wananchi na wachimbaji wadogo katika kutambua madini yaliyopo katika maeneo yao na matumizi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, Serikali kupitia *Geological Survey of Tanzania* itaendelea kufanya tafiti zaidi za kijiosayansi katika mwaka 2019/2020 kwenye maeneo ya Ruhuru na Nkongogwa katika Wilaya ya Kakonko ili kubaini madini yaliyopo katika maeneo hayo. Pia itatoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu njia bora za uchimbaji na uchenjuaji ili waweze kuelewa kuhusu jiolojia na madini yaliyopo kwenye maeneo yao na kuwashauri namna bora ya kufanya uchimbaji na uchenjuaji salama wenye tija kwa lengo la kuhakikisha kuwa wananchi wanafaidika na rasilimali ya madini iliyopo katika maeneo yao.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Christopher Chiza, swali la nyongeza.

**MHE. ENG. CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Naibu

Waziri, majibu yanaleta matumaini. Nina swali moja tu kwa Mheshimiwa Naibu Waziri; kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri Bunge liliopita aliniahidi yeye mwenyewe jua linawaka kwamba angefuatana na mimi kwenda kuwasaidia wananchi hawa ambao tayari wameanza kuchimba madini haya, lakini bahati mbaya mambo yakawa mengi.

Sasa kwa kuwa wananchi hawa wameanza kuchimba madini kwa kutumia nyenzo duni, utaalal duni na wakati mwingine hata hawajui uzito wala *purityya* madini; je, sasa anawaahidi nini wananchi hawa ambao wameanza kuchimba madini ili waweze kutumia sasa fursa hii na fursa za masoko ya madini ambayo yamefunguliwa kama lile la Geita ambalo amezindua Waziri Mkuu juzi, anawaahidi nini hasa katika uwezeshaaji waweze kufanya shughuli hii kwa ufanisi zaidi? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa *Engineer Chiza* kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikubaliane na yeye kwamba nilimuahidi kweli nitakwenda Kigoma, hasa maeneo ya jimbo lake. Mimi tu nipende kusema kwamba nitashiriki naye, nitakwenda, tutakwenda hadi kwa wachimbaji, tutakwenda kufanya kazi na tutakwenda kuwaelimisha na kuwapa maelekezo ya Serikali yanavyostahili. Kwa hiyo kwa hilo mimi sina tatizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusiana na suala la wachimbaji wadogo. Kweli tuna matatizo makubwa sana ya kimitaji, teknolojia, maeneo, tafiti kwa wachimbaji wadogowadogo. Sisi kama Wizara ya Madini tumejipanga vizuri na tumeamua sasa hivi kuititia *Geological Survey of Tanzania* pamoja na *STAMICO* tutaendelea kufanya tafiti mbalimbali ambazo zitawasaidia wachimbaji wadogowadogo ili tuweze kuwapa yale maeneo ambayo

tukiwapa tunakuwa na uhakika kwamba wataweza kupata madini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ninapozungumza *STAMICO* tayari tumekwisha kununua *rig machine* ambayo inaweza kufanya kazi ya *drilling* kwa wachimbaji wadogo kwa gharama ndogo. Kwa hiyo tunawaomba wachimbaji wadogowadogo waje waombe maombi yao katika Wizara yetu tuwafanyie tafiti mbalimbali kwa gharama ndogo kwa sababu kufanya tafiti ni gharama kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile tunaendelea kutoa elimu ya uchimbaji, uchenjuaji, na uwepo wa masoko haya ambalo Mheshimiwa Waziri Mkuu amelifungua kule Geita na lingine juzi nimekwenda kufungua pale Kahama na maeneo mengine, tunaendelea na mikoa yote ambayo inakwenda kufungua masoko ya madini. Tunakwenda kuhakikisha kwamba wachimbaji wadogo wanapata ile tija ambayo wanadhamiria kuipata tofauti na sasa hivi walikuwa wanakwenda kuuza katika masoko ya pembedi wanadhlumiwa, wanaauza kwa bei ndogo, vilevile wanaabiwa. Sisi kama Wizara ya Madini tumejipanga kuwasaidia wachimbaji wadogowadogo kwa kuhakikisha kwamba wanapata tija. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wetu umekwisha. Kabla sijasoma matangazo tuliyonayo leo niwakumbushe tu; kwa kuwa hili ni Bunge refu na mlisahasomewa maelezo kwenye *Briefing*, maswali yatakuwa zaidi ya 500 kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge wale ambao hamjapeleka maswali yenu mpeleke ili usijisikie vibaya sana kama hukupewa swalii la nyongeza.

Pia jambo lingine ni kujitahidi kwa sababu ya muda wetu, maswali ni machache, tujitahidi kuuliza maswali yale ambayo yanahusiana na swalii la msingi.

Sasa nianze na wageni walioko Bungeni siku ya leo; wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunao wageni wawili wa Mheshimiwa Khatib Said Haji ambao ni ndugu zake kutoka

Jijini Dar es Salaam, ndugu Nuru Masoud na ndungu Sofia Mrisho, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Rose Kamili ambaye ni mtoto wake kutoka Usa River Arusha, ndugu Jovita Cyprian, karibu sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Yahaya Massare ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Kata ya Mbandu, ndugu Lameck Mwamkamba, karibu sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Esther Nicholas Matiko ambaye ni mpigakura wake kutoka Jimbo la Tarime Mjini, ndugu Nicholas Saronge, karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Godwin Mollel ambaao ni viongozi wa CCM na Serikali kutoka Jimbo la Siha. Wa kwanza ni Mheshimiwa Onesmo Buswelo ambaye ni Mkuu wa Wilaya ya Siha, karibu sana; tunaye pia Mheshimiwa Godson Ngomuo ambaye ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Siha. Waheshimiwa Wabunge naambiwa huyu ni Mwenyekiti mpya kabisa aliyechaguliwa. Pia yupo Mheshimiwa Valerian Juwal ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Siha, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni 22 wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambaao ni Wajumbe wa Kamati ya Hamasa ya Michango ya Timu ya Yanga pamoja na Wasanii wa Filamu na Muziki ambaao ni mashabiki wa Yanga ... (*Makofi/Vigelegele*)

Waheshimiwa Wabunge, ngoja nirudie tangazo tutulie basi. (*Kicheko*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** *TASAF, TASAF.* (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Ngoja nirudie tangazo. Wageni 22 wa Mheshimiwa Seif Gulamali ambaao ni Wajumbe wa Kamati ya Hamasa ya Michango ya Timu ya Yanga pamoja na Wasanii wa Filamu na Muziki... (*Makofi/Vigelegele*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** *TASAF, TASAF.*

**WABUNGE FULANI:** Bakuli, bakuli. (*Makof!*)

**NAIBU SPIKA:** Ambao ni mashabiki wa Yanga kutoka Jijini Dodoma wakiongozwa na Katibu wa Kamati hiyo, Eng. Deo Mutta. Karibuni sana. (*Makofi!*)

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** *TASAF, TASAF. (Kicheko)*

**NAIBU SPIKA:** Yupo pia mgeni wa Mheshimiwa Cosato Chumi ambaye ni Mtangazaji wa *Azam TV* na *UFM Radio* kutoka Jijini Dar es Salaam, Ndugu Mussa Kawambwa. Karibu sana. (*Makofi!*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Fredy Mwakibete ambaye ni Katibu wa *Busokelo Development Organization* Ndugu Aliko Brown. Karibu sana. (*Makofi!*)

Tunao pia wageni ambao wapo Bungeni kwa ajili ya mafunzo na hawa ni wanafunzi watatu kutoka Shirika la Arise Amka Arise ya Jijini Arusha, ambao wamekuja kujifunza jinsi Bunge linavyofanya kazi. Karibuni sana. (*Makofi!*)

Waheshimiwa Wabunge, yapo matangazo mengine hapa, tangazo la kwanza linatoka kwa Mheshimiwa Venance Mwamoto ambaye ni Mwenyekiti wa Tawi la Yanga Bunge, leo kuna matangazo mengi sana ya Yanga hapa na mashabiki wa Simba muwe mnapiga makofi kwa sababu Yanga wanawapigia pia. (*Makofi!*)

Waheshimiwa Wabunge, tangazo hilo linahu uzinnduzi wa Kampeni ya Uchangiaji *Young Africans Sports Club*. Uongozi wa Tawi la Yanga hapa Bungeni unapenda kuwakaribisha Wabunge na wadau wote wenyewe maslahi na mapenzi na klabu yao wanaombwa kufika kesho siku ya Jumamosi tarehe 6 Aprili, 2019 katika Ukumbi wa Morena. Kamati hiyo iliyo chini ya Mwenyekiti, Naibu Waziri wa Vijana Mheshimiwa Antony Mavunde imekwishawasili Jijini Dodoma.

Wote mnakaribishwa ikiwa ni pamoja na wapenzi wa Simba ili muweze kuwasaidia Yanga. (*Makofi/Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, lipo pia tangazo lingine linatoka kwa Katibu wa Bunge, mnatangaziwa kwamba kwenye *pigeonholes* zenu mmewekewa nakala za vitabu vya Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka 2019/2020 kwa mchanganuo ufuatao: *Financial Statement and Revenue Estimate Volume I; Public Expenditure Consolidated Fund Services and Supply Votes Ministerial Volume II; Public Expenditure Supply Votes Regional Volume III;* na *Public Expenditure Estimates Development Votes Part A.* Kwa hiyo, mnashauriwa mpitie kwenye *pigeonhole* zenu mchukuwe vitabu hivi muanze kuvipitia wakati mjadala ukiendelea.

Waheshimiwa Wabunge, lipo pia tangazo la *Capital City Marathon*, mnatangaziwa kwamba siku ya kesho tarehe 6 Aprili, 2019 saa kumi na mbili asubuhi kutakuwa na *Capital City Fun Run* ya kilometer 10 hapa Dodoma. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge wote ikiwa ni kuunga mkono agizo la Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan la mwezi Desemba, 2016 mnakaribishwa sana kushiriki katika mbio hizi ambazo sasa zinafanyika kwa mara ya tisa. Zitafanyika kwenye barabara ya 18, Jakaya Kikwete eneo la kuanzia ni Jengo Jipya la PSSSF mpaka Mlima wa Chuo Kikuu Dodoma (*UDOM*).

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo, siku ya kesho mnakaribishwa sana lakini pia wakati mkienda mnaombwa muende na Sh.5,000 kwa sababu mtahudumiwa huko. Pia kutakuwa na kupima bure magonjwa yasiyo ya kuambukiza. Kwa hiyo, baada ya mbio hizi kutakuwa na kupima pia magonjwa ni muhimu tukashiriki, mnakaribishwa sana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya matangazo hayo tutaendelea na utaratibu wa leo.

## **MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ali Keissy.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwa kuwa Wana-Yanga wamekuja hapa kwa ajili ya kuchangisha, naomba wamkabidhi Ndugu Seif au Mheshimiwa Mwamoto kikapu ili tuwachangie. Kama hiyo haiwezekani, namwomba Mheshimiwa Mkuchika awaingize katika Mfuko wa *TASAF* unaosaidia kaya maskini wawe wanachangiwa. (*Kicheko/Makof*)

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo haujapokelewa, umefutwa. (*Kicheko*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Frank Mwakajoka.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba Mwongozo wako kuititia Kanuni ya 68(7). Sasa hivi tuko kwenye Bunge la Bajeti na mwezi Februari, Mheshimiwa Waziri wa Fedha aliletta Mpango wa Bajeti wa mwaka 2019/2020 lakini pia kulikuwa na Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna magazeti yalitoa taarifa ya fedha za washirika wa maendeleo ambao walikuwa wanatakiwa kutuchangia, tulikuwa tunatakiwa kupata karibu shilingi trilioni mbili, bilioni mia moja na thelathini nukta tisa kwa mwaka 2018/2019 lakini fedha ambazo zimetoka mpaka kipindi hiki alichokuwa analeta taarifa Mheshimiwa Mpango ilikuwa ni shilingi bilioni mia moja na arobaini na nne. Vyombo hivi vya *Citizen* pamoja na Mwananchi walisema kwamba fedha hizi ni sawa na asilimia 7.6 ambazo washirika wa maendeleo wamechangia. Hata

hivyo, Msemaji wa Serikali alikataa na alitoa taarifa kwamba vyombo hivi vimetoa taarifa ambazo siyo sahihi akasema kwamba taarifa zilizoko sahihi ni kwamba washirika wa maendeleo wametoa asilimia karibuni 67.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka tupate taarifa sahihi, kama makadirio ya fedha ilikuwa shilingi triliioni 2.13 na fedha zilizotoka ni shilingi bilioni 144, ipi ni sahihi kati ya hizi asilimia kama shilingi bilioni 144 ni asilimia 67 au ni asilimia 7.6 kama ambavyo vyombo vilitoa taarifa hizo ili wananchi waweze kujua usahihi uko wapi.

**MBUNGE FULANI:** Mwongozo wa Spika.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa miogozo miwili hapa mmoja na Mheshimiwa Keissy na mwingine na Mheshimiwa Frank Mwakajoka. Mheshimiwa Keissy amezungumza kuhusu kuichangia Yanga na mwongozo wake anazungumzia kapu kuletwa hapa kutokana na matangazo yaliyokuwepo. Kwa kuwa wote tunamfahamu Mheshimiwa Keissy na kuhusu michango nadhani tumkubalie Mheshimiwa Keissy kwa maana ya kwamba tukatwe fedha... (*Makofi*)

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Tusikilizane Waheshimiwa Wabunge.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Kapu lipite.

**MBUNGE FULANI:** Tukatwe shilingi 50,000.

**MBUNGE FULANI:** Tukatwe zote.

**MBUNGE FULANI:** Tukatwe shilingi 100,000.

**WABUNGE FULANI:** Hatutaki.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nimeombwa Mwongozo hapa na kwa sababu jambo hili linahusu Wabunge kuridhia. Kwa mujibu wa Mheshimiwa Keissy, napendekezo lake nitawahoji. (*Makofi*)

**WABUNGE FULANI:** Hatutaki.

**MBUNGE FULANI:** Tukatwe, tukatwe.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tunajua wewe ni Simba.

**MBUNGE FULANI:** Keissy, Keissy. (*Makofi/Kicheko*)

**MBUNGE FULANI:** Hoji, hoji, hoji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane vizuri.

**MBUNGE FULANI:** Kata posho.

**MBUNGE FULANI:** Hakuna.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Peleka *TASAF*.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane.

**MHE. JOSEPH K. MUSUKUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, tuhoji.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane. Mheshimiwa Keissy ameniomba Mwongozo na kwa sababu jambo hili linahitaji maamuzi ya Wabunge wenyewe, sasa nitawahoji kuhusu utayari wenu wa kuchangia Timu ya Yanga.

**WABUNGE FULANI:** Simba, Simba, Simba.

**WABUNGE FULANI:** Yanga, Yanga, Yanga

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tusikilizane nitoe uamuzi, waliokataa wameshinda. (*Makofi/Vigelegele/Kicheko*)

*(Hoja Ilitolewa Iamuliwe)  
(Hoja Iliamuliwa na Kukataliwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, pia nimeombwa Mwongozo na Mheshimiwa Frank Mwakajoka, ametoa maelezo marefu ambayo sikusudii kuyarudia lakini kwa sababu sote tunafahamu Kanuni zetu zinataka Mwongozo uombwé kwa jambo ambalo limefanywa ama limezungumzwa hapa ndani mapema leo.

Kwa hiyo, hilo analolizungumza halijatokea kwenye maswali wala kwenye matangazo ya siku ya leo, hivyo, Kiti hakina Mwongozo wa jambo hilo.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, Katibu.

**NDG. ATHUMANI HUSSEIN – KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 - Ofisi ya Waziri Mkuu**

*(Majadiliano yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na mjadala kuhusu hoja ya Mheshimiwa Waziri Mkuu inayohusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi yake kwa mwaka 2019/2020. Nimeletewa majina hapa ya wachangiaji kwa kadri ya uwiano wetu ulivyo, tutaanza na Mheshimiwa Mbaraka Dau atafuatiwa Japhary Michael.

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa fursa hii. Nianze kusema kwamba naunga mkono hoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu jana kwa namna nzuri sana aliyowasilisha makadirio ya Wizara yake kwa uweledi mkubwa sana. Jana mama yangu Mheshimiwa Anna Kilango alizungumza suala la uwekezaji na nashukuru kwa kuwa suala la uwekezaji hivi sasa lipo katika Ofisi ya Waziri Mkuu na tuna Waziri pale wa Nchi, nami katika mchango wangu nitajikita kwenye maeneo hayo hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utalii, kuna kitu kinaitwa uwekezaji wa utalii wa katika eneo linaloitwa *Southern Circuit*, eneo la Ukanda wa Kusini. Nimeipitia ile *document*, sina uhakika sana kama Mheshimiwa Waziri wa Utalii yupo lakini kwa kiasi kikubwa sana hakuna maeneo yoyote yanayozungumzia ama kujadili utalii katika fukwe za pwani. Utalii kwa Kanda ya Kusini kuanzia Tanga mpaka Mtwaru kule Msimbati, tuna fukwe nzuri sana kwa ajili ya utalii lakini hii *document* inayohusiana na *Southern Circuit* hakuna sehemu yoyote inazungumzia utalii wa fukwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, unapozungumzia utalii wa fukwe huwezi kukiacha kukizungumzia Kisiwa cha Mafia. Kisiwa hiki ni mionganoni mwa visiwa vizuri sana katika pwani ya Afrika Mashariki. Kina maeneo ya fukwe mazuri kabisa, kuna *scuba diving, sport fishing*, ni maeneo mazuri sana kwa uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa masikitiko makubwa sana Kisiwa cha Mafia ambacho sisi wenyewe tunaita ni *New Zanzibar*, kina *offer* mambo mazuri yote ambayo Zanzibar ina *offer* na pengine hata mimi naonekana ni Mbunge ninayetokea Zanzibar kwa sababu Kisiwa cha Mafia kinanasibishwa sana na mambo yanayoendelea kule Zanzibar. Tunatakiwa tuwekeze ili tuifungue Mafia kwani haitambuliki. Pamoja na vivutio vyote vizuri, Mafia inapata watalii wasiozidi 6,000 kwa mwaka wakati Zanzibar inapata watalii kwa malaki, sina takwimu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nini kifanyike? Pengine huo ndiyo ushauri wangu ambao Mheshimiwa Waziri wa

Uwekezaji katika Ofisi ya Waziri Mkuu ningeomba unisikilize. Tunahitaji kufungua Kisiwa cha Mafia lakini unafikaje Mafia wakatu usafiri ni shida? Tuna kiwanja cha ndege pale kina urefu wa *ran way* ya kilomita 1.6 ambayo katika hali ya kawaida ndege kubwa haziwezi kutua. Ningeomba sana Waheshimiwa na nimekuona Mheshimiwa Naibu Waziri wa Uchukuzi pale Kwandikwa, kwa nini msiangalie uwezekano wa kuongeza *ran wayya* Uwanja wa Ndege wa Mafia kutoka kilometra 1.6 kwenda mpaka kilometra 3 na kuruhusu ndege kubwa ziweze kutua pale na kuweza kukifungua kisiwa cha Mafia kwa utalii? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Zanzibar inapata watalii wengi kwa sababu hiyo. Watalii wanakuja na ndege moja kwa moja kutoka nchi za Magharibi na kutua pale Zanzibar lakini ili ufile Mafia lazima utue Dar es Salaam halafu tena uingle kwenye ndege ndogo ndogo na kuja Mafia ambapo watalii wengi hawapendi kadhia ya aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kushauri sana katika namna nzuri na bora ya kufungua Kisiwa cha Mafia ule uwanja wa ndege uangaliwe. Kuna *terminal building* ndogo sana, *runway* yetu pale ni ndogo sana Mheshimiwa Naibu Waziri uweze kuangalia ni namna gani mnaweza mkaongeza *runway* ili Kisiwa cha Mafia kiweze kufikika kwa urahisi na ndege kubwa ziweze kutua sambamba hata na ndege yetu ya *bombardier*. Kwa urefu tuliokuwa nao sasa hivi, ndege ya *bombardier* inaweza ikatua pale lakini bado hawajaanza hizo safari.

Mheshimiwa Naibu Spika, llingine ni *accessibility* kuititia kwenye bahari. Tuna ugomvi wa gati pale wa muda mrefu kidogo, gati la Nyamisati. Tunaishukuru sana Serikali imetutengea fedha na ujenzi umeshaanza pale na tunatarajia ujenzi ule utakamilika ndani ya miezi miwili au mitatu ijayo lakini kukamilika kwa gati la Nyamisati kutakuwa hakuna maana yoyote iwapo Serikali haitatupatia boti ya kisasa ili watu sasa waweze kulitumia gati la Nyamisati sambamba na gati la Kilindoni ili kuunganisha maeneo haya mawili na wananchi waweze kusafiri bila matatizo yoyote.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni barabara. Ndani ya Kisiwa cha Mafia kuna barabara yenye urefu wa kilometa 55, inaitwa Kilindoni kwenda Rasi Mkumbi. Usanifu na upembuzi wa kina umeshakamilika. Naishukuru sana Serikali mambo haya yamekamilika kama miezi miwili, mitatu iliyopita. Sasa kilichobaki ni kutengewa fedha kwa ajili ya kuwekewa lami. Hii nimelisema sana, tatizo linakuja pale kwamba *periodical maintenance* ya barabara ile inakuwa ni gharama kubwa sana kwa sababu kile ni kisiwa, kuweza kupata udongo, udongo unakaribia kwisha. Itafika wakati sasa ili kufanya *periodical maintenance*, inabidi udongo uutoe Dar es Salaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunamwomba sana Mheshimiwa Kwandikwa nimemwona, waangalie uwezekano wa kuiwekea lami barabara hii ili haraka sana tuweze kuondokana na kadhia hii ya kuwa na wasiwasi labda huenda huko mbele udongo ukaisha tukashindwa kufanya *periodical maintenance*. (*Makofii*)

Lingine ni suala la Uwekezaji katika bahari kuu. Namshukuru sana Mheshimiwa Spika katika ile Kamati yake ya kuangalia namna gani nchi inaweza ikanufaika na rasilimali yetu ya bahari kuu; mimi nilikuwa ni mmoja wa Wajumbe wa Kamati ile. Tumeyaona mambo mengi sana na nimekuona ndugu yangu Mheshimiwa Ulega. Tulizungumza sana na wewe mwenyewe unalifahamu sana hili suala la *blue economic*. Kwanini Serikali sasa tusinunue meli ya uvuvi yetu wenyewe?

Mheshimiwa Naibu Spika, meli ya uvuvi gharama yake haitazidi sana, ni baina ya dola milioni moja mpaka dola milioni sita, hapa katikati kulingana na uwezo wetu wa kibajeti. Ninaamini kwa Serikali yetu hii hatushindwi kununua walau meli mbili ama tatu. Suala la uwekezaji katika Bahari Kuu ni zuri sana. Kule huhitajiki kulima kama vile unavyoandaa shamba. Mwenyezi Mungu ameshalima, wewe unakwenda na kapu lako kuvuna tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa  
Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa. Kengele ya pili imeshagonga. (*Makofi*)

**MHE. MBARAKA K. DAU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Japhary Michael, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Mbarouk. Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, ajiandae.

**MHE. RAPHAEL J. MICHAEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia Makadirio ya Bajeti ya Hotuba ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Jambo la kwanza ninalotaka kuishauri Serikali, ni suala la mapato ya Serikali ikiwa ni pamoja na kuimarisha uwekezaji katika sekta binafsi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maoni yangu, mojawapo ya eneo ambalo limekuwa ni kikwazo cha kuimarisha sekta binafsi katika nchi hii, ni viwango vya kodi katika nchi yetu. Viwango vyetu vimeduwa ni kichocheo kikubwa cha kufanya wafanyakishara wengi na wawekezaji wengi wakwepe kodi. Bahati nzuri nimeshaona jitihada zinazofanyika kusukuma hili suala la kupunguza viwango vya kodi. Nilikuwa naiomba Serikali illfanye jambo hili kwa haraka iwezekanavyo ili iweze kuwa kichocheo cha wananchi kulipa kodi na kwa maana hiyo kuwekeza kwa kiwango kinachoridhisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kodi katika nchi hii imeduwa kama ni silaha ya kuadhibu baadhi ya watu ambao inawezekana wakawa na maoni tofauti au wakawa na mitazamo tofauti na Serikali hii. Sasa badala ya kodi kuwa sehemu ya kichocheo cha kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata mapato ya kuendelea na kuweza kujiendeleza vizuri, kodi imeduwa sasa ni sehemu ya kuonyesha kwamba kama mtu ametofautiana na Serikali au ametofautiana na mtu yejote katika Serikali, basi inakuwa kama ni adhabu, kwa

sababu viwango vyake vimekuwa vikubwa, kwa hiyo, vinamfanya kila mtu akikutana na mtu wa *TRA*, aone ni afadhali angekutana na simba kuliko kukutana na mtu wa *TRA*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani ni vizuri tuvirekebishe viwango vyetu nya kodi ili vilipike na visiwe ni kichocheo cha kuwa kama adhabu kwa watu wengine ambao wanaonekana kwamba wanapingana na mitazamo fulani na fikra fulani za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili katika suala hili hili la uwekezaji, ni namna ambavyo kodi imekuwa ikilipwa na kundi fulani la watu wachache katika nchi hii. Bahati nzuri nimesikia Mheshimiwa Rais juzi akitoa takwimu kwamba mpaka sasa hivi tunavyozungumza Tanzania ina watu wasiozidi 2,700,000 kati ya watu millioni 55 ambao ni walipa kodi. Maana yake bado tuna kundi kubwa la watu ambao bado wako nje ambao hawalipi kodi. Inawezekana hatujafanya jitihada kubwa za kuwafanya hawa watu waingie.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai yangu ni kwamba, kwa sababu kuna huo msisitizo wa Mheshimiwa Rais ni vizuri tuhakikishe kuwa tunasukuma ili watu wengi zaidi waingizwe kwenye utaratibu wa kulipa kodi ili tupunguze mzigo huu kwa watu wachache ambao sasa imefanywa kodi kuwa kama adhabu kwa watu fulani katika Taifa letu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nizungumzie suala la vitambulisho nya wajasiriamali wadogo. Kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amedhani kwamba mpango huu utasaidia makusanyo ya mapato katika Halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika na Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kuwaambia kuwa vitambulisho hivi kwa sasa tena siyo msaada kwa Halmashauri zetu bali ni tatizo kwa Halmashauri zetu kuhusu suala la mapato. Kwa sababu wazo la vitambulisho nya wajasiriamali wadogo lilipokuwa limetolewa na Mheshimiwa Rais nilidhani lilikuwa limetazama

Wamachinga wanaozunguka barabarani na mitaani, lakini leo tunavyozungumza, vitambulisho vya wajasiriamali wadogo wadogo vimeenda mpaka masokoni kwenye ambavyo ni vitega uchumi vya Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wafanyabiashara wadogo wadogo walioko kwenye masoko, leo nao wanapaswa kupewa vitambulisho vya Mheshimiwa Rais. Kwa misingi hiyo, ina maana kwamba hata mapato yaliyokuwa yakipatikana kwenye masoko yetu, leo hayapatikani kwa ajili ya kuendesha Halmashauri, masoko hayana utaratibu sahihi wa kufanyiwa usafi. Kwa hiyo, mwisho wa siku zoezi hili linaweza likasababisha uchafu katika maeneo yetu mengi na masoko yetu mengi na Halmashauri zetu nyingi kukosa mapato na pia kushindwa kusafisha maeneo yao muhimu sana katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri suala hili liangaliwe. Pamoja na nia yake njema ya kusaidia wafanyabiashara wadogo wadogo kwa maana ya Wamachinga, wale wanaotembea na vitu kichwani ili watambulike, ili wasibugudhiwe, lakini ni lazima tuone namna gani mpango huu unaendelea kuzibakishia Halmashauri mapato ili dhamira hii ambayo Mheshimiwa Waziri Mkuu ameonyesha kwenye hotuba yake kwamba lengo ni kusaidia Halmashauri zipate mapato badala ya kuathirika kuhusu mapato yake. Kwa sababu kwa hali ilivyo sasa hivi hapa, mpango huu unaziathiri sana Halmashauri nyingi ambazo zilikuwa zinatumia baadhi ya maeneo kama masoko kama sehemu ya vyanzo vyake vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hotuba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kwamba hali ya demokrasia nchini anaona inaimarika. Inawezekana hali inaimarika kwa mtazamo wa tawala, lakini kwa uhalsia na kama wote mnamwogopa Mungu, hali ya demokrasia katika nchi hii imekuwa mbaya sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tulipokuwa tupo kwenye Serikali ya Awamu ya Nne na zilizokuwa nyuma yake hali

ilikuwa angalau ni nzuri hata kama ilikuwa na matatizo kidogo kidogo kuliko hali ilivyo sasa. Kwa kujidanganya kwamba hali ya demokrasia katika nchi hii inaimarika, kujidanganya kwamba chaguzi zilikuwa huru na haki, ni kujidanganya sisi wenyewe kama vile hatuoni. Kimsingi ni kwamba hali ya demokrasia katika nchi hii imekuwa ni mbaya zaidi kuliko wakati wowote mwingine katika nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri, tungejitathmini vizuri bila kuwa na ushabiki wa kisiasa. Katika Taifa hili hatuna ubaguzi wa kidini, hatuna ubaguzi wa kikabila, lakini tumekuwa na ubaguzi mkubwa sana wa kiiitikadi. Leo kuna watu ambao katika nchi hii, kwa kuwa katika itikadi tofauti na Chama Tawala wanaonekana kama vile sio watu wenyewe haki na Taifa la Tanzania. Wanaonekana kwamba hawastahili kukaa Tanzania. Tumejikuta tunatengeneza mbegu ambayo mwisho wa siku itakuwa ni tatizo kubwa katika Taifa hili na inaweza ikaliumiza sana Taifa hili kwa kubaguana kiiitikadi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi wote ni Watanzania tuonane kwamba tuna haki ya kuishi Tanzania na kufaidi rasilimali za Watanzania. Leo tunavyozungumza hapa, Serikali wenyewe mtazamo wake ni kwamba kimaendeleo inaweza ikadhani kwamba kupeleka maendeleo maeneo yaliyochagua CCM ni sahihi zaidi kuliko kupeleka maendeleo maeneo yaliyochagua Upinzani, wakati Upinzani uko kwa misingi ya Katiba ya nchi hii, tumekubaliana wenyewe kwamba lazima Vyama vya Siasa viwepo na wananchi wana haki ya kuchagua anayeona anafaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vizuri tuheshimu haya mambo tuliyokubaliana kwa mujibu wa Katiba yetu ya nchi hii, kuliko kuanza kubaguana kwa misingi tuliyojiwekea wenyewe. Tunatengeneza kizazi ambacho kitakuwa ni cha ubaguzi kisichopendana bila sababu yoyote ya kimsingi. Kazi yote aliyoifanya Mwalimu Nyerere na wenzake katika nchi hii mwisho wa siku itaishia mahali pasipojulikana. Ni vizuri turudishe umoja wetu, itikadi iwe kichocheo cha maendeleo

isiwe sababu ya kubaguana baina yetu sisi wenyewe kwa wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kutoa rai yangu kwa Serikali kwamba hebu rudini nyuma tazameni kwamba hivi tuko katika mstari sahihi? Hivi kweli ni sahihi kusema kwamba demokrasia imeimarika?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, naomba kuwasilisha. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mussa Mbarouk, atafuatiwa na Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub. Mheshimiwa Alhaj Abdallah Bulembo ajiandae.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Labda kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia afya njema na kuweza kukutana kuzungumza mambo mbalimbali ya nchi yetu. Pili niwashukuru wapiga kura wangu wa Jimbo la Tanga Mjini ambaao wameniwezesha nirudie mara kwa mara kuwa Mbunge wa kwanza wa Upinzani kufika katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, vilevile pia niwashukuru wazazi wangu kwa namna walivyonilea mpaka nikakubalika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa, hebu ili taarifa zetu zikae vizuri, wewe ni Mbunge wa kwanza wa Upinzani, au Mbunge wa kwanza wa Upinzani kutokea Tanga? Ili taarifa zikae vizuri kwenye Taarifa zetu Rasmi za Bunge.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mbunge wa kwanza wa Upinzani katika Jiji la Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nianze kuchangia kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nachangia katika bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Nianze kwanza na suala la vijana. Vijana

kuna usemi unaosema kwamba ni Taifa la kesho, lakini mimi niseme vijana ni Taifa la leo. Kwa nini nasema hivyo? Nina mifano ya kutoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika nchi nyingi duniani katika masuala ya maendeleo, katika masuala labda ya michezo, katika masuala ya uzalishaji mali kwa mfano ajira viwandani, wanaojiriwa kwanza ni vijana. Hata hapa tulipofikia leo sisi Tanzania, vijana ndio wanaokuwa ni nguvukazi, wana nguvu ya kufanya mambo ambayo yanaweza kuipeleka nchi mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, muda siyo mrefu tulizungumzia masuala ya vilabu vyetu, ukitazama kwa mfano Klabu ya Simba, vijana wale wa kikosi kipana cha Simba, ndio waliowezesha kuifanya Simba ifanye vizuri kuweza kuipiga JS Saoura, kuifuga AS Vita kuzifunga Al-Ahaly kwa sababu ni vijana wana nguvu. Pia kwa *Taifa Star*. *Taifa Star* wamefanya vizuri kuipiga Uganda bao tatu bila kwa sababu ni vijana wenyewe nguvu ambao wameandaliwa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nami naishauri Serikali yetu vijana tuwaandae vizuri ili tuweze kuwatumia katika nguvu kazi ya Taifa letu. Kwa mfano, leo Tanzania tuna maeneo mengi sana ya mapori ambayo hayajatumika, ajira zimekuwa zikikosekana. Kama Serikali itaweka mipango mizuri ya kuweza kuwatumia vijana, tukaweza kuwawezesha kwa vifaa, mitambo na mashine mbalimbali pamoja na mitambo hii ya *irrigation*, tunaweza kabisa kujizalishia chakula ambacho kitaweza kututosheleza nchi yetu na nchi jirani tutaweza kuwauzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa imekuwa kuna tatizo kidogo ambalo mimi naliona. Kwa mfano, kwenye masuala ya Kambi za JKT vijana zamani walikuwa wakimaliza Darasa la Saba asilimia kubwa wanapelekwa kwenye Kambi za JKT. Sasa hivi kuipata nafasi ya kuingia JKT imekuwa ni shughuli. Lazima pawe na mipango ya chini kwa chini, pawe na undugunaizesheni, pawe na ujamaa ndiyo mtu atawea kuingia katika Kambi za JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hili siyo sawa hata kidogo. Wale wengi ambao wanashindwa kufaulu mtihani wa Darasa la Saba, kwenda *Form One*, wale ambao wanashindwa kufaulu mtihani wa *Form Four* kwenda *Form Five*, *Form Six*, naamini kama tungewawekea mazingira mazuri, tukawapeleka katika Kambi zetu za JKT wakajifunza huko uashi, ufundi umeme, kilimo cha kisasa, *mechanics* na aina mbalimbali ya ufundi hata kuchomelea (*welding*) na mambo mengine, tungekuwa na jeshi kubwa la vijana ambalo lingeweza kuwa la uzalishaji mali. Sasa hivi imekuwa ni kinyume. Kwa hiyo, naishauri Serikali kwamba tuiangalie upya taratibu za kujunga na JKT.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hilo halitoshi, kwenye Sekta ya Walemaru; Tanzania tunao walemaru. Naishukuru Serikali kwamba angalau tunajitahidi sasa katika makusanyo ya kila Halmashauri, 2% ya kat i ya zile 10% inakwenda kwa walemaru; 4% kwa akina mama, 4% kwa vijana. Hivi tukiulizana hapa Waheshimiwa Wabunge, ni kweli hizi fedha zinapelekwa huko kwa walemaru hizo 2%? Ni kweli zinapelekwa kwa vijana hiyo 4%? Kidogo angalau kwa akina mama, lakini kwa vijana bado. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri kwamba hizi asilimia za mapato, lazima Halmashauri tuzisimamie vizuri tuhakikishe kwamba hizi fedha zinakwenda; vijana na akina mama na walemaru wapatiwe hizi fedha. Kwa sababu kama watapatiwa hizi fedha, Watanzania wana upeo wa kuelewa mambo haraka. Kama watawezesha, wataweza kuzitumia vizuri, zitawezesha kuwasaidia katika maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, wapo walemaru wengine ambao ni mafundi viatu, wengine ni mafundi vyerahani tena wanawaajiri na wenzao, lakini mitaji wanakuwa hawana. Sasa niseme tu kwamba tuwawezeshe...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Mbarouk, kuna Taarifa.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Ahsante.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge wa Tanga kwamba Bunge liliopita ziligawiwa hapa Kamusi za Kiswahili na lugha sahihi ya kutumia hapa ni kwamba ni watu wenye ulemavu, sio watu lemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Ahsante. Naibu Waziri

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mbarouk, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimeipokea. Watu wenye ulemavu, sio walemauvu, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, nami niombe tuwasaidie hawa wenzetu kwa sababu, sisi tulikuwa wazima hatukuwa na mipango na Mwenyezi Mungu kwamba tuwe wazima na wale wenzetu waliokuwa wenye ulemavu sio kwamba kuna kitu wamekosea. Kwa hiyo, tuwaangalie kwa jicho la huruma na tuwasaidie pale inapobidi kihalisa, siyo iwe kimaneno maneno tu, kwamba tukija humu tunaambiana maneno, lakini ukirudi huko unamkuta mlemauvu anakwambia Mheshimiwa Mbunge kama ungenipatia mashine ya cherehani, ungenipatia na ngozi na uzi ningewaaajiri vijana wenzangu hapa wenye ulemavu wanne, watano. Sasa tuwasaidie kama inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nije kwenye suala la wazee. Sote sisi hapa ni wazee watarajiwa lakini cha kushangaza, ukienda kwa wazee unaambiwa watatibiwa bure. Wameandaliiwa vitambulisho, wamelipa shilingi elfu elfu lakini

ama akienda hospitalini au kwenye Kituo cha Afya, ataishia kuandikiwa tu dawa aambiwe hizi kanunue. Mzee huyu kipato chake kimeshakuwa kidogo kwa sababu hizo pensheni zenyewe pia wanazopewa hapewi moja kwa moja hiyo shilingi 66,000/= analimbikiziwa baada ya miezi mitatu ndiyo apewe. Kwa hiyo, hana uwezo hata wa kununua ile dawa anayoandikiwa. Niseme, hawa wazee kama tumeamua watibiwe bure, akina mama wajawazito na watoto basi iwe wakienda wanapata dawa zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya PAC tumekwenda kutembelea bohari la madawa *MSD* Dar es Salaam, tumekuta kuna madawa mengi mpaka yanafikia ku-*expire* kwa sababu hayafikishwi kule kunakohitajika. Tulipowahoji wataalam wetu, wanasema Madaktari wa Wilaya, na wa mikoa dawa nyingine hawaziombi. Kwa mfano, dawa za nyoka, dawa za mambo mengine, sukari na nini haziombwi, kwa hiyo, zinakaa mpaka zina- *expire*. Tungezipeleka kule ili hawa wazee na akina mama na watoto wanaotakiwa kutibiwa bure, zi-*expire* huko huko kwenye Vituo vya Afya sio zi *expire* pale *MSD*. Kwa hiyo, nasema wazee wetu watibiwe bure.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta amekwenda labda mzee, mwanamke ana cheni ya dhahabu. Daktari anamwambia ah, wewe unataka kutibiwa bure, mbona una cheni ya dhahabu? Sasa kwani cheni ya dhahabu ni dhambi? Si Sera ya Taifa kwamba wazee watibiwe bure? Ama amekwenda na gari, au amekwenda na *taxis*, sera inasema atibiwe bure.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Taarifa.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**MHE. MUSSA B. MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, lingine niende kwenye hali ya kiuchumi. Kwenye kitabu cha Waziri Mkuu ukurasa wa 11.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Mbarouk, kuna taarifa. Sasa kengele ya pili imeshagonga. Nitakuongeza dakika moja ili umalizie.

Mheshimiwa Ummy, Taarifa.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpa taarifa Mheshimiwa Mussa Mbarouk kwamba, sera kuhusu matibabu bure kwa wazee ni kwa wazee wasio nauwezo na sio kila mzee anatakiwa kupata matibabu bure, ni mzee asiyé na uwezo. Niliona nitoe taarifa hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Mbarouk unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. MUSSA MBAROUK:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenda suala la kiuchumi, pato la Taifa limekuwa kwa 6.7% mwaka 2018 na 6.2% kwa mwaka 2017, lakini niseme linakuwa katika makaratasilakini kihalsia ukiwatazama watanzania huko nje wako hoi bin taabani...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Nafikiri juzi tulimsikia Mheshimiwa Spika hapa akitoa maelezo kuhusu hicho unachokisema hapo, sikusudii kuyarudia. Pia ni vizuri upande wa Serikali mtakapokuwa mnajibu hii hoji ya kuharibika madawa lazima taarifa zetu zikae vizuri, kwa sababu nadhani kutoka wilayani na mikoani wanaagiza dawa wanazozihitaji. Sasa kama maeneo mengine kuna baridi hakuna nyoka, sina hakika wanaweza kuagiza hizo dawa, kwa hiyo zinaharibikia kule, lakini kama Serikali lazima dawa ziwepo ila mliweke vizuri saa ya kujibu hoja ili taarifa zetu Bungeni zikae vizuri.

Mheshimiwa Jaku Hashim Ayoub, atafutiwa na Alhaj Abdallah Bulembo na Mheshimiwa Vedastus Mathayo ajilanda.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana kwa kuniruhusu kuchangia bajeti hii muhimu ya Waziri Mkuu. Kabla suaanza kuchangia kwanza namshukuru Mwenyezi Mungu aliyenipa nguvu za kuweza kusimama hapa na kuchangia, uwezo huu si wangu, wala maarifa yangu, wala nguvu zangu, ni neema zake yeye Mwenyezi Mungu. Ndio pale aliposema katika kitabu chake kitukufu "*Wakhulka I-insaanu dhwaif*" maana yake tumemuumba mwanadamu kuwa ni dhaifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kwa dhati kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na timu yake kwa umakini wa hali ya juu kwa kutuletea ripoti hii. Namjua Mheshimiwa Waziri Mkuu umakini wake, lakini mchango wangu utalenga katika sehemu tatu: Kwanza sehemu ya Muungano; pili, sehemu ya Bunge; na tatu, *TRA*. Nitajikita zaidi kwenye Muungano ukurasa wa 81 ambapo tunakaribia kutimia miaka 55 ya Muungano wetu huu ambaa ni mfano kwa dunia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Muungano wetu huu ni matokeo ya mahusiano kihistoria kwa pande zote mbili, kwa hiyo hatuna budi kuheshimu na kulinda ili kuendeleza kudumu kwa faida ya watu wetu. Katika kuimarisha Muungano wetu Serikali zote mbili zinaendelea kuzitafutia ufumbuzi changamoto mbalimbali zinazoukabili. Tarehe 21 Januari, 2019 kilifanyika kikao cha Baraza la Mawaziri kilichohusu utozwaji wa kodi wa thamani (*VAT*) cha 0%. Hili jambo niendeleee kulishukuru tena kwa mara ya pili ndani ya chombo hiki na huu ndio Muungano, sio upande mmoja. Limepata suluhu na kiana yake niendeleee kumshukuru sana Spika wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kazi kubwa aliyofanya pamoja na Mawaziri

Mheshimiwa Naibu Spika, sitawafanya haki Mheshimiwa January Makamba na Naibu Waziri wake katika

sekta hii ya Muungano, Mheshimiwa Mussa Sima kama sitawapongeza kwa jitihada walizozifanya. Hata hivyo, kuna baadhi ya hizi kero za muda mrefu za 4.5%, kwanza naishukuru Benki Kuu kwanza hapa Waziri wa Fedha naomba *a-take note* hapa kidogo kwa faida ya wananchi wa Zanzibar; 4.53 toka dunia ilipoanza mpaka muda na mwanzo ilipokubaliana *IMF*, formula hii ni ya muda, sasa Zanzibar imekua, watu wameongezeka, mahitaji ya barabara yamekuwa makubwa, hii muingalie tena upya na hii ilikuwa ya muda 4.5. Zanzibar ishakuwa kubwa kupita kiasi kwa muda huu, ifike mahali walitatue tatizo hili, ni la muda mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ajira katika sekta ya Muungano, upande wa Jeshi, upande wa Mambo ya Ndani, *Migration*, Polisi na Mambo ya Nje wanawashirikisha Zanzibar lakini waangalie *formula* nyingine, sasa hivi ajira imekua ngumu, pamoja na kuwa Tanzania bara ni kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la kusikitisha, *formula* iliyokuwepo zamani Marais wengi wamekuwa wakitumia, viongozi waliokuwa wakifika Tanzania Bara walkuwa wakifika Zanzabar, sasa hivi hatuwaoni. Hili niliombe, viongozi sitaki kuwataja, ni wengi wamefika Tanzania Bara, viongozi mashuhuri, lakini wengine hawafiki Zanzibar. Hili halileti picha nzuri, hili naomba sana ifike mahali viongozi wanaofika huku wawapeleke Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni kuhusu bidhaa za Zanzibar kuingia katika soko hili la Tanzania bara, hiki ni kilio cha muda mrefu sana na wengine wameanza kufunga biashara zao. Itafutwe *formula*, maziwa hayafiki huku, sukari ipo Tanzania Bara, huku hailetwi, tunalinda viwanda vyta Tanzania, sio vyta Tanzania Bara. Tanzania ikiwepo Zanzibar, tuwe wakweli, tutafute *formula* itakayoweka sana. Zanzibar inategemea karafuu, ndio uchumi wake, ukiacha karafuu, pili ni utalii.

Mheshimwa Dau alizungumza pale hajui watalii wanaofika Zanzibar ni wangapi karibu laki saba kwa mwezi au zaidi ya hapo kama sikosei.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ifike mahali tuangalie *formula* hii inavyokwenda. Zanzibar kipato chake kikubwa sasa hivi ni utalii, tufike mahali tuangalie, watusaidie. Bidhaa inayitoka Zanzibar ikafika huku, suala hili tumepega kelele muda mrefu jamani, waitafutie *formula*, *TRA* ni moja Tanzania. Leo hesabu inaanza moja ndio ije mbili. Mtoto akizaliwa leo hatembe iku hiyo hiyo hutambaa, akakamata kibambaza akaanguka, hili halileti picha nzuri jamani. Niombe sana suala hili liangaliwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi sasa Tanzania mambo mengi Tanzania Bara imeiga Zanzibar bila kuficha, Mheshimiwa Waziri wa Fedha hapa nataka aliangalie na Benki Kuu awafahamishe, *formula* inayokuja ya *Bureau De Change* nasikia itakuwa ngumu na Zanzibar ni ndogo na inategemea sana utalii itawasumbua. Vigezo vyta *formula* hii Tanzania Bara wameiga toka Zanzibar, waangalie masharti yatakayokuwepo yawe na uwiano.

Narudia tena Zanzibar itategemea utalii, watalii watapata shida, kwa hiyo *formula* ya *Bureau De Change* zinazokuja waziangalie ili angalau kuwe na uwiano, nafikiri hii *formula* itawasokota sana wananchi. Kwa hiyo, jambo hili waliangalie.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kwa kumalizia, namwomba Mheshimiwa Waziri Mkuu na Ofisi yake tunamhitaji Rais wa Jamhuri ya Muungano kwa upande wa Tanzania Bara angalau na sisi atutembelee, roho ina choyo, tunaomba sana. Kachanguliwa na Tanzania ikiwepo Zanzibar tunamwona kwa wenzetu, hili tunaliomba sana, tupelekeeni salam kwa wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Jaku, lakini umezungumza lugha moja hapo kuhusu mtoto kushindwa kukimbia naamini hukukusudia kuita Zanzibar mtoto. Kwa kuwa hukukusudia hayo maneno kwenye Taarifa Rasmi za Bunge yasi...

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niweke *hansard* sawa unajua Kiswahili cha kwetu pwani mtoto akazaliwa haendi mbio siku hiyo hiyo hutambaa akakwetwa, maana yake haya mambo yawe na formula maalum kwa upande wa Zanzibar.

**NAIBU SPIKA:** Hiyo hiyo kauli ndio sitaki iingie kwenye taarifa rasmi za Bunge kwa kuwa Zanzibar sio mtoto wala hajaanza jana Muungano ni wa muda mrefu.

**MHE. JAKU HASHIM AYOUB:** Mheshimiwa Naibu Spika, kama ni hivyo au kama imefahamika hivyo nafuta kauli hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Alhaj Abdallah Bulembo atafuatiwa na Vedastus Mathayo, Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa ajiandae.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye hutuba ya Waziri Mkuu kwanza ni kupongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyotusomea kitabu chake chenyе mafungu kama tisa hivi. La pili, nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, kwa ziara anazifanya kusimamia llani ya Chama chetu cha Mapinduzi, Makamu wa Rais mama Samia anavyozunguka kuweka mambo sawa huko na Mheshimiwa Majaliwa na Mawaziri na wengine wote nawapongeza sana kwa mambo wanayoyafanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, dakika sijui ni tano au ni kumi?

**NAIBU SPIKA:** dakika ni kumi.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. La kwanza nitaanza kwenye eneo la madini na naomba ku-*declare interest* kuwa mimi ni mchimbaji mdogo. Kwanza tumpongeze Mheshimiwa Rais na Makamu wake, Waziri wa Madini na Waziri aliyehamia kwenye uwekezaji kwa mkutano tuliofanya pale Dar es

Salaam siku mbili, tunaipongeza sana Serikali kwa kuweza kuwasikiliza wadau wa madini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la madini tuliahidi mambo mengi. Serikali yetu cha Chama cha Mapinduzi ni sikivu ilioa kodi kwenye 27 tukaenda *royaltiesita* kuongeza moja. Si jambo dogo ni jambo kubwa sana. Hapa sasa nataka kuiomba Wizara ya Madini na wachimbaji wadogo wadogo, tulikubali mbele ya Rais kwamba tutalipa kodi, tulikubali mbele ya Rais kwamba hatutatorosha madini, tulikubali mbele ya Rais kwamba lazima tukusanye kodi ili nchi iweze kuendeshwa. Niiombe Wizara ya Madini na Tume waache kuchekacheka na watu wanaoharibu dhamira nzuri ya wachimbaji wadogo. Tumekubaliana mtu akikamatwa na madini mahakamani tena uhujumu uchumi basi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo ndani ya Wizara hao wachimbaji wadogo wanasmamiwa na wafanyakazi wa Wizara ya Madini, hawa wafanyakazi wa madini ambaio sio waadilifu waanze kuwachuja wasituletee matatizo. Sisi tumeshakubali kuchimba, tumeshakubali kulipa kodi, lakini unajikuta watu wanaunga, wanafanya jambo baya sana hili. Nimpongeze Waziri wa Madini juzi nilimuona Chunya, wale watu wameondoshwa, waondoshwe wengi, wapo watu wengi sana wanaoharibu kwenye sekta hii. Sekta hii ni nzuri, mwaka kesho wakati tunasomewa hotuba, sekta ya madini itakuwa imepanda mara dufu. Kwa hiyo msingi sisi tunachimba tunalipa kodi, lakini Wizara na Tume wasimamie watu wao. Kwa sababu kule ndani ndio watopandisha leseni anampa huyu na huyu, anageuza huku na huku, lakini kama hatuwezi kuipa umuhimu kama Rais alivyoipa umuhimu kodi hii ukusanyaji wake utakuwa shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, pale pale kwenye madini walikamatwa watu kwenye makinikia wakazuia michanga yao, sheria imekuja, kuna wenzetu ambaio hawana matatizo ya kulipa kodi na kusafirisha michanga yao, kwa nini hawawapi ruhusa Serikali ikapata fedha yake? Wanakosa gani hawa? Mtu yupo tayari kulipa kodi, mtu hana tatizo ni mchimbaji, kuna watu wamewekeza katika nchi hii, kwa nini

hawawaruhusu wakafuata taratibu kodi ile ikakusanya? Nawaomba sana watu wa madini, hili eneo ni nyeti, lakini kuna watu wanafilisika, watu hawahudumiwi. Kwa hiyo, naomba kosa la mtoto mmoja lisimzuie mtoto mwingine kupata haki yake ya maisha. Kwa hiyo nawaomba sana watu madini, waende waangalie eneo hilo, wale watu ambao hawana shida wawaruhusu wasafirishe, walipe kodi, kwa nini wanarundika, wameweke mitaji, hali si nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijamaliza niende katika suala la ardhi hapo hapo kwenye madini. Kwenye eneo la ardhi kumepimwa kuna madini lakini pale juu kuna mtu analima mahindi, siku ukienda kuchimba anakwambia sitaki, khaaa wewe unalima mahindi mimi nachimba dhahabu tofauti iko wapi? Niwaombe watu wa ardhi waende kule wawaelimishe hawa watu ambao wapo kwenye maeneo ya madini, nikishapewa ardhini kwa maana nimepewa leseni, mimi nitakuwa chini wewe utakuwa juu, msingi tujadiliane ili watu wote wawe wa moja. Hata hivyo, ukienda eneo la ardhini unakuta nao wameweke masharti yao, imeenda imerudi, wanachelewesha kuchangamsha uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Maliasili na Utalii, mtu kapewa leseni ya madini pale vijimiti, kipori anasema ni hifadhi, hifadhi ipi? Wakati mali kubwa ya kuleta ushuru ipo wanaikatalia na hawaifanyii chochote? Hapo tusaidie Watanzania, wachimbaji wadogo wakusanye kodi hii msiweke vikwazo wakati sehemu hii haitumiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, namba mbili naenda Wizara ya Mifugo na Uvuvi, mwaka jana nilipambana na wao lakini mwaka huu nawapongeza sana, hongera sana kwa kazi wanayoifanya hasa hasa kwenye eneo la mifugo. Kwenye eneo la mifugo kulikuwa na shida sana sana tu, wafugaji wanatangatanga, wanaenda huku na huku wanafanya hivi, lakini naipongeza Wizara, juzi nimeona wamesaini mkataba wa kujenga viwanda vya nyama vingi na juzi nimeona wametangaza kule kwenye *ranch*, yale maeneo ya watu kupewa *ranch*, suala hili ni la muhimu na la

kupongeza, wapo Watanzania walikuwa wanakaa na vitalu hivi bila kulipa chachote Serikali haipati kodi. Sasa leo kwa sababu wamekuja na nia njema waisimamie, vitalu vipatikane, watu wachangie pato la Taifa, maziwa yapatikane, viwanda wanavyovijenga zaidi ya vitano, vipate malighafi. Katika hilo nampongeza Mheshimiwa Mpina, leo nampongeza na Mheshimiwa Ulega, nawapongeza sana wameenda vizuri, waweke utaratibu ili angalau makusanyo ya nchi yapatikane kila eneo yanapotakiwa kupatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo lile la *ranch* kuna mwenzangu jana alisema Mheshimiwa Kamala sijui kama yupo, kwamba kuna wananchi walikuwepo, tunapotaka kuweka utaratibu watu wamekaa na ranchi miaka zaidi ya 15 Serikali haipati hata senti tano, acheni vitalu vigawiwe, Serikali ikusanye kodi, watu wafuge kwa uzuri ili maendeleo ya nchi yapatikane, sio cha mjomba, cha shangazi, mimi nasema wakaze kamba, tunataka kufuga, tunataka kufua, tunataka Tanzania uchumi uchangamke.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoka mifugo niende hapa kwenye Mambo ya Ndani, neno hili nalisema kwa mara ya nne, si zuri sana, Ofisi ya Waziri Mkuu na Ofisi ya Mambo ya Ndani wafanyakazi wa nje walipo humu nchini, vibali hivi kuna watu wana haki ya kupewa, kuna watu hawana haki ya kupewa. Wapo watu humu nikisema tunanuniana, lakini mimi ni mzee, sina shida, ukininunia mimi naenda kulala, kwa hiyo haisaidii kitu chochote. Yaani mtu ana miaka 20, leo hii wanafanya mpango kumpa uraia, Wizara ya Kazi na Mambo ya Ndani nasema suala hili tutaliweka hadharani hapa, mimi nakusanya vielelezo tu, mtu muda wake umekwisha, anatakiwa kutoka nchini, amekaa zaidi ya miaka 20, anafanya siasa, si Mtanzania.

*Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Waziri Mkuu kupitia kwa Mheshimiwa Jenista na Wizara ya Mambo ya Ndani nasema neno hili kwa mara ya mwisho, waende kwa huyu mtu, wampe vibali vyta uraia, tutakutana hapa, sisi wote ni Watanzania. Kuna Mzee Raza jana kasema kuna kiwanda, kina watu zaidi ya 300, wanawaombea Engineers wawili*

wanakataa, watu 300 wote, hawatapata kazi? Huyu mtu anaitwa *Vedigree* anawalipa shilingi ngapi? Niko tayari kuweka vielelezo mezani nasema kwa mara ya tano leo ndani ya *Bunge* hili. Sasa wamwandalie uraia halafu tuone uraia huo ataupataje katika nchi hii, sababu si lazima watangaze. [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa kengele ya pili.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulembo naomba ukae. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niliweke vizuri jambo hili kwa sababu nisipoliweka vizuri sidhani kama maneno yalijotumiwa na Mheshimiwa Mbunge kama yapo sawasawa sana kwamba tunapewa shilingi ngapi kwa ajili ya suala hili. Hapana, si sawa, sidhani kama ana hakika kama kuna fedha yoyote imeingia kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya jambo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaomba tu nimthibitishie Mheshimiwa Mbunge Ofisi yangu jambo hili imeshalishughulikia na yeye anajua. Kwa hiyo masuala mengine ya mtu kuendelea kuomba kitu chochote, atafuata utaratibu na majibu ya kiutaratibu yatatolewa wakati utakapofika. Tukifika mahali Ofisi imeshachukua hatua naimeendelea kulishughulikia jambo lenyewe, halafu Mheshimiwa Mbunge anajenga hisia kwamba labda Ofisi ya Waziri Mkuu ina jambo fulani, nadhani si sawasawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge na vinginevyo nitumie ile kanuni ya

kumwomba aondoe hili jambo katika taarifa yake aliyoisema leo, ama tutumie kanuni nyingine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimimu sana Mheshimiwa Bulembo na naomba nimpe hiyo taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulembo, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa watu wenye busara suala la hela nalifuta lakini mazingira ya rushwa siwezi kufuta.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, huwa tunakumbushana na si jambo baya tukiendelea kukumbushana. Sheria zinatungwa na Bunge na watu haki zao ziko Kikatiba na pia kisheria kwa kadri sisi kama Bunge tulivyoelekeza kwenye sheria zinazohusika. Haki ya mtu haiwezi kuchukuliwa kwa kutumia Bunge. Vyombo mahsusii kwa ajili ya kazi hiyo vipo.

Kwa hiyo, kwa maana ya maneno aliyoayazungumza Mheshimiwa Jenista ili tusifikie huko kwenye kuvutana kikanuni, kuweka kwamba kuna mazingira ya rushwa kunanipelekea mimi kwenye maamuzi tofauti. Kwa sababu hiyo na kwa sababu sikusudii kumpa Mheshimiwa Jenista fursa tena, maneno hayo yaondoke kwa sababu kama alivyosema kwamba hii ni mara ya tano ni kweli, hili jambo lilishawahidi kuagizwa kwamba likafanyiwe kazi. Mimi nataraji kwamba Serikali ilichukua hatua ya kufanyi kazi.

Kwa mujibu wa maelezo yako Mheshimiwa Bulembo umesema mtu huyu ametoka sasa kwenye kuomba kibali anaomba uraia. Utaratibu wa mtu kupata uraia uko kisheria, kwa hiyo, kama anakidhi sheria hata kama atapewa huo uraia haina uhusiano na kuwa na mazingira ya rushwa. Kama atanyimwa uraia ni kwa kutokukidhi vigezo ambavyo sheria zetu imeweka. Kwa hiyo, tusiweke hayo mazingira ya kuona kwamba kuna namna ambayo jambo likichukua pengine muda mrefu linaleta hisia fulani.

Kwa upande wa Serikali iko hoja ya watu wengine wenye uhitaji wa jambo hilo pengine linatazamwa tofauti. Hilo sasa ni jambo la kiutendaji kwenu Ofisini ili watu wanaostahili kupewa wapewe na wasiostahili kwa mujibu wa vigezo viliviyowekwa na Katiba na sheria zetu basi utaratibu huo uliopo ufuatwe.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Vedastus Mathayo atafuatiwa na Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa, Mheshimiwa Aida Khenani ajiandae.

**MHE. VEDASTUS M. MANYINYI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia katika hii hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kazi nzuri ambayo ameendelea kuifanya yeye na wasaidizi wake kwa maana ya Makamu wa Rais, Waziri Mkuu pamoja na viongozi wote wa Serikali. Mambo haya kusema kweli yako wazi kwa maana ya maendeleo ambayo yameendelea kufanyika hasa katika kuboresha huduma za jamii.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda nizungumzie kwanza ushahidi huo katika Jimbo langu la Musoma, kwamba ni kwa kiasi gani katika kipindi hiki kifupi huduma za jamii zimeendelea kuboreshwa sana. Leo unapozungumza upande wa elimu, nakumbuka Mheshimiwa Rais aliposema kwamba sasa elimu itatolewa bure, kiwango cha uandikishwaji wa watoto kimekuwa kikubwa sana na mpaka kimepelekea darasa la kwanza kwenye shule mbalimbali wanaenda mpaka watoto 800 kwa darasa moja badala ya yale madarasa matatu. Hiyo yote inaonesha ni kwa kiasi gani wanafunzi wengi zaidi wamejiunga katika elimu ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata unapozungumza habari ya afya, mfano mwaka jana tu achana na miaka mingine tumepata shilingi millioni 400 kwa ajili ya huduma ya afya lakini tumepata zaidi ya shilingi bilioni 3 kwa ajili ya

Hospitali yetu ya Rufaa. Kwa hiyo, hayo yote ni matokeo ya uongozi mzuri na kuwajali wananchi ndiyo maana yameendelea kujitokeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika, hata upande wa habari ya maji, kwa Musoma Mjini tulikuwa na tatizo kubwa la maji lakini leo shida kubwa tuliyonayo ni tatizo la mabomba kupasuka shauri ya *pressure* ya maji. Kwa hiyo, hii yote inaonesha ni kwa kiasi gani Serikali ya Chama cha Mapinduzi imeendelea kushughulikia matatizo ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi nakumbuka katika hiki cha miaka miwili pale kwangu nimepata shilingi bilioni 12 kwa ajili ya barabara, lakini hata kwa mwaka huu tu nimepata shilingi bilioni 4. Hata ile Kamati ya Bunge iliyokuja Mjini Musoma nadhani iliweza kuona maana ilizitembelea zile barabara iliona ni kwa kiasi gani ule Mji wetu wa Musoma umekuwa mzuri kwa ujenzi wa barabara za kiwango cha lami. Kwa hiyo, ndiyo maana tunasema tuna kila aina ya sababu ya kuishukuru na kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa na nzuri ambayo imefanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Mbunge wa Jimbo la Musoma nimeona nizungumzie tu yale ya pale mjini zaidi ya yale makubwa ambayo yanaonekana katika nchi nzima. Mfano leo ukipita wakati wa usiku kwenye maeneo mengi utadhani kama ni mjini kwa sababu karibu kata na miji inazo taa kwa maana kwamba umeme umesambaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo kwetu sisi kama nchi matumizi yetu ya umeme ni wastani wa MW 1,100 lakini umeme ambao unazalishwa sio chini ya MW 1,600. Kwa hiyo, hii tu inaonyesha ni kwa kiasi gani tumejitahidi lakini Serikali ina jukumu la kuhakikisha ule umeme unasambaa katika maeneo mengine ambayo bado hayajapata umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi nilisafiri nilipofika pale *Airports* saa 12.00 wakati na-*board*, ukiangalia ule uwanja wa ndege umepambwa kwa ndege za *Air Tanzania*. Katika siku

za nyuma ulikuwa unakuta hata kile kibao kile kimoja tu cha *Air Tanzania* kilikuwa hakiwezi kuonekana. Haya yote ni mambo makubwa tuna kila aina ya sababu ya kuyasemea wala hatuhitaji kumung'unya maneno. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba wajitahidi sana kama ambavyo *speed* kubwa imeelekea kwenye hii reli ya mwendo kasi, mwaka jana nilisema na mwaka huu nasema, pale reli itakapofika Morogoro tu basi na vichwa pamoja na mabehewa vianze kutembea ambayo yatakuwa yanaleta abiria pale na abiria kuanzia saa 1.00 wanachukuliwa kutokea pale. Matokeo yake kila Mtanzania atakuwa siku hiyo ametoka Dar es Salaam na atalala nyumbani kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya sana leo watu wa Kanda ya Ziwa wakiondoka Dar es Salaam lazima walale njiani kwa sababu ya urefu wa barabara. Kwa hiyo, tunadhani kwamba kwa kufanya hivyo, ndivyo Serikali inavyoendelea kushughulikia matatizo ya wananchi wake ili waendelee kuishi kwa amani na raha mustarehe.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo mafanikio mengi maana nilidhani nizungumzie machache lakini niendelee kuzungumzia changamoto ambazo bado zinawasumbua Watanzania lakini na watu wa Jimboni kwangu, wa Jimbo la Musoma. Kwangu mimi pale Musoma Mjini sasa yamebaki matatizo mawili makubwa. Tatizo la kwanza Mheshimiwa Waziri Mkuu analifahamu vizuri, niendele tu kumkumbusha na hili sasa badala ya kumkumbusha wale wananchi nitawaleta katika Bunge kwake waje wamuone yeeye mwenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, wako wafanyakazi waliokuwa wa Kiwanda cha *Mutex* ambao malipo yao nimekuwa nikiyasemea kila leo lakini hayo malipo yamekuja kufanyika ambapo kile kiwango walichokitaa ambacho hawakupewa miaka ishirini iliyopita leo wamekuja kupewa tena nusu ya hicho. Kwa hiyo, hilo kwa kweli kwa wale wananchi ni kero kubwa, ni kero ambayo inawasumbua na kwa sababu Serikali imeahidi kulishughulikia kwa muda mrefu

na mpaka leo haijalishughulikia nitawaleta wenyewe waje kuzungumza na Mheshimiwa Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la pili ni suala la kiwanja cha ndege. Tuliomba kiwanja cha ndege na Mheshimiwa Rais aliridhia na tathmini ya fidia ilishafanyika lakini mpaka leo wananchi hawajalipwa na kuna sintofahamu kama kiwanja kitajengwa au hakitajengwa.

Naiomba Serikali iseme kama hakijengwi tufute zile alama za 'X' ili wananchi waendelee na maisha yao kama kinajengwa basi fidia ilipwe ili ule uwanja uweze kujengwa. Kwa hiyo, hilo nalo nategemea katika kikao hiki au Ofisi ya Mheshimiwa Waziri Mkuu itakapokuwa inajibu italicijibu suala hilo ili wananchi waweze kupata taarifa za uhakika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ni tatizo la ajira. Pamoja na juhudzi zote ambazo tumeendelea kuzifanya za kuongeza viwanda lakini tunatambua kwamba ajira pekee au sehemu pekee itakayopunguza tatizo la ajira ni Wizara ya Kilimo. Kwa hiyo, mimi bado sijaona kama Serikali imeweuka vipi nguvu kwenye Wizara ya Kilimo katika kupunguza tatizo la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia pekee ni kuhakikisha kwamba tunaweka nguvu kubwa kwenye kilimo cha umwagiliaji. Leo ukienda katika Kanda ya Ziwa na hata katika hizi Kanda zingine, Manyara au Arusha maeneo mengi sasa leo ni kiangazi na vyakula vimekuwa. Hii inaonesha kabisa kwamba kama tungekuwa na kilimo cha umwagiliaji nguvu zile walizozitumia wananchi leo lisingekuwa tatizo. Wananchi wamelima, mvua hazikupatikana matokeo yake yale mazao yao yanakuwa. Hii inaonesha moja kwa moja kwamba yawezekana mwaka huu kutakuwa na njaa kubwa, si kwamba wananchi hawakulima ni kwa sababu mazao yao yamekuwa kwa sababu ya kiangazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana naomba kuunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Victor Kilasile Mwambalaswa atafuatiwa na Mheshimiwa Aida Khenan na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu ajandae.

**MHE. VICTOR K. MWAMBALASWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja hii iliyo mbele yetu. Napenda kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake hii nzuri sana, ya kitaalamu. Pia napenda niwapongeze Mawaziri wa Nchi, Mheshimiwa Jenista Mhagama na Mheshimiwa Angella Kairuki, Naibu Mawaziri Mheshimiwa Antony Mavunde na Mheshimiwa Stella Ikupa, Makatibu Wakuu Bibi Maimuna Tarishi, Bwana Andrew Massawe na Bibi Dorothy Mwaluko, hotuba yenu hii ni ya kitaalamu sana, hongereni sana. (Makofii)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ruhusa yako, naomba kunukuu sehemu chache sana, ukurasa wa sita ambapo hotuba inasema: "Mheshimiwa Spika, katika mpango wa maendeleo na bajeti ya 2019/2020, Serikali itaendelea kutekeleza Mradi wa Umeme wa Maji yam to Rufiji, ujenzi wa miundombinu ya reli ya kisasa, barabara pamoja na kukuza sekta ya anga. Utekelezaji wa miradi hiyo ya miundombinu wezeshi ya kiuchumi una lengo la kufungamanisha ukuaji wa sekta hizo na sekta nyingine hasa hasa za biashara, kilimo na utalii".

Mheshimiwa Naibu Spika, kukuza sekta za miundombinu ni kukuza uchumi. Nchi ya Tanzania imebahatika kuwa na bandari nyingi na tumezungukwa na nchi nyingi ambazo hazina bandari. Tumezungukwa na nchi za Malawi, Zambia, Congo hasa upande wa Mashariki, Burundi, Rwanda na Uganda na Jamhuri ya Kati ambazo hazina bandari. Kwa hiyo, bahati hii ambayo ametupa Mwenyezi Mungu kuwa na bandari tuitumie vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefurahishwa sana kwamba Serikali sasa inaboresha bandari zote, imeanza na bandari ya Dar es Salaam, inakwenda bandari ya Tanga na

bandari ya Mtwara na kujenga bandari mpya hapo Bagamoyo. Tunapozitumia bandari hizi, tujue kwamba kuna wenzetu nao ambao wana bandari, Msumbiji wana bandari ya Beira, Afrika Kusini wana bandari ya Durban kubwa sana, Angola kuna bandari ya Luanda, zote hizi zinaangalia nchi hizi ambazo ziko *landlocked*. Kwa hiyo, naomba tunapoziboresha bandari zetu tujue kwamba kuna ushindani wa kibiashara, wataalamu wetu wahakikishe wanaweka vivutio vizuri vya kuweza kuzivutia nchi hizi zije kuitisha mizigo yao kwenye bandari zetu kuliko bandari za wenzetu, tulitilie maanani sana suala hilo. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukichukua reli ya katii, hii mpya ambayo inajengwa ya *Standard Gauge*, tulikuwa tunakazania sana kutoka Dar es Salaam, Tabora, Isaka kwenda mpaka Kigali ambako na nchi ya Rwanda nayo inajenga kipande kile kule na hili inayokwenda mpaka Kigali inalenga mizigo ya Rwanda, Uganda na Jamhuri ya Kati. Nchi ya Burundi ina madini ya *platinum* zaidi ya tani milioni 6,7,8, sasa reli yetu tukitoa Uvinza, Msongati tuongee na nchi ya Burundi na yenye ijenge kutoka Bujumbura kuja Msongati, tuongee na nchi ya Congo ijenge reli kama hii kutoka bandari ya Uvira ije mpaka Bujumbura ili tuweze tuweze kuidaka ile mizigo ya Congo kwani ina madini mengi sana. Tukiacha sisi wenzetu wa Angola watajenga reli kutoka Rwanda kuja Lubumbashi au Lusaka.

Kwa hiyo, naomba sana tulenge mizigo ya Congo, Burundi na Jamhuri ya Kati kwa sababu reli yetu hii ya *Standard Gauge* itakapokuwa tayari ina uwezo wa kubeba tani karibu milioni 20 za mizigo kwa mwaka, naomba tulenge kuelekea huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na reli hii ya katii ya *Standard Gauge*, nimefurahishwa sana bado Serikali inaendelea kuikarabati hii reli ambayo ipo sasa hivi ya *Metre Gauge*. Kwa hiyo, hapa katii tutakuwa na reli mbili, Reli ya *Standard Gauge* na *Metre Gauge*. Mwaka jana nilisema kwamba tunaponunua *rolling stock* tuhakikishe tunanunua *rolling stock* ambayo unaweza ukatumia kwa reli zote mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tuna reli yetu ya TAZARA, yenyewe haihitaji kuboreshwa katika miundombinu mingi, inahitaji umeme tu. Reli ya TAZARA yenyewe ni Cap Gauge inaoana na reli za Afrika Kusini na Zambia. Naomba na hii reli tuiboreshe kwa kuiwekea umeme ili reli zetu zote tatu, *Standard Gauge, Metre Gauge* na hii *Cap Gauge* zifanye kazi za kuhudumia nchi ambazo ziko *Landlocked*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo naipongeza sana Serikali kwamba imenunua meli mbili au tatu kwenye Ziwa Nyasa ambazo zinafanya biashara nzuri sana ya kusafirisha binadamu na mizigo katika nchi ya Tanzania, Malawi na Msumbiji. Naomba sasa pale Inyara tuweke bandari kavu na vilevile Serikali ifikirie kujenga sasa reli kutoka hapo Inyara kuelekea bandari ya Itungi ili tuweze kuihudumia nchi ya Malawi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchango wangu ulikuwa ni huo tu katika hotuba hii, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Aida Khenan, atafuatiwa na Mheshimiwa Balozi Adadi Rajabu na Mheshimiwa Amina Mollel ajiandae.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Nami namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na kuweza kusimama tena ndani ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitachangia hotuba ya Waziri Mkuu kwenye mambo makuu matatu. Sehemu ya kwanza ni ajira kwa vijana, jambo ambalo imekuwa ni kilio kwa vijana wa Kitanzania. Kwa sasa kumaliza elimu ya chuo kikuu imekuwa ni kama laana kwenye nchi yetu. Mpaka nasimama kuchangia hapa *message* za vijana waliotuma kwamba hebu waambie watuambie hatma ya sisi tuliomaliza vyuo vikuu toka mwaka 2015 ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la ajira ukiangalia ajira inayotokea kwa mwaka hailingani na idadi ya wahitimu kwa mwaka kwenye nchi yetu. Nataka Serikali

iye ituambie nini hatma ya vijana hawa wa toka mwaka 2015 mpaka leo? Kwa sababu kitu kingine ambacho kingewasaidia kujajiri ni upande wa kilimo, suala la kilimo liko hoi bin taabani.

*Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala hili la ajira kwa vijana sasa kumekuwa na suala la ubaguzi. Kwa sasa watu wanapotafuta ajira kuna maeneo imefikia wanaambiwa waoneshe Kadi yao ya Chama cha Mapinduzi. Naomba suala hili Serikali iliangalile kwa sababu ubaguzi huu hautaishia kwenye chama peke yake, athari za ubaguzi ni kubwa sana, zikianzia kwenye vyama zitakwenda kwenye makabila, zikitoka kwenye ukabila zitakwenda kwenye udini, ni vizuri Serikali ifuatilie jambo hili. Si kwamba limejificha kiasi kwamba hamuoni, kama mlikuwa hamjui mimi nawaambia kwamba kuna hilljambo kwenye suala la ajira sasa watu wanaambiwa wapeleke Kadi za Chama cha Mapinduzi jambo ambalo kwenye Katiba yetu ya nchi halipo. Sasa kama ni utekelezaji wa llani ya Chama ya Mapinduzi pia tujue kwamba ajira kwa sasa lazima uwe na kadi ya Chama cha Mapinduzi. (Makof)*  
**[Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]**

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo nitaenda kulizungumzia ni suala la kilimo. Tunapozungumzia kilimo, ni lazima tuzungumzie masoko na pembejeo.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Aida Khenani ukae. Mheshimiwa Antony Mavunde, kanuni iliyovunjwa.

#### **KUHUSU UTARATIBU**

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU (KAZI, VIJANA NA AJIRA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 64(1)(a) ambayo inazuia Mbunge kutotoa taarifa ambazo hazina ukweli. (Makof)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mbunge anayezungumza, anatoa taarifa kwamba kuna ubaguzi mkubwa kwenye eneo la ajira na kwamba ni lazima mtu aoneshe kadi ya CCM ndiyo aweze kupata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili siyo kweli. Matangazo yote ya ajira, huwa yanatoa vinavyohitajika kwa maana mwombaji awasilishe nini. Kwa hiyo, kwa sababu taratibu zimebekwa vizuri kabisa katika kila ajira ambazo zinatangazwa na mwombaji anatakiwa awasilishe nyaraka ambazo zimesemwa; na katika nyaraka hizo haijawayi kuwemo kadi ya Chama cha Mapinduzi kama kigezo cha mtu kupata ajira; hiyo kwa mujibu wa kanuni; na kwa sababu mimi nimethibisha kwamba siyo kweli, tunamtaka mtoa taarifa aondoe maneno yake au lah, athibitishe mbele ya Bunge lako tukufu na kanuni za Bunge hili ziweze kuchukua hatua. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, amesimama Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Waziri Mkuu, Ajira na Vijana, akitumia kanuni ya 64(1)(a) inayozungumzia mambo yasiyoruhusiwa Bungeni, lakini amesoma kifungu kidogo cha (1) kinachosema Mbunge hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli. Sasa ukishazungumza kuhusu taarifa ambazo hazina ukweli zinakupeleka kwenye kanuni ya 63 inayohusu kutokusema uongo Bungeni.

Sasa ukiisoma kanuni ya 63, huwa inamtaka anayemwambia Mbunge mwingine kwa maana ya mchangiaji kwamba amesema uongo, yeye anatakiwa kusema maelezo yake yanayoonesha kwamba yule Mbunge aliyetangulia kusema kabla yeye hajasimama na kusema kuhusu utaratibu, alikuwa akisema uongo.

Kwa maelezo ambayo ameyatoa Mheshimiwa Naibu Waziri na amesema kuhusu matangazo yanayotolewa na vigezo vinavyowekwa na kwamba kigezo ambacho alikuwa anakitaja Mheshimiwa Mbunge aliyekuwa akichangia hakipo kwenye ajira kama ambavyo yeye amekisema. Sasa kwa masharti ya kanuni inayokataza kusema uongo Bungeni,

Mheshimiwa Mbunge anapewa fursa ya kufuta usemi wake ama kuthibitisha.

Kwa hiyo, kwa mujibu wa Kanuni zetu tulizojiwekea nitampa fursa Mheshimiwa Aida Khenani kufuta kauli inayosema ajira Serikalini inataka mtu awe na kadi ya Chama cha Mapinduzi. Mheshimiwa Aida Khenani.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Ni vizuri tukaacha hofu. Nimesema wakafuatilie, ndiyo jambo nililozungumza, *Hansard* ziko wazi. Kwa kuwa umeniongoza, nayafuta, ila mimi nimesema na ni wajibu wa Serikali kwenda kufuatilia jambo hilo. Mitandao iko wazi, mambo hayo yako wazi kabisa yanaonekana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khenani, ili Taarifa zetu Rasmi za Bunge zikae vizuri, kama unasema unafuta kama ulivyzungumza, huwezi tena kuendelea kutoa maelezo juu ya jambo hilo hilo ambalo unalifuta. Kwa hiyo, lifute ili taarifa zikae rasmi, halafu uendelee na mchango wako.

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimefuta maelezo yangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazidi kusema, kama kuna nchi wanalia njaa kwenye Taifa lao, vijana wa Tanzania wanalia na ajira kwenye Taifa lao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda kwenye suala la kilimo ambalo tunaamini vijana wengi walikimbilia huko kujikita, lakini nako hali ni mbaya kupita kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la kilimo nitazungumzia masoko. Suala la masoko ya mazao mchanganyiko na mazao yote nchini, imekuwa ni shida kubwa sana kwa wakulima na sasa wanajiona ni kama hawana uhalali wa kuendelea na kilimo, hasa wakulima wa zao la mahindi wa Mkoa wangu wa Rukwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumza mwaka 2018 kwamba kabla ya tamko la Mheshimiwa Waziri Mkuu ndani ya Bunge kukataza wakulima kuuza mazao yao nje ya nchi hali ya mazao yao na bei halisi ilikuwa ni shilingi 75,00/=.

Baada ya tamko lile, baadaye akaja kuruhusu wakati huo tayari nchi ambazo zilikuwa zina uhitaji, hazihitaji tena, inakuwa ni hasara kwa mkulima. Ni vyema Serikali kabla ya matamko yake ikafanya kwanza tafiti kuliko kuwapa adhabu wakulima wa nchi hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pembejeo bado ni shida kwa wakulima wetu. Serikali ya Awamu ya Tano, *slogan* yake ni Serikali ya viwanda. Kwa nini sasa wasiweke kipaumbele cha kujenga viwanda zizalishwe pembejeo hapa ili kupunguza hali ngumu ya bei kwa wakulima wanaopata shida? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Ofisi ya Waziri Mkuu watakapokuja watuambie, wana mkakati gani wa kuanzisha viwanda vitakavyotengeneza pembejeo nchini ili kupunguza bei kubwa ya pembejeo ambayo inaenda kuwaumiza wakulima wetu? Bei kubwa ya pembejeo haiendani na hali ya bei ya mazao ambayo wanazalisha. Kwa hiyo, ni vyema, wakipunguza bei ya pembejeo itawasaidia hata uzalishaji wa kulima ambapo kilimo chetu sasa kitakuwa ni chenye tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, mahindi kwetu ni siasa, mahindi ni maisha na mahindi ni biashara. Hapa nataka kuzungumzia jambo moja, kwenye korosho fedha zimetoka kwenye Benki ya Kilimo. Sasa mimi sijui kama ile benki imebadilika imekuwa ni Benki ya Korosho. Kama ni mazao mchanganyiko, haya mazao mengine utaratibu ukoje? Ningependa kujua, Serikali ina mkakati gani na mazao mengine? Je, huu utaratibu utakuwa ni wa kila mwaka wa kuchukua pesa kwenye Benki ya Kilimo kwenda kununua mazao ambayo yatakosa soko?

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba ni iambie Serikali tu kwamba baba akinunua chakula nyumbani hapongezwi

kwa sababu ni wajibu wake. Kwa hiyo, tunategemea Serikali ni wajibu wenu kuhakikisha mnawatengenezea soko wakulima wanchi hii. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakwenda kuzungumzia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa. Mpaka leo mimi ni Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa. Jana limejibiwa hapa kwamba Wenyeviti wa Serikali wanalipwa shilingi 20,000 kama posho. Kabla sijamaliza muda wangu wa miaka mitano, nimezungumza hili jambo mara tatu ndani ya Bunge. Hili jambo inategemeana na makusanyo ya Halmashauri, kwa nini Serikali isilete heria hapa ambayo itakuwa *uniform* kwamba hawa Wenyeviti watalipwa posho kiasi gani? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Halmashauri sasa hali ni mbaya na huwezi kufananisha Mwenyekiti wa Sumbawanga MJINI ukamfananisha na Mwenyekiti wa Kinondoni kwa sababu zile Halmashauri za MJINI zitakusanya tofauti na Halmashauri za Vijiijini. Sasa kama Serikali ina uwezo wa kutenga fedha kwa ajili ya uchaguzi, kwa nini wasitenge fedha kwa ajili ya kuwalipa posho Wenyeviti wa Serikali? Kama jambo hili halijaandaliwa, ni vizuri kwa ushauri tu, kabla hawajajipanga na uchaguzi, wajipange kwanza ni namna gani wataanza kuwalipa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa? Hili jambo...

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI.

## TAARIFA

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Naomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge kwamba kabla uchaguzi wa Serikali za Mitaa haujafanyika, wananchi wenye sifa wanajipanga kwa nafasi ambazo wanahitaji; ama kuwa

Mwenyekiti wa Mtaa au wa Kijiji, au wa Kitongoji au Mjumbe wa Serikali ya Kijiji au Serikali ya Mtaa. Utaratibu ni kwamba kazi za Uenyeviti wa Mitaa ni kazi za kujitolea na ni lazima awe na kipato ambacho kinamwingizia maisha yake halali ili aweze kufanya kazi bila kumdhulumu mwananchi na bila kuiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika mazingira hayo, hata kabla posho haijapangwa, anakuwa anapanga na anakwambia kwa sababu zipi na ataishije?

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya pili ni kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Taarifa ni moja Mheshimiwa. Mheshimiwa Aida Khenani, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. AIDA J. KHENANI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza najua wana muda wa kujibu, sijui ana *pressure* ya nini; lakini pia alikuwa Mwenyekiti mwenzangu, anajua kwa nini hiyo nafasi ameikosa kwa wakati huu. Kwa hiyo, aniache Mwenyekiti nizungumze kwa sababu nawajua Wenyeviti wenzangu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hili suala la ukusanyaji wa mapato linategemea na uwezo wa Watendaji kwa maana ya Wakurugenzi, anaweza kubuni vipi vyanzo vya mapato? Kwa hiyo, hii hali itaweka utofauti mkubwa sana wa Wenyeviti juu ya posho zao. Kama Serikali inaweza kumwamini Mwenyekiti akaandika barua ya kumdhaminu mtu, inakuwaje ashindwe kutambua kwamba ana mchango gani ndani ya nchi hii? Ni kiongozi pekee wa Serikali wa Mtaa ambaye hana usiku, hana mchana, hana juu, hana mvua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuwaambia tu Serikali, kama bado hawajatambua mchango wa Wenyeviti, ni bora wafute suala hili la uchaguzi wa Serikali za Mitaa, wabaki wabaki Madiwani tu ambao wanapata posho. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, nilikuwa nimemtaja Mheshimiwa Balozi Adadi Rajab, atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Mollel. Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo, ajiandae.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami nashukuru sana kwa kupata nafasi hii ya kuweza kuchangia hoja hii muhimu sana ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Kwanza, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote kwa jinsi Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyopresent hoja yake kwa weredi mkubwa sana, kwa sababu ametumia *system* ya *PowerPoint* na mambo yote mazuri ambayo alikuwa anayasema tulikuwa tunayaona pale. Kwa hiyo, nampa hongera sana. Nategemea na Waheshimiwa Mawaziri wengine basi na wenyewe wata-present kwa *system* ya *PowerPoint* ili tuweze kuona kazi nzuri ambazo zinafanyika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kazi nzuri ambazo zinafanywa na Serikali ya Awamu ya Tano, tumeona kazi nzuri sana na nyngi sana ambazo hazijawahi kufanyika katika nchi hii katika kipindi kifupi. Tumeona mambo ya kisasa ambayo yanakwenda na ambayo yanafanyika kwa weledi mkubwa sana na miradi mikubwa sana. Sasa pamoja na kazi hiyo, nilitaka kuchangia kwenye sekta zifuatazo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaanza na suala la uchumi. Hivi karibuni Mheshimiwa Rais aliwaelekeza *TRA* kuangalia uwezekano wa kupunguza mapato kwa sababu kodi ambazo wanatoza ni kubwa sana *to the extent* kwamba wananchi wa kawaida wanashindwa kulipa kodi na badala yake wanatumia njia mbalimbali za kukwepa kodi au kukimbia nje ya nchi ili mradi tu wawewe kuona kwamba watafanya vipi kukwepa kodi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Rais aliposema *TRA* ni lazima waangalie namna gani wanaweza kupunguza kodi, wananchi wasiweze kukimbia kulipa kodi. Hivi karibuni tulikwenda Kampala kuangalia wenzetu

wanafanya kwenye *Treasury Single Account*. Kule Kampala pamoja na mambo mengine tulikutana na Watanzania wengi. Watanzania ambao wanatoka hapa wanakwenda Kampala kununua bidhaa na kuzirudisha hapa, bidhaa hizo hizo zimepita kwenye bandari yetu hapa hapa na zimekwenda na baadaye wale wale wanazifuata kuzirudisha hapa. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hii *system* kwa kweli ni kitu ambacho Mheshimiwa Rais alikuwa anasema. Kwa sababu hapa ilikuwa ni kama *hub*, ilikuwa ni kana Dubai, tuna bandari sisi. Walikuwa wanakuja wafanyabiashara wengi, Afrika Kusini, Zimbabwe, Malawi, Zambia, wote walikuwa wanakuja hapa. Sasa wamehama wote, tumewakuta kule. Sasa ni vizuri suala hili likaangaliwa. Tiliongea na Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwenye Kamati na aliahidi kutuma watu ili kuangalia kwamba tutaweza kulirekebisha namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni muhimu sana watu waende kwa sababu tunafanya mambo mazuri sana juu kule, miradi mikubwa sana inafanyika, lakini bado sasa hivi tuangalie namna gani tunaweza kupunguza kodi, namna gani tunaweza kufanya wananchi wetu kulipa kodi bila ya kukimbia au bila kufanya mchezo mwingine. Kwa sababu hapa karibuni tu kule Tanga kuna kiwanda kikubwa sana cha Pembe ambacho ni cha ngano; jamaa kafunga kiwanda kwa sababu ya kukimbia kodi. Kafunga kiwanda na kageuza mambo mengine; kwa mfano, magari yake sasa yanasonomba mchanga au kitu kingine chochote. Kwa hiyo, ni suala muhimu sana ambalo naomba liangaliwe kwa undani wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni suala la hizi ndege zetu ambazo zimekuja. Tunategemea ndege hizi zifanye, nimeona faraja sana kwa sababu tulikwenda na *Airbus* mpaka Kampala na tukaja kuchukuliwa na *Airbus* hiyo. Kwa kweli tulipofika *K/A* ilijaa kabisa ile ndege. Kwa hiyo, ni fahari kubwa kwamba hizi ndege zina umuhimu wake na zitasaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu sikuona akitaja uwanja wa ndege wa Tanga. Tunategemea nasi tupate ndege ya *Bombardier* iweze kushuka pale. Sasa nategemea wakati Wizara itakapokuja kutoa taarifa zake, basi itaona kwamba Tanga sasa hivi kwa sababu ya umuhimu wake, wawekezaji wengi wanakuja, basi nasi tuweze kupata ndege ambayo itakuwa pale Tanga. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ambalo nataka kuchangia ni wawekezaji. Ni kweli ukiangalia kwenye taarifa ya Mheshimiwa Waziri Mkuu kwenye *World Investment Report* ya mwaka 2018, sisi tunafanya vizuri sana hapa Afrika Mashariki. Pamoja na kufanya vizuri, inabidi tuangalie kituo chetu hiki cha *TIC*. Tunategemea *TIC* tumeita ni lakini ni lazima tuhakikisha kwamba ni kweli *real One Stop Center* kwa ajili ya kuwaweka hawa wawekezaji ili mwekezaji akifika pale, hana sababu ya kuzunguka kwenda mahali pengine popote. Ni kuhakikisha kweli vibali vyote, leseni na vibali vyote vya kuishi nchini vinapatikana bila matatizo yoyote. Bila kufanya hivyo, itakuwa ni *delays* ambazo hazina umuhimu. Mara nyingi sana wanapofanya *assessment* hasa za mambo ya *corruption* na uboreshaji wanaangalia hizi *systems*, wawekezaji wanakuwa *handled* namna gani? Unatoa leseni kwa muda gani? unachelewesha kwa muda gani? Je, kuna *land bank* pale kwenye kituo chetu? Kwa sababu mwekezaji hawezи akaja ukamwambia basi nenda katafute ardhi sehemu nyingine, kuna huyu jamaa uende ukaongee naye. *No*, inatakiwa akija pale kweli ni *One Stop Center*, anakutana na kila kitu; kama ni ardhi anaoneshwa, unataka hapa au hapa? Basi yeye ni juu yake kuangalia kwamba anataka sehemu gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni muhimu sana kurekebisha vitu kama hivyo. Ni muhimu kwenye Wizara ya Mambo ya nchi za Nje ikafungua kitengo kabisa. Sasa hivi Mabalozi nje kule wamehamasishwa sana na wanatafuta wawekezaji kwa bidii sana. Sasa itakuwa wawekezaji wanatafutwa, wanakuja pale, halafu *Foreign Affairs* wanakuwa hawana kitengo au *department* maalum ya

kuwashughulikia au kupokea wawekezaji, badala yake Balozi atoke nje aje nao mpaka hapa, aanze kuzunguka kwenda huko.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu ya *Foreign Affairs* kuweka mazingira mazuri na ni jukumu la *TIC* kuweka mazingira mazuri. Ninaamini kabisa kwa sababu imekuwa ni Wizara maalum, basi Wizara hiyo itashughulikia mambo haya yaweze kwenda vizuri tuweze kupata wawekezaji wazuri zaidi. Ni vizuri ndege yetu hii *Dreamlinersasa* ikaanza kufanya kazi, kwa sababu itategemea kwa sababu hakuna mwekezaji ambaye anafurahia kwenda na *direct flight*. Hakuna mtalii ambaye anafurahia kupata ndege ya *direct flight* badala kuingia kwenye *transit* kwenye Miji mingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni vizuri hizi ndege zianze kufanya kazi tuweze kupata watalii wengi na tuweze kupata wawekezaji ambao ni wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho ambalo nilitaka kuchangia ni suala maji. Maji hasa Muheza ni siasa. Juzi juzi Kamati walikwenda kule na wenyewe watanisaidia kudhihirisha kwamba tuna tatizo kubwa la maji Muheza na tuna tatizo kubwa la maji sehemu mbalimbali hapa nchini. Kuna mradi ule wa shilingi bilioni 500 ambao *ofcourse* nitakuja kuongelea nkipata nafasi kwenye Wizara ya Maji. Suala hilo tunamsubiri Mkandarasi Mshauri (*Consultant*) kutoka India. Sasa tumekuwa tunamsubiri na taratibu nyingine, sasa sijui ni miezi mingapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Wizara ya Maji, kama ni kumsubiri, kwa nini tusitume mtu mara moja kwenda India na kurudi na hivyo vitu ambavyo vimebakia?

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Amina Mollel atafuatiwa na Mheshimiwa Sonia Jumaa Magogo, Mheshimiwa Dkt. Lemomo Kiruswa ajandae.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba ya Waziri Mkuu kwa mwaka huu wa fedha 2019/2020. Awali ya yote namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uzima na kuwepo hapa, bila ye ye tusingekuwepo hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa naomba na naonesha kutokana na jinsi ambavyo Ofisi hii ya Waziri Mkuu na pia Rais kupitia Serikali hii ya Awamu ya Tano kwa jinsi ambavyo wamekuwa wakifanya kazi na hasa katika masuala ya watu wenye ulemavu yalivyopewa kipaumbele. Hii inaonesha kwamba Serikali yetu ni sikivu, inasikiliza wanyonge na inasikiliza hoja mbalimbali ambazo zinatolewa na kwenda kuzifanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa kwa kuanza kuzungumzia Mfuko wa Watu Wenye Ulemavu; tarehe 2 Februari, 2017 niliuliza swali kuhusiana na Mfuko huu na nilisema kwamba kwa sababu Mfuko huu na masuala yote ya watu wenye ulemavu yapo pia katika mkataba wa Kimataifa wa watu wenye ulemavu wa mwaka 2006, lakini pia Sera ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2004 inazungumzia pia haki za watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu tumekuwa tukizungumzia na kuishauri Serikali kuona ni kwa jinsi gani wanatatta changamoto mbalimbali zinazowakabili watu wenye ulemavu na tulidai Mfuko kuhusiana na watu wenye ulemavu lakini pia tukadai bajeti kuhusiana na Wizara hii kwamba tayari tunaye Naibu Waziri na kama tunaye Naibu Waziri tulihitaji kwamba kuwepo na bajeti maalum. Kwa mfano mfuko huu kwa mwaka 2017 haukutengewa fedha, lakini mabadiliko makubwa tumeyaona katika bajeti hii ya mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa nampongeza mwenzangu Mheshimiwa Naibu Waziri, Ikupa Alex, kwa ushauri mzuri ambao ameweza kuutoa kwa kushirikiana kwa pamoa hatimaye sasa kwa kweli tunajivunia

kuona kwamba kitengo cha watu wenye ulemavu kimetengewa fedha. Kwa kuanza kwa mwaka huu ambayo ni *subvote* 2034 na imetengewa zaidi ya bilioni moja na naamini kabisa huu ni mwanzo, tunapokwenda ni pazuri na tutaweza kuongezewa pia hiyo bajeti. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hili kwa kweli nampongeza sana Waziri mwenye dhamana, dada yangu Mheshimiwa Jenista Mhagama yeeye ni jembe lakini pia niwapongeze Manaibu Waziri, Mheshimiwa Mavunde na Mheshimiwa Ikupa. Jembe lingine ambalo limeongezeka katika Ofisi hii nimpongeze sana Mheshimiwa Angella Kairuki, lakini pia naamini kabisa ni kutokana pia na Makatibu Wakuu waliopo ambao na wao kwa kweli kipekee nawapongeza sana kwa mchango wao katika kuwasimamia na kuwashauri vizuri Mawaziri hatimaye tunakwenda pamoja sasa. Nawapongeza sana na nimpongeze sana Katibu Mkuu baba yangu Massawe. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na pongezi hizo na kazi nzuri ambazo kwa kweli zimefanywa na Serikali ya Awamu ya Tano, napenda kushauri mambo mawili, matatu ili basi kuona kwamba ni kwa jinsi gani na kama ilivyo sisi ni kiunganishi katika ya Serikali na wanachi na wajibu wetu ni kuwasimamia Serikali na kuishauri. Napenda kuishauri Serikali katika mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwamba tumeona tunacho kitengo na tayari tumekwishatengewa fedha. Naishauri Serikali kuona umuhimu sasa kutoka kwenye kitengo na kwenda kwenye idara kamili ambayo idara hii ndiyo itakuwa Idara ya Watu Wenye Ulemavu na siyo kitengo. Huu ni ushauri wangu naomba sana watakapoendelea basi waone kwamba ni kwa jinsi gani tunakwenda kufikia huko na kuwa Idara ya Watu Wenye Ulemavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, miundombinu bado siyo rafiki katika majengo mengi na hata ya Serikali pia kwa watu wenye ulemavu. Bado miundombinu siyo rafiki na hata baadhi ya majengo mengine watu hawazingatii. Nawaomba

waliopewa dhamana ya kulismamia hili kuona kwamba tunaweza kuondoa changamoto zote hizi ambazo zinawakwamisha watu wenye ulemavu kuweza kushindwa kutimiza majukumu yao au kwenda maeneo ambayo wanapaswa kwenda kufuatilia haki zao au kushughulikia yale mambo ambayo ni muhimu kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nimpongeze Naibu Waziri wa Kazi, Ajira pamoja na Mkurugenzi wa Ajira, Bwana Msaki kwa kazi nzuri wanayofanya. Mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Katiba na Sheria na tunaisimamia Ofisi ya Waziri Mkuu. Tumeshuhudia ni kwa jinsi gani ambavyo Waziri mwenye dhamana, kwa ujumla Ofisi hii kwa jinsi ambavyo wanafanya kazi na tunesikia kwamba watu wakilalamika kuhusu suala la ajira na tunapoolekea hata Marekani bado tatizo la ajira lipo na ni nchi zillizoendelea. Kwa kuona kwamba Serikali haiwezi pia kuwatimizia wananchi wake wote kuwapa ajira, Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi na Ajira wao wameandaa utaratibu mzuri ambaao wanakusanya maoni na hasa vijana mbalimbali ambaao wamemaliza Chuo Kikuu, wanatuma maoni na maombi hatimaye Ofisi hii kwa utaratibu mzuri ulioandaliwa wanapelekwa katika Taasisi mbalimbali ikiwemo mabenki. Kule wanakwenda wanapata ujuzi na wengi tayari hivi sasa kule walikopelekwa wamekwishapata ajira na kuchukuliwa na mabenki na maeneo mengine tofauti tofauti. Hii ni kazi nzuri inayofanywa na Ofisi ya Waziri Mkuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile bado utaratibu mzuri ambaao umeandaliwa katika suala zima la kilimo na tumekuwa tukizungumza hapa kilimo cha kutegemea msimu wa mvua siyo kilimo ambacho kitawezu kutukomboa. Serikali yetu imekuja na utaratibu mzuri wa kuona ni kwa jinsi gani tunalima katika kilimo biashara, kilimo chenye tija kwa kuona ni kwa jinsi gani tunalima kwenye kilimo cha kutumia maji hasa kilimo cha umwagiliaji. Ofisi hii utaratibu mzuri iliyoandaa katika Halmashauri zetu hivi sasa katika kila Halmashauri vijana wanatakiwa zaidi ya 100, Halmashauri zetu zimeandaa baadhi ya maeneo na vijana hawa wanapewa ujuzi, wanajengewa nyumba-vitalu yaani *green house* ambazo

wanapewa ujuzi kuweza kujua ni kwa jinsi gani wataweza kulima mazao ya kule ndani kwenye bustani hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mazao hayo yatakuwa ni mazao ambayo kwanza ni yenye ubora, ni mazao ambayo yataweza kuuzwa katika maeneo tofauti tofauti na yataweza kuwakwamua vijana wale na vijana hao watakaokuwa wamepata huo ujuzi watatoka sasa pale. Tunayo mabenki yetu, naamini kabisa Serikali itawawezesha vijana hawa ili basi waweze kujitegemea badala ya kutegemea hasa ajira kutoka Serikalini. Huu ni utaratibu mzuri unaoandaliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu na tayari vijana wapo *site* wanafanya kazi hiyo. Halmashauri zetu tunaziomba sana zihakikishe kwamba zinasimamia zoezi hili na kutoa ushirikiano kwa walengwa ili waweze kufanyia kazi hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitakuwa mchoyo wa fadhila kama kweli sitawazungumzia *OSHA* pamoja na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Tulikuwa na malalamiko mengi kwa *OSHA*, lakini hivi sasa *OSHA* wameondoa vipengele vingi ambavyo vilikuwa ni kero kwa wawekezaji na vipengele hivyo vimeondolewa hivi sasa na tumeona kwamba, pamoja na kuondoa vipengele hivyo, wawekezaji sasa wengi wamekwenda, vibali vinatolewa kwa muda muafaka, lakini pia wanapata fedha kutokana na vibali hivyo. Kwa hiyo, napongeza sana huu utaratibu unaofanywa na nimpongeze sana Mkurugenzi wa *OSHA*, Bi.Khadija kwa kazi nzuri sana anayofanya.

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja na naishukuru sana Serikali.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimetaja Mheshimiwa Sonia Magogo atafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Lemomo Kiruswa, Mheshimiwa Hamida Mohamed ajiandae.

**MHE. SONIA J. MAGOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia. Awali ya yote ningependa kuupongeza uongozi mzima wa Chama changu cha Wananchi (*CUF*) ukiongozwa na Mwenyekiti wetu mahiri kabisa, Profesa Ibrahim Haruna Lipumba kwa kuaminipa na Wanachama wote na kupewa tena ridhaa ya kukiongoza chama chetu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende moja kwa moja kuchangia kwenye hoja na nitaanza na suala la uwekezaji. Katika kuwekeza, Serikali pia inawekeza kwenye Mashirika ya Umma ambayo yapo nchini kwetu na inaweka mtaji wake kwa lengo la kupata gawiyo ambalo litakuja kuisaidia Serikali katika shughuli zake mbalimbali za kuinua uchumi pamoja na huduma mbalimbali za jamii na tumeona mwaka jana baadhi ya Mashirika haya yametoa gawio zuri kwa Serikali. Ndhani kama Ofisi ya Msajili wa Hazina ambayo ndio msimamizi mkuu wa mashirika haya, ikiwezeshevizuri na kupewa bajeti ya kutosha na kwa wakati ikayasimamia zaidi haya mashirika gawio hili litaongezeka maradufu ya lile ambalo tulipata mwaka jana.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ningependa kuongelea kuhusu wazee waliokuwa wa Jumuiya ya Afrika Mashariki. Wazee hawa waliitumikia nchi yetu kwa uaminifu, walisaidia kuleta mahusiano mazuri baina ya nchi yetu na waliokuwa Washirika wetu wa Afrika Mashariki, lakini bado wazee hawa wanahangaika kila kukicha na madai ambayo bado hayajapata suluhu mpaka leo. Kumekuwa kuna kesi mbalimbali wanaendesha, kwa hiyo, inabidi wakati mwingine watoe michango kwa ajili ya zile kesi, wakati mwingine inabidi wasafiri kutoka sehemu mbalimbali kuja Dar es Salaam kwa ajili ya mikutano yao ya kukutana kufuatilia madai na ukizingatia wazee hawa hali yao ya kiuchumi siyo nzuri. Kwa hiyo napenda kuishauri Serikali katika suala hili watoe tamko rasmi kwa hawa Wazee. Kama kuna chochote ambacho wanadai basi Serikali iwalipe ili waweze kupumzika na kama hakuna madai vilevile lingetoka tamko ili wakajua ni nini ukweli wa haya madai ambayo wanafuatilia kila siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, kingine bado nipo kwa Wazee na nazungumzia suala la pensheni wanayopata kila mwezi. Kwa kweli *pension* wanayopata kila mwezi baadhi ya Wazee ni ndogo. Kumlipa Mzee *pension* ya chini ya kiwango cha laki moja kwa mwezi ni kama unamwonea. Tukilinganisha hali ya maisha tuliyonayo kwa sasa na kile kiwango wanachopata, wazee wale wana familia, wazee wale wanatunza wajukuu lakini kile kiwango wanacholipwa kwa ajili ya kuendesha maisha yao ni kidogo sana. Hivyo naiomba Serikali iangalie inawasaidiaje ili kuongeza hiki kiwango cha pensheni ya kila mwezi hawa wazee waweze kujikwamua na umasikini ambao wanao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi nikizingatia wazee hawa pia hawana mfuko maalum kama walivyo vijana, walemvu, wanawake ambao wanapata asilimia 10 kwenye Halmashauri zao, lakini kwa upande wa Wazee wao hawamo katika hii asilimia 10. Kwa mujibu wetu ni kwamba vijana wanaishia miaka 45. Kwa hiyo, kuanzia miaka 46 tunasema tunawachukulia kwamba wapo kwenye kundi la Wazee, lakini bado ni watu ambao wana nguvu, wanaweza kuitumikia nchi yetu, wanaweza kujenga uchumi. Kwa hiyo, wakiwezeshwa na Serikali kama wanavyowezeshwa vijana, akinamama na walemvu nao wataweza kuchangia kwenye uchumi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni vijana; mara nyingi tumekuwa tukiwalaumu vijana kwamba wana akili mgando ya kutaka kuajiriwa hawataki kujajiri. Hata hivyo, hili mimi nalitazama kwa mtazamo mwingine kwamba, je, hawa vijana tunawaandaa vipi ili waje kujajiri? *System* yetu ikoje kuanzia shule ya msingi, sekondari hata vyuoni, wanaandaliwa vipi ili baadaye wanapomaliza elimu yao waje kujajiri na kuondokana na lile wimbi la kuwaza kwamba nitaajiriwa, nitaajiriwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, hapo hapo kuna wale ambao wana mawazo yale ya kujajiri lakini mazingira yenewe ya kujajiri yanakuwa ni magumu. Mlolongo wa kuanzisha mathalan biashara au sehemu yake ya kazi

unakuwa ni mrefu sana au unakuwa na gharama ambazo yule kijana anashindwa kuzikidhi na kuweza kufungua biashara yake na kujajiri. Pia wakati huo huo tuna mapori mengi sana katika Tanzania yetu. Ingewezekana Serikali kuwakusanya wale vijana kwenye makundi, kuwapatia zana za kilimo ama kwa kuwakopesha au kuwasaidia wakawenza kuanzisha kilimo na kuweza kuendeleza uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwenye ndugu zetu wale mavu; kumekuwa na kesi mbalimbali za wale mavu na wengine wanababishiwa ulemavu huo na watu ambao ni wageni katika nchi yetu, labda wawekezaji ama watu mbalimbali. Hata hivyo, zinapokwenda zile kesi za hawa ndugu zetu wale mavu na ukiangalia na mazingira ambayo wanakuwa tayari wanayo zile kesi zinachukua millongo mingi sana, zinakuwa na ucheleweshwaji ndani yake hivyo kuwasababishia kuwa na maisha magumu zaidi. Hivyo, ningependa pia Serikali iwasaidie hawa ndugu zetu kwa kuwasimamia kwenye kesi zao na kuwahakikisha ufumbuzi unapatikana haraka kwenye hizo kesi ili waweze kuendelea na harakati za maisha yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Sonia hasa kwa utetezi wako kwetu sisi wazee, nawashangaa wazee wenzangu humu ndani wamenyamaza kimya. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Dkt. Lemomo Kiruswa, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Muro, Mheshimiwa Hamida Abdallah ajiandae.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii ili nami niweze kuchangia katika hotuba hii ya bajeti ya Waziri Mkuu. Nitangulize pongezi zangu za dhati kwake yeye Waziri Mkuu na timu yake yote kwa kazi nzuri wanayoifanya na kwa jinsi walivoiratibu na kuangazia masuala chanya ya maendeleo yanayoendelea katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nitumie fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Longido kutoa shukurani zangu za dhati kwa sababu ya maendeleo chanya yaliyoonekana na kushangiliwa na wananchi wa Longido katika Serikali hii ya Awamu ya Tano ambapo mradi mkubwa kabisa wa maji kutoka Mlima Kilimanjaro uliogharamiwa kwa jumla ya shilingi bilioni 15.9 hatimaye umefika Longido, watu wamepata maji safi na salama na mengi na ya kutosha. Wananchi wa Longido wamesherehekea na wanaendelea kufurahia, sasa watu wanaweza wakaoga hata mara tatu kwa siku kwa sababu yale maji yamekuja kwa wingi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa sababu kulikuwa na ahadi za Serikali za kuendeleza maji haya yawafikie na majirani waliko pembezoni mwa bomba hilo kubwa katika vijiji mbalimbali kuanzia kule maji yanapotokea Kata ya Olmolog Kijiji cha Eleral; Kata ya Sinya, Kijiji cha Sinya; Kata ya Tingatinga, Kijiji cha Ngereyani na hivi vijiji vya pembezoni mwa Longido hadi Kimokouwa na Namanga ambapo hata Rais mwenyewe alipokua kuzindua ule mpaka wa pamoja alitolea tamko kwamba nao wamepelekewe maji hayo. Kwa kweli Longido wameona haya maji kama ni uzima, wamepewa maisha na mimi nakumbuka kila nikipita pale Moshi kuna mnara wa Askari ambapo kuna *sloganchini* yake inasema "maji ni uhai" nikawa najiuliza kwa nini Askari anashika bunduki anaelekeza Mlima Kilimanjaro kumbe analinda uhai. Maji ni uhai, ni ya kulindwa, ni ya kuenziwa na wananchi wa Longido wamefarijika sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia wananchi wa Longido kwa mwaka huu wamepata mgao mkubwa wa fedha za kujengewa hospitali ya Wilaya ambayo hatukuwahi kuwa nayo. Hospitali ya Wilaya imetengewa bilioni moja na nusu bila kuhesabu vituo vya afya viwili ambavyo vimejengwa viko katika hatua ya umalizaji, japo bajeti imekwisha lakini naamini bajeti hii itawapa watu wa Eworendeke na Engarenaibor fedha za kumalizia na moja ambayo wananchi kwa ari kabisa wa Tarafa ya Ketumbeine nao wameanza kuijenga kwa nguvu yao wenyewe mpaka wamefikia hatua ya kupaua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya shukrani hizo kwa sababu nataka tu kuonyesha ni kwa jinsi gani Serikali hii inawaenzi wananchi wake tena watu wa Wilaya za pembezoni kama Longido, sasa napenda kuchangia katika hotuba hii ya Waziri Mkuu kwa kudonoa baadhi ya mambo machache ambayo nime-*note*. Kwa suala la ardhi kuna hii sera ya Serikali inayosema kwamba Mpango wa Taifa kufikia mwaka 2033 ni kuhakikisha kila kipande cha ardhi ya Tanzania kimemilikishwa na kinamilikishwa baada ya kupangwa na kupimwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa angalizo kama Mjumbe wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Utalii kwamba tulivyofanya ziara katika baadhi ya mikoa inayopakana na nchi za jirani tumeona ardhi yetu inavamiwa hovyo kabisa na sisi Watanzania naona ardhi yetu ni kubwa hatujakaribia sana ile mipaka kama wenzetu. Tumetembelea mipaka yetu na Rwanda, Uganda, Kenya upande wa Tanga maeneo ya Horohoro tukashangaa nchi za jirani zimejenga mpaka zimeingia katika ardhi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiunganisha suala hilo na hili la barabara, wao wametengeneza barabara za kuzunguka mipaka yao lakini sisi hatuna. Kwa sababu tumedhamiria kufanya hilo zoezi la kupima na kumilikisha kila kipande cha ardhi, naomba kuiasa Serikali ilipe kupaumbele zoezi hilo ili twende kwa kasi kubwa tuweze kuimarisha mipaka yetu na kuilinda hiyo rasilimali muhimu ya ardhi ambayo ndiyo chimbuko letu sisi sote.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia hili suala la barabara ni la muhimu sana katika kuzunguka hii mipaka yetu maana tulikuwa tunaenda mpaka nchi ya jirani ndiyo tuone *beacon*. Hili jambo siyo salama na ni lazima Serikali sasa ione umuhimu wa kutenga fedha za kutosha ili kuimarisha hiyo yetu mipaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija kwenye suala lingine la msingi la mawasiliano, katika hotuba ukurasa wa 51 yameongelewa mawasiliano ya Mkongo wa Taifa lakini kuna kipengele muhimu ambacho sijakiona mawasiliano ambayo

nafikiri ni sehemu ya huduma za jamii, mawasiliano ya simu za mkononi. Sasa hivi simu ni kama sehemu ya uhai wetu, ukitaka kujua hebu Waheshimiwa Wabunge wote waambiwe waache kutumia simu kuanzia asubuhi mpaka jioni. Biashara zinaendeshwa kwa simu, mawasiliano na kila kitu kinafanyika kwa simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, wananchi wengi katika baadhi ya maeneo nchi hii bado hawana hiyo huduma ya simu. Naomba zaidi Serikali itilie mkazo maeneo ya mpakani. Tumezungumza hiyo mipaka nilioitaja kila mpaka wenzetu wa nchi tunayopakana nao wao wana minara ya simu na watu wetu wanatumia minara ya simu ya nchi nyiningine wakati suala hilo pia ni la kiusalama. Naomba Serikali yetu iwekeze katika kusimamia ule Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote, wawekezaji au wadau wa mitandao ya simu minara ijengwe katika vijiji vinavyopakana na mipaka ili kuimarisha ulinzi na ili wananchi wetu walio katika hii mipaka wapate minara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukianzia katika Wilaya yangu ambayo kilomita 300 tumepakana na nchi jirani ya Kenya ukienda Kata ya Kamwanga nusu ya watu wanatumia minara ya Kenya. Ukienda Kata za Matale, Wosiwosi na Kilailungwa wote wanatumia minara iliyoko Kenya na kuna Kata ndani ya Wilaya yangu ambazo hazina mawasiliano na Watanzania wale nao wanaona kwamba sasa ifike wakati wapewe minara ya simu kwambabu tuko karne ya teknolojia ya mawasiliano ya kielektroniki.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kugusia suala la mifugo. Ni kweli mifugo ni sekta ambayo haijapewa kipaumbele katika nchi hii. Kwa masikitiko niseme kwamba kuna zoezi lilitanyika la kuwadhibiti watu wanaovusha ng'ombe kupeleka Kenya katika mipaka ya Wilaya yangu, wale watu kweli walionewa. Sheria tumeweka sisi tukaweka na faini ambazo siyo za kiulihalisa na wananchi wale walikuwa wanakwenda kule kwa sababu hatuna masoko. Sasa hivi sisi tuna kiwanda cha mwekezaji kinajengwa mpakani kitakamilika mwezi Oktoba basi naomba Serikali

ijihushe na kuweka mikakati thabiti ya kuhakikisha kwamba masoko ya uhakika yatapatikana. Serikali itoe bei elekezi kama inavyotoa katika mazao ya kilimo, waangalie minada ya nje wapange kabisa bei ambayo itawafanya wafugaji na wafanyabiashara wa mifugo wasipate sababu ya kutaka kuvusha ng'ombe na kuuza kwenye masoko ya ndani. Kwa kufanya hivyo, zile bidhaa nyingine kama ngozi, pembe, mifupa, kwato zitaweza kuongeza mnyororo wa thamani kwa sekta hii ya ufugaji.

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa muda wako umekwisha.

**MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja. *(Makof)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mary Muro atafuatiwa na Mheshimiwa Hamida Mohamed na Mheshimiwa Ritta Kabati ajiandae.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba iliyopo mezani. Kwanza namshukuru Mungu kwamba nina afya njema, kwa hiyo nitakuwa niko vizuri kuweza kuchangia yale ambayo naona ni muhimu kwa ajili ya Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuanza na suala la hifadhi ya jamii. Hifadhi ya jamii mifuko iliunganishwa ya LAPF, GEPF na PPF ikaunda PSSSF. Kwenye kitabu chao ukurasa wa 70 wanahitimisha kwa kusema hatua hii imewezesha kutatua kero za wastaafu ambazo zilidumu kwa muda mrefu lakini ukiangalia kwenye uhalisia ni kwamba wastaafu wengi wanahangaika sana kupata mafao yao. Nina ndugu zangu ambao mpaka leo hii wana mwaka mzima hawajapata mafao. *(Makof)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Ukiachia hao wastaafu, kuna watoto ambao waliachwa na hao ambao walikuwa ni wafanyakazi na walijunga katika mifuko hii. Nina watoto yatima ambao ninaishi nao kuanzia Januari mpaka sasa hivi ni mwezi Aprili hajalipiwa ada ya shule. Wakati nafuatilia nimekuta na akina mama wengi sana ambao wanalamikia suala la watoto wao kutolipiwa ada na sasa watoto wako majumbani hawaendelei na shule. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ukiangalia wanavyohitimisha kwamba eti kero zimepungua, sijaona kwamba kero zimepungua kwa mifuko hii kuunganishwa labda Serikali ijipange upya kuhakikisha kwamba tatizo hili linapungua. Nafahamu kabisa hii Wizara ina wanawake wengi, Makatibu Wakuu watatu kama sio wawili ni wanawake, Mheshimiwa Waziri wa Nchi ni mwanamke, kwa kiasi nillichokutana na wale wanawake wanahangaika na watoto mitaani huko hawasomi kwa sababu waume zao wamefariki na mifuko hii tangu imeunganishwa watoto hao wanapata shida kulipiwa mafao yao ya elimu, kwa kweli naomba Serikali mkajipange vizuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua kabisa Mheshimiwa Jenista unasikia na unafahamu jinsi gani akina mama wanateseka katika kuhangaika na hawa watoto. Nakupa mifano hiyo miwili kwamba nina watoto wa ndugu zangu tena kaka yangu ambaye ananiachia ziwa, mpaka sasa hivi tangu mwezi Januari hawajalipiwa ada. Nimejaribu kulipa na mimi napokea posho kama watu wengine nimeshindwa, ina maana hao ambao hawana hata ndugu wa kuwalipia hali yao ikoje? (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuhamia sehemu ya Mahakama. Napenda kusema kwamba Mahakama ni mahali ambapo tunatakiwa tupate haki na kama haki na kwa wakati. Ukiangalia jinsi kesi zinavyocheleweshwa Mahakamani imesababisha msongamano mkubwa sana wa mahabusu na ukienda magerezani unakuta hali ni mbaya sana ambayo imesababishwa na ucheleshwaji wa kesi

ambazo zingeamuliwa kwa haraka ina maana mahabusu kule magerezani wangebungua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa tunapanga bajeti ya kulisha watu magerezani ni kwa sababu tumeshindwa kuwa na kesi zinazoenda haraka ili kupunguza mahabusu, ukipunguza wafungwa maana yake umepunguza na bajeti ya Serikali. napenda kuwaambia Serikali kama tunataka kupunguza gharama za kuendesha baadhi ya mambo ni pamoja na kuhakikisha kwamba kesi zinaendeshwa haraka. Kwa kufanya hivyo, tunapunguza gharama za uendeshaji wa Serikali na pia tunaongeza pato kwa sababu kesi zikiisha haraka watu wanaenda kufanya kazi zao walizozizoea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho nakishangaa sijajua kama msongamano ulioko magerezani na ile mito ndoo ambayo inawekwa kule zote hizo ni adhabu za huyo mtu ambaye amefungwa au ni nini? Haki za binadamu ziko wapi kumfanya mtu aishi na kinyesi? Kwa nini Serikali isitengeneze vyoo hata kama maeneo ya kulala ni finyu lakini vyoo vingetengenezwa kulikoni watu wanalala na vinyesi, haki ya binadamu inakuwa wapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia habari za UKIMWI. Tunafahamu kabisa UKIMWI ni janga la Taifa na Serikali inajitahidi kuhakikisha kwamba dawa za kufubaza ugonjwa wa UKIMWI zinapatikana lakini watu hawafi kwa sababu ya wadudu wale wa UKIMWI wananchi wengi wanakufa kwa sababu ya magonjwa nyemelezi magonjwa kama Kifua Kikuu, kuharisha na kadhalika ambayo tumekuwa tukisema humu ndani mara nydingi kwamba kama ARV ingekuwa na *package* ya *Seprin*, it means wananchi wenyewe magonjwa nyemelezi wangeweza kupata dawa hizo na wakapona. Kama tunawapa dawa za UKIMWI hatuwapi dawa za magonjwa nyemelezi wagonjwa wengi wanakufa kwa magonjwa nyemelezi na wala sio kwa ugonjwa wa UKIMWI wenyewe. Kwa hiyo, naiomba Serikali ifanye mkakati wa kuweka *Seprin* kwenye *package* ya *ARV* ili mtu anapopewa dawa za *ARV* apewe na zile za *Seprin* zitasaidia

anapopata magonjwa nyemelezi anatumia zile dawa.  
(*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ni tatizo la vituo  
vya kupimia UKIMWI.

## TAARIFA

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika,  
taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mary Muro kuna taarifa

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika,  
naomba tu kumpa taarifa Mheshimiwa anayechangia hivi  
sasa kwamba si kila mgonjwa anayepewa dawa za *ARV*  
anahitaji kupewa *Septrin*. Tunachotaka kushauri wagonjwa  
wote au watu wote wanaopata huduma ya *ARV* ni vizuri  
wanapojisikia tofauti waende kwenye vituo vyao kwa ajili ya  
kutibiwa, watapewa dawa zingine kwa sababu watakuwa  
wanapewa zile kule lakini sio lazima *package* ya *ARV* apewe  
na *Septrin*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa taarifa  
hiyo. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mary Muro, unaipokea  
taarifa hiyo.

**MHE. MARY D. MURO:** Mheshimiwa Naibu Spika,  
kwanza ningeomba wasubiri baadae watajibu, lingine ni  
kwamba vituo vilivyo vingi watu wanapewa sawa dawa za  
*ARV* lakini wanapokuwa na magonjwa ya nyemelezi hakuna  
*Septrin*. Sasa tunaweza tukawauwa hawa watu kwa kukosa  
*Septrin* na sio *ARV*. *ARV* zinapatikana na ugonjwa wa UKIMWI  
shida ni magonjwa nyemelezi na wala sio ugonjwa wa  
UKIMWI wenyewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongea vituo  
vya kupimia UKIMWI. Kuna vituo vichache vya kupimia

UKIMWI halafu viko mbali kwa hiyo havifiki. Nashauri Serikali ijitahidi kuongeza vituo vyatupu kupimia UKIMWI. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna tatizo la *viral load mashine*, nashauri Serikali ijpange *at least* kila mkoa uwe na *viral load mashine* kwa sababu unakuta vipimo vite vinapelekwa mbali njiani vinakutana na shida kadha wa kadha tunawenza tusipate *really* matokeo kwa sababu ya ule ubebaji labda unatoka Njombe kwenda Mbeya au utoke sehemu moja na kupeleka sehemu nyingine ambayo ni mbali. Sehemu fulani Serikali imesema imejitahidi kununua dawa na kujenga vituo basi ijitahidi kuongeza na hizo *viral load mashine*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuongelea suala la kodi ya mapato. Ni kweli Watanzania wanaishi kwenye wakati mgumu sana kwa sababu ukienda ofisi za Kodi ya Mapato unaweza ukashinda siku nzima unahangaikia kitu kimoja. Haijulikani kama wafanyakazi ni wachache au ndiyo *system ilivyo?* I ile hali ambayo inaonekana katika Ofisi za Kodi ya Mapato inasababisha watu wengine kukata tama. Kama Serikali ina nia ya kukusanya mapato iongeze watendaji ili kurahisisha kazi. Ni mara nyingi sana mimi nimefika pale nimekuta watu wanagongana tu kwenye *corridor*, kila sehemu kumejaa. Sasa watu hawa wanatuletea pesa na wao wanaisaidia Serikali kukusanya mapato, kama watendaji ni wachache ina maana wanahangaika siku nzima na wanapoteza muda wa kufanya kazi zingine na Serikali inakosa mapato. (*Makof*)

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili ilishagonga Mheshimiwa, ahsante sana. (*Makof*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Hamida Mohamed atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati, kama watakuwa hawajamaliza muda wao tutamalizia na Mheshimiwa Anna Lupembe.

**MHE. HAMIDA M. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hotuba ambayo iko mbele yetu. Nianze kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa uwasilishaji wa taarifa yake ya utekelezaji kwa kipindi hiki cha 2019/2020, hotuba ambayo imesheheni mambo mbalimbali ambayo yametekelawa lakini na mwelekeo wa Serikali katika kukuza uchumi wetu na katika kutekeleza Mpango wa Miaka Mitano ambao tutaumalizia mwaka kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa namna ambavyo anajitoa na namna ambavyo anatumikia Serikali hii lakini kwa namna ambavyo anawajali wananchi wake wa Wilaya ya Ruangwa kule Jimboni kwake. Pamoja na kwamba ana majukumu makubwa ya kitaifa lakini anapopata fursa hata ya siku moja, mbili anakimbia na kwenda kuungana na wananchi wake katika Jimbo lake la Ruangwa. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Makamu wake wa Rais kwa namna ambavyo wanasimamia utekelezaji wa miradi mikubwa na kuona ni namna gani wanaendelea kukuza fursa za uchumi katika nchi yetu lakini kuendelea kukuza uwekezaji kwa kutekeleza hii miradi mikubwa. Tumeona namna ambavyo ujenzi na upanuzi wa barabara pamoja na madaraja makubwa ambayo yanajengwa katika kuhakikisha kwamba Watanzania tunasafiri bila matatizo yoyote kutoka mkoa mmoja kwenda mkoa mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wetu wa Lindi tumebahati kipindi kilichopita tulitenga fedha kwa ajili ya kujenga barabara inayotoka Nanganga – Luchelegwa – Nachingwea - Masasi. Wananchi wa Wilaya hizi tumefarijika sana kuona kwamba tulitengewa fedha. Mpaka sasa ujenzi hauaanza napenda kujua wamekwama wapi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona kwamba Serikali imeendelea na ujenzi wa reli ya *Standard Gauge* ambayo

inaendelea vizuri. Kwa speed inayokwenda nayo nina hakika kabla hatujamaliza Bunge hili na sisi tutakuwa tumeshuhudia namna ambavyo reli hizi za kisasa zinafanya kazí katika nchi yetu. (*Makofí*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona pia upanuzi wa bandari ya Dar es Salaam kule Tanga na Mtwara. Upanuzi huu wa bandari umetoa fursa kubwa kwa wananchi wa Mikoa hii ya Kusini kwa sababu sasa nafasi za ajira kwa vijana wetu zinaongezeka kwa kutumia bandari ya Mtwara. Si hivyo tu hata wafanyabiashara wanaouza mafuta sasa wanapata urahisi wa kupokea mafuta kutoka Mkao huu wa Mtwara kwa sababu ya upanuzi wa bandari ile ya Mtwara. (*Makofí*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuishukuru pia Serikali imeendelea kuboresha kwa kujenga vituo vyá afya na hospitali na kuboresha zahanati katika maeneo mbalimbali. Sisi katika Mkao wa Lindi tumebahatika katika Majimbo yote tumepata vituo viwili viwili katika kila Jimbo na viko kwenye hatua nzuri sana na vingine viko tayari kwa ajili ya ufunguzi. Nachoiomba Serikali kufanya maandalizi sasa ya watumishi pindi vituo hivi vyá afya vitakapokamilika basi tuwe na watumishi wa kutosha wa kusimamia vituo vyetu vyá afya ili kuendelea kuboresha afya kwa wananchi wa Mkao wa Lindi. (*Makofí*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kwa kuongeza uzalishaji wa umeme kuititia mradi wetu wa *Stigler's Gorge*. Nimebahatika kutembelea eneo la mradi wa huu, kwa fedha iliyotoka kwa hakika mradi unekwenda vizuri sana. Naomba Mheshimiwa Rais wetu asirudi nyuma katika kuhakikisha kwamba mradi huu unafanikiwa na hatimaye tuweze kuwa na umeme wa kutosha kwa sababu uwekezaji unategemea sana uwepo wa umeme katika nchi yetu. Kwa hiyo, umeme huu utakuwa ni mkombozi mkubwa sana na uwekezaji utakuwa ni mkubwa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii pia kuipongeza Serikali, kumpongeza Mheshimiwa Rais wetu kwa ujasiri ambao ameujonesha katika ununuzi wa ndege, maana

sasa tunapata heshima kubwa katika nchi yetu kumiliki ndege zetu wenyewe. Hilo ni jambo la faraja sana, ni jambo jema katika kukuza uchumi na kuendelea kuimarisha uwekezaji katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie katika Mkoa wetu wa Lindi. Katika Mkoa wetu wa Lindi sasa tumefungua fursa za uwekezaji. Kwa hiyo, ninaomba sana ushirikiano na Serikali kuhakikisha kwamba eneo hili la uwekezaji katika Mkoa wetu wa Lindi tunafanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo mbalimbali kwa kila Wilaya, kuna fursa mbalimbali za uwekezaji, nami nitumie nafasi hii kuwaalika Waheshimiwa Wabunge mbalimbali, karibuni kwetu Lindi, mje kujiona, yawezekana nanyi mkabahatika au mkapenda kuja kuwekeza katika maeneo mbalimbali ilimradi katika Mkoa wetu wa Lindi tuendelee kukuza uchumi wetu, lakini tuweze kutengeneza ajira mbalimbali. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Mkoa wetu wa Lindi tuna viwanda vidogo vidogo na nina hakika kwa nafasi hii tumekuwa tukiongoza kwa kuwa na viwanda vingi vidogo vidogo vinavyofikia karibu 400 na zaidi. Viwanda hivi vyenye ajira kuanzia mtu mmoja, wawili, watatu; kwa hiyo, *SIDO* Lindi wamefanya kazi nzuri maana viwanda hivi vimetokana na mafunzo ambayo *SIDO* wameweza kuyasimamia katika kuhakikisha wananchi wa Mkoa wa Lindi wanaweza kupata ajira kwa kujajiri wenyewe. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaiomba sana Serikali kuhakikisha kwamba tuendelee kuwasaidia *SIDO* Lindi ili waendelee kufanya kazi zao za kuendelea kutoa mafunzo mbalimbali katika maeneo mbalimbali kuhakikisha kwamba wananchi wa Lindi wanaendelea kuingia katika eneo hili la viwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali katika kukuza utalii katika Mkoa wa Lindi kwamba tunao mji mkongwe wa Kilwa, mji ambao ulianza kutumia sarafu yake

wenyewe katika eneo hili la Afrika Mashariki. Kwa hiyo, yako mambo mbalimbali ambayo tukiyasimamia yanaweza yakatuletea fedha nydingi za kigeni na kuwavutia watu mbalimbali kuja kutembelea katika eneo hili la Kilwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunatambua kwamba Vita vya Maji Maji vilianzia pale Kilwa katika Kata ya Kipatimu. Eneo lile lina historia yake kwa sababu, ndugu zetu Wakoloni walikuwa wanashangaa namna ambavyo Kinjikitile Ngwale aliweza kutengeneza jambo ambalo lilitanya Wakoloni watupige risasi za moto maana yake zinabadilika na kuwa maji. Kwa hiyo, ni historia kubwa sana. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna kila namna ya kuukuza utalii katika eneo hili, kwa sababu ndugu zetu Wakoloni waliweza kukata kichwa cha Kinjikitile Ngwale na kupeleka kwao kwenda kuchunguza kwamba mtu huyu, utaalamu huu amewezaje kubadilisha risasi ya moto na kuwa maji? (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tuna kila namna ya kukuza utalii katika eneo hili. Maana ya...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Muda wako umekwisha. Ahsante sana.

**MHE. MAIDA H. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

**NAIBU SPIKA:** Asante sana. Mheshimiwa Ritta Kabati, kama muda utakuwa unaturuhusu, Mheshimiwa Anna Lupembe atamalizia.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia bajeti ili yoko mezani kwetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa nianze na kuipongeza Serikali hii ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais wetu, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa sana ambayo amefanya kwa kweli katika nchi yetu na hata imefanya baadhi ya viongozi wetu akiwepo Mheshimiwa Lowassa kurudi CCM, baadhi ya Wabunge wengine wote kurudi CCM na viongozi mbalimbali baada ya kuona kazi nzuri sana na mno inayofanywa na Chama chetu cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi yake nzuri. Kwa kweli, amefanya kazi nzuri sana, ametembea karibu nchi nzima kuhakikisha kwamba miradi inakwenda. Pia nawapongeza Mawaziri waliopo katika Ofisi ya Waziri Mkuu; Mheshimiwa Jenista Mhagama, Mheshimiwa Ikupa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kazi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa kumteua Mheshimiwa Angellah Kairuki kwa kuongeza tena kasi katika ofisi yake kwenye suala la uwekezaji. Ninaamini kabisa uwekezaji sasa unaenda kuinua nchi yetu. Bila kuwekeza, sidhani kama nchi yetu itaweza kusikika hata katika viwanda au katika nyanja zozote. Bila kuwekeza, kuleta wawekezaji, kuweka vivutio vingi na kutoa changamoto nyingi ambazo kwa kweli tulikuwa tunaona kama ni kero sana katika nchi yetu, nchi hii haiwezi kuendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nashauri kwamba Mheshimiwa Jenista sasa apewe wataalam na ofisi ambayo itasaidia sasa kuondoa ule urasimu ambaao ulikuwepo kwa wawekezaji wetu ili waweze sasa kuwekeza na nchi yetu iweze kuongeza ajira na kipato kikubwa kabisa katika nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba nipongeze sana mambo makubwa yanayofanyika katika Mkoa wetu wa Iringa. Ukarabati wa Kiwanja cha Nduli, kwa kweli Wana-Iringa tunasema Kamwene. Kazi ile ni nzuri sana na mpaka

sasa hivi ukarabati ule tarehe 29 nawakaribisha wote, ndege kubwa *Bombadier* inatua pale Iringa. Kwa hiyo, niwaombe muionje siku hiyo, twende tukatue pale hata Naibu Spika ili mwone kazi na kasi kubwa kabisa inayofanywa na nchi yetu ikiongozwa na Chama cha Mapinduzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu, Iringa ni kitovu cha utalii, sasa ukarabati ule uende sambamba na ukarabati wa kiwango cha lami, ile barabara inayokwenda mbuga za wanyama *Ruaha National Park* kwa sababu, ni mbuga ya pili. Tunaamini kama itajengwa kwa kiwango cha lami, sasa utalii utaongezeka, uchumi wetu wa Iringa na uchumi wa nchi hii kutumia utalii tutaongeza hata watalii wengi sana watakuja, hata wananchi watajajiri kwa kupitia utalii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naiomba Serikali yangu, wale wananchi walipisha ukarabati ule, basi wapewe fidia zao mapema kabisa. Vilevile uzio ujengwe kwa sababu kuna wanyama wanazunguka, ili kuhakikisha kwamba mambo ni motomoto Iringa. Iringa siyo ile ya wakati ule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nizungumzie kuhusu utafiti. Kwa kweli nchi hii haitaendelea bila kufanya tafiti mbalimbali, kwa sababu, tunavyo vituo vingi sana vya utafiti; *TARIRI*, *COSTECH*, *NIMRI* na *NBC*. Hivi vituo vina hali mbaya mno. Sasa tutaendeleaje?

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda, bila kuboresha mambo ya utafiti, bila kutenga pesa ya utafiki katika hivi vituo ili tafiti mbalimbali katika nchi hii ziweze kufanyika, hatutakwenda. Nchi za wenzetu zinaendelea kwa sababu wanafanya tafiti za kutosha. Tunaona tunapata pesa za kigeni, lakini wao wanalenga tunataka kufanya tafiti tulani. Nchi yetu bado hatujajipanga kuweka pesa ya kutosha kwenye utafiti. Unaona karibu 90% inaenda kwenye ya mbegu. Asilimia 90 tunaagiza mbegu kutoka nje wakati tunacho Kituo cha Utafiti cha Mbegu nzuri,

nasi tumekwenda, wanashindwa tu kupata pesa. Kuna changamoto kubwa sana kwenye vituo hivi vya tafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali yetu kwa kweli sasa ione umuhimu mkubwa kabisa wa kuhakikisha tunatenga fedha za utafiti. Kwa tulishasema katika Mpango wa Maendeleo kwamba 1% ya bajeti tutenge kwa ajili ya tafiti mbalimbali hapa nchini. Kwa hiyo, naomba hii iwe ni lazima itengwe ili tufanye utafiti wa kutosha ili uchumi wa viwanda uende vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nielezee kitu kingine kuhusu barabara zetu za kiuchumi. Barabara za kiuchumi kwa kweli naomba zipatiwe kipaumbele cha kutosha. Kwa sababu barabara nyingi sana za Mkoa wetu wa Iringa ambazo ndiyo uchumi mkubwa; na nafikiri tunaenda kwenye viwanda na kule ndiyo kuna malighafi za kutosha, bado sasa hivi hazipitiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu mfano mmoja, kwa sababu najua nitakuja kuchangia kwenye mambo ya barabara; utakuta pale Mufindi kuna Barabara ile ya Mtirili – Ifwagi – Mdabulo – Ihanu – Mpanga TAZARA mpaka Mlimba huko kwenda kule kwa Mheshimiwa Susan Kiwanga. Hii barabara ni muhimu sana, lakini hapa ninapozungumza sasa hivi ile barabara haipitiki kabisa. Malori yamekwama, wananchi hawafanyi shughuli zozote. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ziko barabara nyingi sana za Iringa ambazo kwa kweli ni za kiuchumi kabisa ambazo hazipitiki. Naomba hizi ziangaliwe na ikiwezekana tuzijenge kwa kiwango ambacho magari yaweze kupita yasilale barabarani, maana uchumi ndiyo unazidi kuharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu kingine ambacho nilitaka kuzungumzia pia kuhusiana na tozo katika viwanda vyetu, Mheshimiwa hizi tozo zimekuwa nyingi. Tumekuwa tukiuliza sana maswali hapa Bungeni, tozo zimekuwa nyingi mpaka wakati mwingine zinafika hata 28 kwenye viwanda vyetu. Sasa tunaelekea kwenye uchumi wa viwanda, lakini

viwanda vinakufa kabla hata havijaanza kwa sababu, watu wakifkiria tozo nyingi sana karibu 28. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika usindikaji wa maziwa, nakipongeza sana kiwanda chetu cha ASAS pale Iringa, kinafanya kazi nzuri, kimetoa ajira nyingi sana, lakini tozo zimekuwa shida. Unakuta kwamba hata zile *flavour* za maziwa kila *flavourinalipiwa*. Sasa ifike sehemu jamani Serikali iangalie. Kwanza tusaidie viwanda vyetu vikue, kwa sababu viwanda vikukua, tukipata ajira nyingi, pato litaongezeka kwa kiasi kikubwa na hapo ndiyo tutakuta kweli kazi inakwenda vizuri zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi tulikuwa tumeenda kwenye ziara, kwa kweli wamempongeza sana Mheshimiwa Rais. Ziara yetu ya Kamati ya Kilimo, Mifugo na Maji, tumepata pongezi nyingi sana kwa wananchi, lakini kuna changamoto ambazo zipo kwa mfano kwenye miradi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta katika miradi ya maji kwanza vibali vya kutoa vile vifaa kwa ajili ya kufanya kazi havitoki kwa wakati. Kwa mfano, tulienda kwenye mradi ule wa maji Arusha. Ule mradi tayari maji yameshatobolewa pale Moshi, lakini sasa ili waanze kufanya ile kazi, bado hawajapewa vibali. Mizigo iko bandarini imekaa karibu wanasema kwamba ni miezi mitatu sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi, hii miradi ni ya kwetu, Serikali ya kwetu, hebu wekeni mpango mzuri kuhakikisha kwamba vitu vikija kwa mfano labda hawa wenzetu ambao wamekata huu ukandarasi, basi vifaa vyao vitolewe haraka sana bandarini ili iweze kusaidia miradi iende kwa haraka ili gharama za kutengeneza hii miradi ziwe kwa kiasi cha chini. Tunapochelewesha hii miradi kwa ajili tu ya kuchelewesha vifaa bandarini sidhani kama inaleta picha nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, walisema pia vibali vya kazi vya wataalamu wao vinachelewa kutoka. Kwa hiyo, hilo nalo liangaliwe kwa haraka zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile nisisahau, sisi ni walemavu watarajiwa. Nizungumzie watu wenye ulemavu. Mheshimiwa Ikupa nakupongeza sana, umefanya kazi nzuri sana, mpaka Iringa umefika, lakini kwa kweli kuna tatizo ambalo liko. Watoto wenye ulemavu wanapoenda kwenye hizi shule, zamani walikuwa wanapatiwa nauli. Sasa matokeo yake watoto wanabaki kwenye mashule hawarudi kwa wazazi wao. Wazazi wao wengi hawana uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali iweke utaratibu wa kuwasaidia hawa watoto wenye ulemavu ili mara wanapofunga shule, basi warudi kwa wazazi wao. Hili ni tatizo kubwa, naomba Serikali iliangalie kwa umuhimu wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze *Kamal Steel*, kwa kweli, namshukuru Mheshimiwa Ikupa, alitualika tukaenda kwenye kiwanda cha Kamal. Amekuwa akisaidia sana, ameweka kiwanda kwa ajili ya kutengeneza viungo. Kama watu hawafahamu hapa, basi Kamal anafanya hiyo kazi na kwa kweli, ametoa viungo vingi sana vya bandia; na hata Mkoa wangu wa Iringa wameguswa, kwa sababu, pale tuna karibu watu wanaohitaji kama 100. Kwa hiyo, ameshatoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru pia Mengi naye ametoa mchango, amewapatia mtaji watu wenye ulemavu waliopatiwa na Kamal shilingi laki mbili, mbili. Kwa hiyo, *Mr. Mengi* pia tunamshukuru kwa kuwasaidia watu wenye ulemavu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli, naomba pia nikupongeze, lakini niipongeze Tanzania yetu kwa michezo. Sasa hivi tuko mbali sana kimichezo na tupongeze hili kombe la *AFCON* kwamba angalau na sisi sasa tuko juu sana kimichezo. Tuendelee kusaidiana, tuendelee kushirikiana na kuhakikisha kwamba nchi yetu inapiga hatua kubwa kabisa katika michezo.

Mheshimiwa Spika, nina imani kabisa nchi hii tutaanza kutengeneza vipaji kwa watoto wetu, tutapata nchi ambayo itakuwa inatangazika kimichezo. Nafikiri kimichezo tunaweza...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa kengele ya pili imeshagonga. Naamini hutakosa kwenye mchango wa kuwachangia Yanga, maana umesisitiza watu tuchangie timu. Kwa hiyo, utaenda kuchangia Yanga. (*Kicheko*)

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo. Yanga unajua rangi zake ndiyo zitanifanya na mimi pia nichangie, lakini...

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. (*Makofi/ Kicheko*)

Mheshimiwa Anna Lupembe, nikupe uhuru kama unawenza kuchangia kwa muda uliobaki nikuruhusu. Kama utataka kuchangia baadaye, pia ni sawa.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie mchana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa.

Waheshimiwa Wabunge, sasa nitaita majina ya Wabunge tutakaoanzanao mchana kuchangia, haimaanishi watakaoitwa kwanza ndio watakaokuwa wa kwanza. Tunao kwenye orodha Mheshimiwa Anna Lupembe, Mheshimiwa Devotha Ninja, Mheshimiwa Sebastian Kapufi, Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhil, Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Maulid Mtulia, Mheshimiwa Marwa Rioba Chacha, Mheshimiwa Rashid Shangazi na Mheshimiwa Zubeir Kuchauka. Hawa ndio tutakaoanzanao mchana, majina mengine tutaendelea kuwataja kwa kadiri tutakavyokuwa tukiendelea.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa Wabunge nasitisha shughuli za Bunge mpaka Saa 11.00 jioni, leo.

*(Saa 6.56 Mchana Bunge lilsitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

Tunaendelea na majadiliano, tutaanza na Mheshimiwa Anna Lupembe, atafuatiwa na Mheshimiwa Devotha Ninja, Mheshimiwa Sebastian Kapufi ajiandae.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, naomba nikushukuru kwa kunipa nafasi hii. Vilevile nimshukuru sana Mungu kwa kibali alichotupa katika Bunge hilli la Bajeti, tunamwomba aendelee kutulinda na kututunza katika Bunge mpaka tumalize.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya katika kusimamia na kuhimiza maendeleo ndani ya nchi yetu. Vilevile naomba nimpongeze Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ambayo anaifanya katika ziara ya nchi yetu kwa ajili ya kuangalia juhudhi na maarifa ya Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Waziri, Mheshimiwa Jenista Mhagama pamoja na wasaidizi wake, Mheshimiwa Mavunde pamoja na Mheshimiwa Ikupa kwa kazi kubwa wanayoifanya. Tumeona jinsi gani Mheshimiwa Ikupa anavyokwenda kufanya kazi katika mikoa, kuangalia jitihada za wale mavu. Nataka nimkumbushe tu Mheshimiwa Ikupa, ametembea katika mikoa mingi, naomba basi Katavi nako wanamsubiri aje kuongea na wale mavu wa Mkoa wetu wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naipongeza Serikali kwa kutuletea Mkoa wa Katavi bilioni moja kwa ajili ya uanzishwaji

wa Hospitali ya Mkoa, tunashukuru sana na vilevile mmetuletea fedha kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkoa pamoja na nyumba ya Mkuu wa Mkoa. Nilizungumzia bajeti ya mwaka jana, lakini utekelezaji umeshafanyika, naomba niipongeze sana Serikali kwa sababu inafanya kazi kwa vitendo. Naomba tuwashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkoa wetu sisi una uhaba mkubwa sana wa watumishi, hususan kwenye Halmashauri zetu pamoja na ndani ya ofisi za mkoa. Ndani ya mkoa wetu kuna takriban ya wafanyakazi elfu sita mia saba na kitu. Ina maana kuwa tunatakiwa tuwe na wafanyakazi elfu sita na kitu, lakini ndani ya mkoa wetu kupitia Halmashauri zote tuna wafanyakazi takriban elfu nne na upungufu wetu kama elfu mbili hivi, kwenye sekta ya afya, kilimo pamoja na elimu. Nategemea Serikali yangu sikivu, hivyo itatuongezea *staff* kwa sababu mkoa wetu una uhaba sana wa wafanyakazi, tunaomba wasitusahau kwa ajili ya utendaji kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndani ya mkoa wetu sisi na sasa hivi ni sera ya viwanda, hatuna umeme wa uhakika sana, tunaomba Serikali itusaidie kutuletea umeme wa *grid* ya Taifa ili wananchi wa Katavi waweze kujenga viwanda kwa sababu sera yetu ni ya viwanda. Tunaombasana kwa sababu umeme wetu si wa uhakika kabisa, tunaomba *grid* ya Taifa iweze kutufikia katika Mkoa wetu wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wetu wa Katavi, ma-*DC* wetu toka wateuliwe, hawajawahi kupata magari mapya na ukizingatia jiografia ya Mkoa wa Katavi ni ngumu sana, wanabahatisha tu magari, wanachukua magari ya watendaji ndio wanafanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunashukuru kwa kuwakumbuka kuwajengea nyumba na wameshawalettea fedha kwa ajili ya nyumba za Wakuu wetu wa Wilaya, lakini vitende kazi, ukianzia mkoani mpaka hata Mkuu wa Mkoa mwenyewe, gari hana, kwa sababu gari lake liliipata ajali, mpaka leo anatumia tu magari ya kubahatishabahatisha.

Sasa niaomba Serikali yangu iangalie sanaMkoa wa Katavi, upande wa ma *DC* wetu, wanafanya kazi kubwa sana ya kuhamasisha maendeleo ndani ya mkoa wetu na kusimamia maendeleo ndani ya mkoa wetu, lakini vitendeakazi hawana na Halmashauri zetu hazina magari kabisa mpaka mkoa. Naomba Serikali yangu sikiu iangalie Mkoa waKatavi kwa ajili ya vitendea kazi ili waweze kuendelea kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuja sasa kwenye mambo yetu ya uchumi, naomba niishauri Serikali yangu, najua Wabunge wengi wamesema, wamezungumzia kuhusu masuala ya uvuvi, najua zamani ndani ya Wizara yetu ya Uvuvu, tulikuwa tuna Shirika lilikuwa linaitwa *TAFIRI*, lilikuwalinavua samaki na samaki wale walikuwa wanawasaidia sana Watanzania kwa kuwapata kwa bei nafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile naomba niipongeze Wizara ya Mifugo, pamoja na Uvubi kwa kuweka Dawati la Sekta Binafsi kuititia Uvubi, wamefanya vizuri sana. Naomba nimpongeze sana Waziri, Mheshimiwa Mpina pamoja na Naibu wake ninajua dawati hili linafanya kazi vizuri sana na usimamizi unaendelea kuwa mzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika,naomba niikumbushe Serikali yangu, naomba sana, tununue meli yetu. Kazi aliyofanya Mheshimiwa Mpina na Naibu Waziri wamefanya kazi kubwa, sasa hivi samaki kwenye maziwa ni wakubwa kwelikweli. Tulienda Mwanza, wenyewe tulishuhudia jinsi gani kazi imefanyika, mpaka samaki wakubwa wapo katika maziwa yetu.

Sasa tukinunua meli kuititia bahari, meli ikafanya kazi hiyo ya kuvua kwenye maziwa, nafikiri Tanzania yetu itapata uchumi mkubwa, Taifa litafaidika na vilevile wananchi wetu watafaidika kuititia uvuvi. Ukizingatia sasa hivi wenzetu Uganda na Kenyawamefungua viwanda vingi sana kwa ajili ya kuchakata samaki, sisi ndani ya Tanzania kuititia Mkoa wetu wa Mwanza tuna viwanda vichache sana kwa ajili ya uchakataji wa samaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niipongeze Serikali kwa kazi kubwa kwa upande wa mifugo, tumejenga sana viwanda na tumeshuhudia, Longido tumeona kiwanda kikubwa cha machinjio kwa ajili ya kusindika mifugo yetu.Hata hivyo,ng'ombe wengi wanasafirishwa kupelekwa Kenya.

Naomba, kwa sababu na sisi Tanzania tunataka kusindika mifugo yetu, tupunguze tozo. Tumekuta pale tozo ni kubwa sana kwa upande wetu wa Tanzania, naiomba sana Serikali yetu sikivu ili tuweze kufaidika na usindikaji wa mifugo yetu, basi ninaomba tupunguze tozo ili wale Watanzania wa Longido waweze kuuza mazao yao ndani ya nchi yetu sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile, sasa hivi naipongeza Wizara hii, inafanya kazi vizuri, sasa hivi ngozi. Sisi tunesema sera ya viwanda, ngozi nydingi zinasafirishwa nje ya nchi na sisi tunazitaka hizo ngozi zibaki Tanzania. Naomba sana ngozi hizi zibaki katika nchi yetu kwa sababu ni sera yetu ya viwanda, viatu vitengenezwe hapahapa ili uchumi wa Tanzania uweze kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile ninakuja kwenye sekta ya maziwa, naomba kuipongeza Serikali, sekta ya maziwa inakuana inatuletea kipato kikubwa ndani ya nchi yetu, tumeona, sisi wenyewe tumefanya ziara, kuna viwanda vya maziwa ambavyo vinafanyakazi vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupita huko, tumekuta matatizo machache, kwa sababu ndani ya maeneo yetu...

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari!

**MBUNGE FULANI:** Tayari, unga mkono.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:**Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sanana naomba kuunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Devotha Minja atafuatiwa na Mheshimiwa Sebastian Kapufi na Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhil, ajiandae.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii ya kuchangia hotuba hii ya Waziri Mkuu. Nimepitia vizuri kitabu hiki cha Waziri Mkuu hasa katika ukurasa wa tisa ambapo amezungumzia mafanikio ya miradi ambayo imefnywa na Serikali hii ya Awamu ya Tano. Moja ya mafanikio aliyoazungumza ni kuhusu ujenzi wa *Standard Gauge* unaendelea hivi sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatupingani kabisa na mradi huu, tunachokizungumza ni kuhusuproper planning za mradi huu. Ili nchi yoyote iendelee lazima iwe na mikakati endelevu, nchi za uarabuni ambazo zina mafuta, ukiwaliza hata kesho yao baada ya mafuta kwisha, wanafahamu. Kwa sababu wanaingia gharama ku-implement teknolojia ambazo zinabaki kwa wazawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, leotunafanya *Standard Gauge*, asilimia 20 ya *labour skills* ni Watanzania, asilimia 80 ni Waturuki. Tunasema kwamba mradi huu unatoa ajira kwa Watanzania kwa kiwango kikubwa, labda watuambie Watanzania wataishia kufanya zile kazi ndogondogo za mamantilie na zinginezo, asilimia 80 ya teknolojia kubwa zinafanywa na Waturuki. Kwa hiyo, tunachosema sisi, tuwe na miradi ambayo ina proper planning, tuandae watu wetu kwanza kuingia katika hiyo teknolojia, tupate watu professionals ambao sasa kwa asilimia 90 watakuwa...

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Devotha Minja kuna taarifa.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. INNOCENT L. BASHUNGWA):** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpe taarifadada yangu Mheshimiwa Devotha Minja kwamba, akizungumzia mambo ya ajira wakati wa ujenzi wa SGR, ni

*very short term* yaani kama kuzungumza leo na wakati ule mradi ni wa miaka nenda rudi. Kwa hiyo, azungumzie labda *impact* ambayo nchi itapata kupitia mradi huu, badala ya kuzungumzia vitu vya leo wakati ule ni mradi wa muda mrefu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Devotha Ninja unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ana muda baadaye anaweza akajibu kama Naibu Waziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachokisema, tulitegemea, neema ambayo aliisema Rais, kwamba ajira zitabaki kwa Watanzania, asilimia zaidi ya 90 kazi hizi zifanywe na Watanzania, lakini sasa zinafanywa asilimia 20 ambaao ni Watanzania. Hoja yangu ni kwamba, tulitakiwa tuijlandae kabla ya kuingia kwenye mradi huu, kwa maana kuwaandaa watu ambaao wana uwezo wa kufanya hizi kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la mataruma, mataruma hivi sasa ya reli yanatoka China. Hivi tulikuwa na sababu gani ya kukimbiliakuanza mradi huu, badala ya kufufua miradi ya Mchuchuma na Liganga, tukapata mataruma, yakatusaidia, tukaweza kupunguza gharama ya fedha nyngi ambayo sasa hivi inakwenda China badala ya kubaki hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza miradi hii, inaleta maswali kwa wananchi. *SGR*, unazungumzia bilioni 16, kwa wananchi wa kawaida tu, ukiwaliza kipaumbele ni nini sasa hivi watakwambia tunataka huduma za afya, ni suala la kisera kwamba, kila kata iwe na kituo cha afya. Katika vituo vya afyakata 4,420, kuna vituo vya afya 513 na katika hivyo 513, vituo 115 ni vya *private*.

Kwa hiyo, kwa mwananchi wa kawaida ukimwambia unapeleka bilioni 16 kwenye *SGR*, ambapo hana huduma yoyote ya afya, wananchi wa kawaida hawatuelewi.

Mheshimiwa Naibu Spika,tunasema yote ni mipango, lakini lazima tuangalie *basic needs* kwa wananchi. Kuna maeneo hivi sasa yanapata maji kwa asilimia tatu, lakini ukimwambia mtu habari za *SGR* hakuelewi, anataka maji, anataka huduma zaafya. Kwa hiyo, tunasema *niproper planning* Tanzania kuangalia *priorities* za nchi na kwa wananchi wake.

Mheshimiwa Naibu Spika,Mheshimiwa Waziri Mkuu amesema kuhusu mradi wa kufua umeme wa *Stiegler's*sambao utagharimu takriban trioni 6.5. Tulikuwa na mradi wa Kidunda, ambao ulikuwa una uwezo wa kuzalisha *megawatts* 20 za umeme, ulikuwa na uwezo wa kuzalisha maji yatakayotumika kwa wakazi wa Dar es Salaam kwa ajili ya viwanda, kwa ajili ya mashamba ya umwagiliaji, lakini hivi sasa tumeacha huku, tunakimbilia kwenye *Stiegler's*. Kwa hiyo, ni wakati ambao tunataka kusema ni kwanini Serikali inakuwa na miradi mingi halafu *implementation*yake, mingine inaachwa, mingine inapewa kipaumbele!

Mheshimiwa Naibu Spika,kama suala ni umeme, tunganeza na Kidunda, watu walishalipwa fidia, ndipo twende kwenye *Stiegler's*, tuangalie kwamba tuna upungufu wa umeme kiasi gani, ndipo tunganeza mradi huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo ambayo tukijiuliza, umeme wa maji siyo *reliable*siku hizi, kwa nchi nydingi sasa hivi kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Tungeweza tukafikiria zaidi hata kuwa na umeme, sisi tuko chini ya *equator*, kuwa na umeme wa juu, umeme wa upepo na kadhalika, badala ya hivi sasa nguvu zote, Kidunda wananchi wamelipwa, wameachwa kama walivyo, sasa hivi nguvu za Serikali zinaenda kwenye *Stiegler's*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimemsikiliza Waziri Mkuu pia amesema suala la ununuzi wa ndege. Ndege nne *Bombardier*zimegharimu zaidi ya bilioni 280, lakini hivi karibuni tumeambiwa, *maintenance* ya ndege hizi zimetumika zaidi ya bilioni 14, hivi tunatengeneza faida? Hivi ni biashara kwenye ndege! *Airbus* moja ambayo ni takribani

bilioni 200 iliyokuja juzi, tunajuliza iko wapi! Tuliambiwa italeta watalii kutoka Marekani, kutoka Uingereza kutoka wapi, hivikwa nini hatuioni ikifanya shughuli hizo, kwa nini hatuioni sasa hivi ikifanya shughuli hizo?

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba Waziri atakapokuja kujibu atueleze iko wapi hiyo ndege. Kwa sababu ukisoma kwenye mitandao unaambiwa mara imeuzwa Kenya, mara iko kwenye matengenezo, mara iko *garage*, mara inapakwa rangi. Ndege iliyokuja juzi, shughuli zote za nchi zikasimama kwa sababu ya ndege moja, ambayo imekuja nchini. Leo hatuelewi kwamba huo uzalishaji wa ndege hii mpaka sasa umeingiza faida kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo taarifakwenye mitandao, mara inaonekana inabeba nyama kutoka Mwanza, tunataka tuambiwe, kwa sababu zimenunuliwa na kodi za Watanzania, ziko wapi ndege hizi za kuleta watalii ziinue utalii wa nchi hii, inafanyakazi gani hivi sasa? Ndiyo ugomvi wetu, tunahitaji fedha za Serikali zitumike vizuri, badala ya kuleta ndege miezi mitatu toka Januari, *image-ground*, badala ya kwenda huko nje, ikafanya yale ambayo Serikali imesema, matokeo yake tunayasikia tu ya mitandao yanayoendelea. Kwa hiyo, watu wanataka kufahamu *specificni* kitu gani kinaendelea.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Devotha Ninja, unapokea taarifa hiyo.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ana muda wa kutosha kuja kujibu. Nilitegemea angeniambia *airbus* iko wapi sasa hivi ambayo Watanzania wanataka kujua. Sheria za kimataifa zinasema ili uende nchi kama Amsterdam na kwingineko kwenye mataifa yaliyoendelea lazima uwe na ndege tatu, kwa maana ya mbili ziwe angani na moja iwe *reserved*. Sasa ya kwetu tutaiweka *reserved* tukisubiri zingine zije ndipo zianze kuruka, tunasema ni kuilaza pesa chini. Nafikiri atakuwa na muda mzuri wa kunieleza. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwenye hali ya kisiasa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

## TAARIFA

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwakajoka, kengele ya pili imeshagonga nilikuwa nampa dakika yake moja ili aweze kumalizia sentensi. Kwa hiyo, naomba tumruhusu amalizie sentensi yake, Mheshimiwa Devotha Minja dakika moja.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Watanzania wanataka kujua kuhusu ndege yao kubwa iliyokuja ambayo ilifanya shughuli zote nchi nzima zikasimama, watu wakaenda kuipokea mpaka kwenye *runway* wamekaa wanashangilia, iko wapi ndege hiyo, inafanya nini, imeingiza nini toka imeingia hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nilikuwa najiuliza siku nikikutana naye Mheshimiwa Devotha Minja kwenye *bombardier* namna nitavyopiga *selfie*. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Sebastian Kapufi, atafuatiwa na Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili, Mheshimiwa Sabreena Sungura ajiandae.

**MHE. SEBASTIAN S. KAPUFU:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwanza, nianze kwa kuunga mkono hoja. Nimshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu na Mawaziri wote walioko katika ofisi hii, kitabu kimesheheni mambo mbalimbali na nitajikita katika maeneo machache, eneo la afya pia madini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, uhakika wa sera zisizoyumba, amani na utulivu, vitu hivi vikiwepo vinatengeneza ustawi wa uchumi. Kama hiyo haitoshi doplomasia ya kiuchumi ndiyo gari tunaloweza kusafiria na likatufikisha katika uchumi wa kati na uchumi wa viwanda. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kitabu cha hotuba ya Waziri Mkuu katika sekta za uzalishaji kwa maana ya ukurasa wa 27, eneo la utalii ambao ni ukurasa wa 32, eneo linalogusia uendelezaji wa utalii Ukanda wa Kusini kwa maana ya *REGROW* nimeona linazungumziwa suala zima la uendelezaji wa viwanja vya ndege, ni jambo jema na lenye afya. Kwa kuwa Mkoa wangu wa Katavi uko katika Ukanda huo wa Kusini tunao Uwanja mzuri wa Ndege wa Katavi, bila kuufanya uwanja ule ukafanya kazi habari hii ya kuendeleza ukanda ule kiutalii itakuwa pia hajakaa vizuri. Nendelea kumkumbusha Waziri Mkuu Uwanja wa Katavi, Uwanja wa Mpanda ni mzuri, ni changamoto katika kuibua suala la utalii katika ukanda ule. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaenda kwenye eneo la madini natamani kwanza nigusie masuala yanayogusa afya, kwa maana ya kitabu cha Waziri Mkuu tutaikuta ukurasa wa 56, 57, 58, najielekeza katika suala la hospitali. Nafarijika sana nikija katika eneo hilo kwa maana ya Hospitali ya Taifa ya Muhimbili, Hospitali ya Benjamin Mkapa na Hospitali ya Mloganzila.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo hili likitumika vizuri na kwa jinsi ambavyo nchi imejiwekeza kwenye kuimarisha sekta hiyo ya afya, tunakuja kwenye kitu kinachoitwa utalii wa tiba. Tukifanya vizuri, tukiendelea kuimarisha hospitali zetu hizo watu kutoka nchi za jirani iwe ni Malawi, Zambia au Kenya kama ambavyo Watanzania tumekuwa tukitoka hapa tukienda India, tutumie nafasi hii ya kuimarika kwa hospitali zetu kwenda kwenye eneo la utalii wa tiba. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa misingi hiyo siwezi nikashindwa kuzitaja hospitali zote za rufaa. Najua nchi kama

nchi imejipanga vizuri na nafahamu mara ya mwisho tuna zaidi ya hospitali zile 67 kwa maana ya Halmashauri mbalimbali lakini kuna hospitali mbalimbali za rufaa ambapo nchi imejipanga kwenda kuzijenga, hospitali hizo ni pamoja na Hospitali ya Mkoa wa Katavi. Rai yangu ni moja, kusema ahsante ni namna ya kuomba tena. Najua tumetengewa takribani shilingi bilioni 1 lakini kwa maana ya bajeti ya zaidi ya shilingi bilioni 9, naomba sana Serikali yangu siku uwezekano wowote wa kuona namna ya kupatikana kwa fedha ili badala ya kuwa na muda mrefu wa kujenga hospitali hizo tuwe na muda mfupi na tukamilishe zoezi hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikilisema hilo ninamaanisha nini? Niliwahi kusema katika Bunge lako hili Tukufu kwa sisi ambaao tuko Mikoa hiyo kama Katavi, kumtoa mgonjwa kutoka Katavi kumpeleka Bugando au Dar es Salaam umbali huu unaweza ukamalizwa kwa kuwa na hospitali ya rufaa pale pale Katavi. Ndiyo maana naendelea kusitiza ujenzi wa hospitali hizo za rufaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la madini na kama ilivyo ada mimi pia ni mchimbaji mdogomdogo wa madini, naomba hilo lifahamike mbele ya umma huu. Rai yangu katika eneo la madini, tumekuwa tukiongelea habari ya ajira. Nitoe ufanuzi mdogo, eneo la madini katika muda mfupi na ukizunguka nchi hii ukaangalia eneo la machimbo ya madini ndiko ambako ni maeneo yamekusanya watu wengi. Kukiwa na kitu wanaita *gold rush* kwa wakati mmoja usishangae kukuta una watu hata 5,000 na zaidi ya hapo. Kwa hiyo, unaweza ukaona jinsi ambavyo eneo la madini limesheheni watu wengi na linatoa nafasi kubwa ya ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafahamu kazi nzuri ambayo inafanywa na Rais wetu, najua tarehe 22 Janauri, 2019 alihamasisha na Wizara ikawakusanya wadau wa madini, kazi aliyoifanya Mheshimiwa Rais ni kazi nzuri. Rai yangu naitoa upande wa Wizara ya Madini, wakati tukiendelea kuboresha, unapomboresha mchimbaji mdogo

hatima yake atatoka hapo atakuwa mchimbaji wa kati na baadaye anaweza kuwa mchimbaji mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, tunapomlenga huyu mchimbaji mdogo hatutarajji abaki kuwa mchimbaji mdogo, kesho atakuwa. Sasa rai yangu ni nini? Kama nchi tuendelee kuandaa watu hawa kwa maana ya elimu. Leo wachimbaji wengi wadogo ikifika sehemu anatakiwa aingie ubia labda na watu wa kutoka nchi za nje, je, kama nchi tumewaandaa vipi watu hawa kwa maana ya elimu ya mikataba, tunafahamu vipi watu hawa katika maeneo ambayo wanayo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna kitu kinaitwa *reserve*, labda kwa kupitia *GST* wanaendeleaje kuwasaidia wachimbaji hawa wakajua hifadhi ya madini waliyonayo kwamba ile inaweza ikawa ni jambo jema la yeye kuingia mikataba? Anapoweza kuingia mkataba asilimia ambazo anaweza akazipata kutokana na eneo lake na hifadhi aliyonayo ya madini pale ni silaha tosha au ni ngao tosha ya kumpa kibali cha kuingia mkataba. Kama watu hawafahamu elimu ya mikataba, wanaishia kudhulumiwa. Naomba elimu hiyo ya mikataba iendelee kutolewa kwa wachimbaji wetu mbalimbali.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umeisha Mheshimiwa, ahsante sana.

Tunaendelea na Mheshimiwa Nuru Awadh Bafadhili atafuatiwa na Mheshimiwa Sabreena Sungura, Mheshimiwa Maulid Mtulia ajiandae.

**MHE. NURU A. BAFADHILI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Kwanza, nimshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili Tukufu na kuweza kuchangia. Vilevile nikushukuru wewe kwa kuweza kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita kuzungumzia afya na hali ya kisiasa. Kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa kujali afya za wananchi wake. Serikali imejitalidi imeweza kujenga zahanati, vituo vya afya na hospitali katika kila mkoa. Cha kusikitisha katika Jiji la Tanga, Kata ya Mianjani, wao wamejengewa zahanati na imemalizika toka mwaka jana lakini mpaka leo haijafunguliwa. Matokeo yake vibaka wanaingia kwenye zahanati ile wanaiba madirisha, milango na taa. Bahati nzuri Mwenyekiti wa Mtaa ametafuta walinzi na anawalipa ili kulinda ile zahanati. Kwa hiyo, naiomba Serikali ihakikishe kuwa zahanati hii inafunguliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kila siku nikisimama hapa nazungumzia kuhusu hospitali yangu ya Bombo. Hospitali ya Bombo ipo katika Jiji la Tanga, ndiyo Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Tanga. Cha kusikitisha hospitali ile haina *lift*, wanatumia mabaunsa, sasa mabaunsa wakati mwingine wanawadondosha wagonjwa. Hebu Serikali ifikirie kwa moyo mkunjufu kuipelekea hospitali ile lift na kuweza kuwasaidia wale wagonjwa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kujali afya zetu Serikali yetu inatilia mkazo sana kuhusu vijana wanaojihusisha na madawa ya kulevyo. Kwa kweli Serikali imejitalidi sana kupunguza hili wimbi la wanaotumia madawa ya kulevyo lakini binadamu si sawa na mnyama, binadamu ana kila mbinu ya kuweza kufanya kumshinda mnyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hivi vijana wetu wanapokosa hizi dawa za kulevyo wamekuwa wezi wa zile taa zinazowashwa nyumbani zina unga mweupe unaotoka, wanachanganya na maji ya kuchanganya sindano wanajichoma au wengine wanachukua *valium* wanasaga wanaweka kwenye sigara wanavuta. Kwa hiyo, Serikali bado ina kazi kubwa kwa hawa vijana ambao ndiyo nguvu kazi ya Taifa letu kwa sababu mimi nasema vijana ni taifa la leo. Sasa tukiwatupa hawa vijana, tukiwaacha wawe wamejihuisha kwenye madawa ya kulevyo hatimaye tutajajikuta taifa ambalo linakosa nguvu kazi. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumza kuhusu hali ya siasa. Tunajua mwaka huu 2019 tutakuwa na Uchaguzi wa Serikali za Mitaa na mwakani tutakuwa na Uchaguzi Mkuu. Katika chaguzi unapotaka kupiga kura unatakiwa uwe na kitambulisho cha uraia na cha kupigia kura. Kuna baadhi ya vijana ambao wakati vitambulisho vya uraia vinatoka walikuwa hawajatimiza miaka 18, sasa hivi tayari wameshatimiza miaka 18 lakini wakati mwingine wanapovifua tilia vitambulisho vile vya uraia inakuwa ni tabu sana kuvipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, masikitiko yangu, mimi nashangaa sisi tunaambiwa tuwe na vitambulisho vya uraia au kitambulisho cha kupiga kura ili kiweze kutusaidia wakati wa kupiga kura. Nilikuja kushangaa wakati wa marudio ya Chaguzi za Madiwani katika Kata, Mkurugenzi wangu wa Jiji la Tanga alitoa Waraka kuwa ambaye atakuwa hana kitambulisho cha kupigia kura au cha uraia anaweza kutumia aidha *passport* au leseni ya udereva. Sasa kumbe kuna leseni za udereva, *passport* na kadhalika kuna haja gani ya kuwa na vitambulisho hivyo? Hii inasababisha kuleta faulo katika uchaguzi kwa sababu watu wanachukuliwa kutoka mitaa mingine na kuja kupiga kura pale. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama hiyo haitoshi, tunajua katika kituo cha kupigia kura kuna orodha ya wapiga kura, anayekuja pale anaenda kuangalia jina lake lakini cha kushangaza kituo kile kile cha kupigia kura Msimamizi wa Uchaguzi tena ana karatasi yake nyingine. Kwa hiyo, wale wanaokuja aidha na *passport*, leseni au *birth certificate* yake wanapiga kura na unajua hivi hivi kuwa hawa watu si wakazi wa eneo husika, wanachukuliwa kwa magari, wanaletwa wanapiga kura, hii inahatarisha pia amani ya nchi. Kwa hiyo, Serikali ihakikishe kuwa anayepiga kura ni yule anayefuata masharti ya kupiga kura. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile nataka kuzungumzia kuhusu zao la michikichi. Tunashukuru Serikali imeipa kipaumbele zao la michikichi. Kweli michikichi ni zao ambalo litaleta faida sana kwa nchi yetu. Wenzetu Malaysia

wameendelea kwa sababu ya zao la michikichi. Katika historia michikichi hiyo ya Malaysia nasikia ilitolewa huku huku Tanzania ikapelekwa kwao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, naomba Serikali isielekeze kilimo cha michikichi katika Mkoa wa Kigoma peke yake ipeleke pia zao hili katika mikoa ambayo michikichi inaweza ikastawi ili watu waweze kuvuna mafuta ambapo tutakuwa tunatumia mafuta yetu sisi wenyewe kwa afya yetu kuliko kutumia mafuta ambayo yanatuathiri. Kuna mafuta tunayoletewa ambayo siyo mazuri, yana *cholesterol*/ambayo inaweza ikatuletea matatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia naomba kama itawezekana Serikali iangalie sana wazee. Kuna wazee ambao wanaishi katika nyumba za wazee wasiojiweza. Nina hakika Serikali inatenga fungu kwa ajili ya kuwahudumia wazee wale lakini utakuta hali zao ni duni halafu wanarandaranda mitaani kuomba, ile ni aibu kwa taifa letu, kumbe wana vituo vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, katika vituo vyao wangkuwa wanaangaliwa kwa malazi, chakula na kwa afya zao kwa sababu utakuta kwenye vituo vingine vya kulelea wazee wale afya zao sio nzuri, sehemu wanazo lala sio nzuri, utakuta wengine godoro analolalia lina mikojo mpaka wanatoka funza kiasi cha kumkosesha raha yule mzee. Kwa hiyo, Serikali iangalie umuhimu na pia iwasisitize wale wanaohusika kuangalia wale wazee wawe wanapata chakula cha kutosha na tiba na pia wawazuie wasirande mitaani kwa sababu anapokuja mgeni akiona watu wanarandaranda mitaani kwa kweli ni aibu kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nasema ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Maulid Mtulia atafuatiwa na Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha na Mheshimiwa Rashid Shangazi ajiandae.

**MHE. MAULID S. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia uzima na kusimama kwenye Bunge lako Tukufu. Pili, nitoe shukrani zangu za dhati kabisa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa namna anavyoliendesha Taifa letu kwa weledi mkubwa sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hotuba ya Waziri Mkuu nimeisikiliza na kwa kweli ilikuwa hotuba nzuri yenye mwelekeo na yenye matumaini. Nianze na ukurasa wa 66 hasa kwa kaka yangu pale Mheshimiwa Mavunde kwa maana nazungumzia vijana na ajira. Sisi watu wa Kinondoni tunakupongeza sana, lakini katika kipengele ambacho amenivutia sana ni kile cha kuhakikisha anatoa ajira kwa vijana; vijana wanapata ajira na mafunzo na hasa mafunzo ya kilimo cha kitalu nyumba. Nasi Kinondoni kwa maana ya Manispaa tumejenga kituo Mabwepande, vijana wanakwenda kusoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna jambo moja tu naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie pale, atuletee angalau madarasa mawili kwa ajili ya vijana wanaotoka mbali waje kukaa pale na inaweza ikasaidia kwa watu wa Temeke, Ubungo, Ilala na Kigamboni. Vijana wote wa Dar es Salaam watakuja kujifunza pale kwa sababu kutakuwa na mabweni kwa ajili ya wasichana na wavulana. Akitufanyia hilo, kaka yangu Mheshimiwa Mavunde atakuwa ametusaidia sisi pamoa na Jiji la Dar es Salaam na kwa ujumla wake atakuwa ameisaidia sana nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ofisi ya Waziri Mkuu kuna wale mavu. Kwa kweli natamani sana kama Serikali ikija na ruzuku kwa ajili ya wale mavu kwa sababu maisha ni mapambano. Kama sisi wengine tunapambana tukiwa tupo timilifu, wenzetu wanaopambana na viungo pungufu maana yake uwanja siyo *fair*. Kama tumetoa mkopo kwa ajili ya wanawake na vijana ambaao ni wazima, haiwezekani na wale mavu tukatoa mkopo kwa *condition* hiyo hiyo, kwa

sababu hawa ni watu wenye upungufu. Kwa upungufu huu lazima tutafute namna ya ku-*subsidize*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, natamani sana Serikali ije na ruzuku kwa ajili ya walemauvu, ije na vifaa kwa ajili ya walemauvu wa kutembea kama vile baiskeli, magongo, vifaa vya kuongeza usikivu na kila namna. Lazima walemauvu hao tuonyeshe kama jamii tunawajali na tunajua kwamba wenzetu wapo kwenye mapambano haya wakiwa na upungufu. Uwanja uko *fair*.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye uwekezaji. Kuna uwekezaji wa watu, kuna uwekezaji kwa maana ya ndani na uwekezaji wa nje. Nina hamu kubwa sana tuzungumzie uwekezaji wetu wa ndani. Kwanza naipongeza Serikali yangu kwa kuhakikisha imekuja na miradi mkakati mikubwa, tuklanza na mradi wa *standard gauge*. Huu mradi ni mradi mkubwa na mtu yeoyote anayeubeza mradi huu kwa kweli tutakosa kumwelewa. Hata leo mradi unakwenda una miaka; wewe mpaka leo unakuja kuubeza mradi huu maana yake utakuwa unajipotezea muda. Huu mradi ni mzuri. Vile vile tuna mradi wetu wa umeme, *ACT* na tuna miradi mingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika miradi hii, tuje na mkakati wa kuona ni namna gani miradi hii inaweza kuwajenga Watanzania? Mfano, tunajenga reli kutoka Dar es Salaam – Mwanza – Kigoma – Rwanda na Burundi wameomba wanataka nao tufike. Haiwezekani tukajenga kwa kutumia Kampuni ya Kituruki tu, lazima tuwe na ajenda. Baada ya Waturuki kuondoka, *transformation of knowledge* inapatikana? Haiwezekani tena wakiwa Congo wanataka kujenga reli kama ile, wakamtafute tena Mturuki, wanatakiwa waje Tanzania wawakute Watanzania wapo tayari kwa ajili ya kujenga reli.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano kama huu uende kwenye viwanja vya ndege. Tuna mpango wa kujenga viwanja vya ndege vya kanda vingi kweli. Viwanda vya Songwe, Dodoma, Iringa, Mtwara na Lindi. Tuna viwanja vingi

tunajenga. Hivi viwanja tunavyovijenga tutakwenda na viwanja vya mikoa, haiwezekani mpaka leo hatuna kampuni hata moja ambayo tunailea kwamba wakati viwanja hivi tunajenga kwa kutumia Wakandarasi wa nje, tukimaliza tukianza viwanja vyetu vya mikoa Watanzania wawe wana uwezo wa kujenga hivi viwanja wao wenyewe na hiyo ndiyo *transformation of knowledge*. Hili hatuwezi tukafanyiwa na mtu, lazima tuwe na mkakati nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo tunapeleka umeme vijjini, makampuni tunayotumia mengi katika vijiji vingi; hivi kweli tukimaliza mradi wa umeme vijjini Watanzania washindwe kwenda kufanya oparesheni za miradi ya umeme kwa ajili ya nchi ya Burundi, Congo na nchi nyingine? Tuendelee tu kuwa sisi kazi yetu ni kutumika!

Mheshimiwa Naibu Spika, mtazamo wangu kwa miradi yote mikubwa tunayoweka fedha nyingi, lazima tuje na mpango wa kuhakikisha elimu inabaki ili Watanzania waende mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, sisi tunajenga reli, lakini tuna mradi wetu wa kimkakati wa Mchuchuma na Liganga. Ni mradi wa muda mrefu. Mchuchuma na Liganga umesimama. Ukiangalia, kuna changamoto. Changamoto ya kwanza, mbia aliyekuja kampuni ile ya Kichina ambayo yuko na *NDC* hakuja na *capital* ya kutosha. Mradi unataka *capital* ya shilingi bilioni tatu yeye amesema anaweza akaja na *capital* ya dola milioni 600. Kwa maana hiyo, anataka atumie mradi wetu kama *collateral* kwa kukopa hela benki. Huo ukawa mgogoro wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, mgogoro wa pili, umeme utakaozalishwa kutoka pale Mchuchuma, *Megawatt* 600, 250 itumike kwenye kiwanda, 300 iingie kwenye *grid* ya Taifa; na ile inayoingia kwenye *grid* ya Taifa, anataka *Megawatt* moja atuuzie kwa senti 12 mpaka senti 15 ambayo ni ghali. Umeme wa gesi tunanunua kwa senti 6 na *TANESCO* wanauza kwa senti 11. Ukiangalia hapo unaona mgogoro mwingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa migogoro hii yote, ndiyo tusitoke? Kwa sababu tukiweza kutengeneza kiwanda cha Liganga, tukatoa chuma cha pua tungeweza kutumia kujenga kama mataruma. Vilevile tunapokwenda kwenye ulimwengu wa Tanzania ya Viwanda, visiwe viwanda nya *juice* tu, viwe viwanda nya chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mawazo yangu ni kwamba lazima Serikali ikae na hawa wabia wetu na *NDC* tutatue huu mgogoro, kwa sababu hiki kiwanda kwetu kina umuhimu mkubwa sana. Chini ya kile chuma kumechanganyika na madini muhimu sana. Kuna madini yanaitwa *vanadium* na *titanium*; ni madini muhimu na ghali kuliko hicho chuma, lakini inapatikana tu baada ya kuchimba chuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata ile reli ya kusini ambayo tunataka kujenga Mtwara mpaka kwenda Songwe ni reli ambayo inategemea mzigo huu mkubwa utakaotoka Mchuchuma na Liganga. Kwa hiyo, tusipopatana na tukaja na suluhisho, maana yake ile reli ya kusini itabaki kuwa ni ndoto.

Mheshimiwa Naibu Spika, imefika mahali Serikali sasa, nimeona kwenye mpango tumetenga fedha kwa ajili ya fidia, lakini kulipa fidia peke yake haitoshi. Namwombe dada yangu Mheshimiwa Angellah, namuamini sana, alichukue hili kama ni jambo la msingi ambalo anaweza akalisaidia Taifa, akatusaidia na sisi pia. Kwa maana mradi huu ukifanikiwa utakuwa ni mradi mkakati wa kuhakikisha kweli tunakwenda kwenye Tanzania ya viwanda na siyo viwanda nya *juice* na maji tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana ahsante. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, atafuatiwa na Mheshimiwa Rashid Shangazi. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka ajiandae.

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. Naomba nimshukuru Mungu kwa kunipa nafasi ya uzima tena. Nianze kwa nukuu ya mstari kwenye Biblia, Mithali 10:15 inasema, "*Mali ya mtu tajiri ni mji wake wa nguvu, uangamivu wa masikini ni umasikini wao.*" Waswahili wanasesema, "*mtaji wa masikini ni nguvu zake mwenyewe.*" (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mungu kwa kutupa Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli. Ni kiongozi mwenye uthubutu na *vision*, anayetupeleka kule kunakotakiwa. Kwa mtu wa kawaida anaweza asielewe, kwa mtu mwenye macho ya hapa (*short sighted*) anaweza asione tunapoenda. Miradi anayoifanya Rais Mafufuli ni miradi mikubwa (*heavy*) ambayo mtu mwelesi asingeweza kuifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi leo unaweza ukaanza kuhoji ndege kwamba hujaona faida ya ndege? Watanzania tu kwenda hapa Uganda unafikiria labda uende Kenya upate ndege ya kwenda Uganda au kwenda nchi nyngine. Leo Air *Tanzania* inaenda Uganda, Kenya na karibia nchi nyngi za Afrika inaenda sasa hivi. Kwa hiyo, ukisema huoni manufaa ya ndege ni wewe, lakini sisi Watanzania tunahitaji ndege ziendelee kununuliwa zaidi na zaidi kwa ajili ya uchumi wa nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, leo vinajengwa viwanja vya ndege kila mkoa. Sasa unajenga kiwanja kila mkoa halafu unaendaje huko kama huna ndege? Kwa hiyo, namshukuru Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, *Stiegler's Gorge*, umeme wa maji ndiyo umeme wa bei ya chini kuliko *sources zozote zile unazojua*. Leo mtu anasimama anasema tungende kwenye gesi, sijui kwenye vitu gani, atuchanganulie gharama za kila *source*. *The cheapest source of electricity* ni maji. Tangu nchi hii iumbwe haijawahi kuwa na umeme wa *Megawatt* 2,115; tunaenda kupata umeme wa *Megawatt* 2,115 kupitia *Stiegler's Gorge*. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaambie Waheshimiwa Wabunge, hakuna atakayetuhurumia Watanzania. Hayupo wa kutuhurumia sisi, tutajikomboa kwa *resources* zetu tulizonazo wenyewe. Wazungu wangependa mpate umeme wa teknolojia kubwa ambayo mtaendelea ku-*depend* kwao. Ndiyo wanataka! Hawapendi kile kitu ambacho ni rahisi kwetu, wanataka *everyday* tuendelee ku-*import* kutoka nje. Ndicho wanachotaka sisi lini tuta-*export*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, namshukuru sana Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli. Sisi Wabunge wa CCM na Wabunge wa Upinzani tumuunge mkono Rais, Mheshimiwa Dkt. Magufuli, songa mbele na *Stiegler's Gorge*. *Stiegler's Gorge* ilipingwa tangu enzi za Mwalimu Nyerere. Leo watu wanasema miti, miti; inatusaidia nini Mura kama haituingizii faida? Sisi tunataka umeme wa uhakika. Ukienda leo kila kona unakuta umeme unakatikakatika, hatuna umeme ambaa ni *stable*. Mheshimiwa Rais anasema tunataka umeme wa haraka na wa haraka ni wa *Stiegler's Gorge*...

**MHE. AHMED ALLY SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha kuna taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Ally Salum.

## TAARIFA

**MHE. AHMED ALLY SALUM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nimpe taarifa mzungumzaji kwamba Mheshimiwa Makamu wa Rais anapambana katika hii nchi kuhakikisha kwamba miti inapandwa kwa wingi sana. Wewe unasema miti inatusaidia kitu gani? (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Chacha, unaipokea taarifa hiyo?

**MHE. MARWA R. CHACHA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sasa taarifa gani hiyo? (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niingie kwenye suala la elimu. Naiomba Serikali yangu na nimwombe Waziri Mkuu na vile vile naomba Mawaziri ambao wapo chini ya Waziri Mkuu wanisikilize vizuri, hususan kwenye elimu. Tunahitaji kubadili Sera ya Elimu. Kwenye suala la vyuo vya ufundi, lazima tuliangalie vizuri kwa upya. Tunahitaji vyuo vya ufundi kila Wilaya kwa sababu tunaenda kwenye uchumi wa viwanda.

Mheshimiwa Naibu Spika, tusipokuwa na vyuo hivi, tutafeli. Kwa nini Mataifa mengi yanakimbilia kuwekeza China? Ni kwa sababu ya *manpower* ambayo ni *skillful* kwenye eneo hili la ufundi. Kwa hiyo, ili tuendelee na tuendelee kupata viwanda, unaweza ukasema unafungua kiwanda hapa ukakosa wataalam wenyе uelewa wa eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili kwenye elimu, tunahitaji kuangalia kwa upya mitaala yetu. Kwa mfano, somo la ujasiliamali ni vizuri lifundishwe kuanzia Shule ya Msingi na kuendelea ili mtoto anapomaliza Shule ya Msingi, Sekondari au Chuo asifikirie kwenda kutafuta ajira Serikalini. Leo tuna mamia wame-*graduate* wanafikiria kwenda kuajiriwa, hiyo hapana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine niongelee kidogo kuhusu *tourism*. Kwenye *tourism* Wilaya ya Serengeti, pale katikati Seronera wanapanua uwanja wa ndege. Tunahitaji uwanja wa ndege uwe nje ya hifadhi. Ukiwa nje ya hifadhi, utakuwa na *multiplier effect*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba iangaliwe *issue* ya *single entry* ambayo ina-affect sana *cultural tourism*. Leo watalii wanapoingia hifadhini hawawezi kutoka sababu akitoka anaambiwa alipe tena. Kwa hiyo, imeathiri sana *cultural tourism*. Wale ambao mpo maliasili na utalii, *single entry* siyo nzuri kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kwenye uzalishaji. Naiomba sana Serikali, kwenye eneo la kilimo, mifugo na uvuvi kama kuna vitu tunaweza kuvitengeneza sisi

wenyewe Tanzania, ni bora kuzuia *importation*ili kusababisha uchumi wetu kukua ili tuweze kuuza nje. Tumeona kwenye suala la korosho ambapo watu wa nje wanatuchazea. Kama tungekuwa na viwanda vyetu, tuna-*process* korosho, tunasafirisha, tunaenda kuuza huko, inaingiza fedha nyingi za kigeni. Kwa hiyo, nilitaka niseme hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho, ni maji. Naomba Waheshimiwa Wabunge wenzangu mniunge mkono kwenye hili. Mwaka huu kwenye *Finance Bill*/tumwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha tuongeze shilingi 50/= kwenye maji ili kukamilisha miradi ya maji vijijini.

Naomba Waheshimiwa Wabunge mniunge mkono kwenye hili, tuungane tumwombe Mheshimiwa Waziri Mpango shilingi 50/= iingie kwenye maji. Ndiyo nakuona Mheshimiwa Mpango unatikisa kichwa lakini hii ni muhimu sana. Kama Mheshimiwa Mpango amegoma kuingiza, atuletee chanzo mbadala cha kwenda ku-*finance* miradi ya maji. Hiyo tu akituletea sisi tunakubali. Kama hajatuletea chanzo mbadala, tunakula sahani moja naye, shilingi 50/= iingie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema, ninamshukuru Mungu sana, tena ningelijua ningewahi siku nyingi kwenda CCM. (*Kicheko/Makofi*)

Kabisa! Yaani nimekuja kugundua kumbe nimechelewa sana. Aisee! CCM kuzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, si unaona sina mawazo sasa hivi, nipo vizuri. (*Makofi*)

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa. Muda wako umekwisha. Mheshimiwa Rashid Shangazi, atafuatiwa na Mheshimiwa Zuberi Kuchauka. Mheshimiwa Sabreena Sungura ajiandae.

**MHE. RASHID A. SHANGAZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa nafasi hii, nami niweze kushiriki katika hoja iliyopo katika Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika sana kuona Mheshimiwa Waziri wa Fedha yupo hapa, lakini Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji yupo pale kwa sababu mambo ambayo nakusudia kuyazungumza yanagusa sana katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza uchumi wa viwanda kwa maana ya kulipeleka taifa kwenye uchumi wa kati ni lazima tuwe na *models* ambazo zinatupeleka huko. Hatuwezi tu kuwa na *model* ya viwanda ambavyo hatuelewi ni viwanda vya namna gani vitatupeleka huko. Kwa maoni yangu nadhani kwa kuwa nchi hii asilimia zaidi ya 70, 75 ni wakulima basi *model* nzuri itakuwa ni ya viwanda ambavyo vinahusianisha au vinajifungamanisha na kilimo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa ulizuka mjadala wa kuhusu matumizi ya ndege, lakini inawezekana labda tu ni kwa sababu vitu hivi sisi kama Watanzania tumechelewa kuvitumia na ndiyo maana wakati mwagine hata tukiona mizigo inapanda ndege tunaona kama ni *israafu*, lakini nataka nikwambie kwamba sehemu mojawapo itakayosaidia kukuza Sekta ya Kilimo ni kuwepo kwa ndege ambazo zinabeba mizigo, hasa mazao haya ambayo ni *perishable*. Tunapozungumza mazao kama maparachichi, mazao ya kilimo ya matunda, mbogamboga, *green beans*, *French beans*, *broccoli*, *coriander*, lakini pia na mazao ya maua, haya yanahitaji ndege ili yaweze kufika kwenye masoko kwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tatizo kubwa katika nchi yetu ni kwamba hatuna ndege nyingi za mizigo zinazotua katika viwanja vyetu. Sio katika Uwanja wa Ndege wa Dar es Salaam, sio Kilimanjaro wala sio kule Songwe, kidogo kwa watu wa Kaskazini wanatumia Uwanja wa Ndege wa Nairobi kwa kupeleka maua na bidhaa hizi za matunda na mbogamboga.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niiombe sana Wizara ya Fedha iangalie hapa kwa sababu kuna tatizo moja. Kwanza ni *airport charges* zetu ziko juu, lakini pia *landing fee* ya kutua katika viwanja vyetu ziko juu sana. Sambamba na hilo, wakiweza kuangalia pia mafuta ya ndege kwamba angalau yasiwe na tozo nyingi, najua yako *zero* lakini ingekwenda mbali zaidi kwamba angalau tuyapate kwa bei ya nafuu sana ili yavutie ndege ambazo ni za mizigo ziweze kutua katika viwanja vyetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi hapa nilimwona Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko kule Rungwe, nadhani alikuwa na Waziri wa Uwekezaji, wakiwa wanaangalia uwezekano wa kusafirisha maparachichi kuitia Uwanja wa Songwe. Sasa kama tutakuwa na ndege za mizigo zinazoweza kutua katika viwanja vyetu hivi maana yake hii itaongeza thamani ya uzalishaji kwa wakulima wetu. Kwa hiyo hili naomba tulitazame sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili katika eneo hilohilo la viwanda, hasa vinavyofungamanishwa na kilimo, ni suala zima la vifungashio. Tanzania bado tuna tatizo la vifungashio, ndiyo maana unakuta maparachichi yanayolimwa Njombe, Iringa na kwingineko yanapelekwa Nairobi yakifika kule yanafungwa katika vifungashio ambavyo ni bora na yanapelekwa kwenye masoko ya Ulaya na Marekani ambapo wanaauza kwa bei kubwa zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana Wizara hii iangalie eneo hili, kwamba tutafute wawekezaji ambao watawekeza katika viwanda vyta vifungashio ili mazao yetu yanapotoka moja kwa moja kutoka Tanzania yawe yako katika ule ubora ambao unaweza kuyafanya yakashindana kimataifa. Unaweza ukaona mfano maparachichi ambayo tunauziwa hapa Tanzania kwa shilingi labda 1,400, huko kwenye masoko ya dunia inafika mpaka dola kumi, kwa hiyo utaona kwamba ni kiasi gani cha pesa ambacho tunapoteza kwa sababu tu hatuyaandai vizuri wala hatuyawekei mpango madhubuti wa ku-process katika ubora ambao unatakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine linalojifungamanisha pia katika kilimo ni suala zima la majokofu ama hizi *cold boxes* za kusafirishia haya mazao. Mazao ya mbogamboga, matunda, yanahitaji kupata ubaridi wa kutosha kutoka kule kwenye mashamba kwenda katika hivyo viwanja tunavyozungumza au kwenda katika masoko. Katika eneo hili unakuta kwamba wakulima hawawezi kuyasafirisha yakiwa katika hali ya ubaridi. Kwa hiyo niiombe sana Wizara ya Fedha wakati tunatoa misamaha kwenye vifaa vingine vinavyosaidia kwenye uwekezaji katika kilimo kama matrektu na pembejeo nyingine, hebu tuangalie na hili suala la *cooler boxes* na *cold rooms* ambazo zinasaidia sana wakati wa usafirishajji wa haya mazao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa wale ambao wamepata bahati ya kuwa na miradi ile ya *MIVARF* katika maeneo yao watakuwa ni mashahidi kwamba *MIVARF* wameweza kujenga *cold rooms* ambazo zinaweza kubeba mazao hata kwa tani 15 mpaka 20, lakini tatizo lipo kwenye kuyatoa kule kwenye vijiji kuyaleta kwenye vile vituo ambavyo ni *post harvest centers*, pale lazima wananchi wetu waweze kupata *incentive* kwenye kodi ili waweze kuwa na hivi vifaa na waweze kuongeza uzalishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye kilimo bado tuna uwezo sasa wa kuhakikisha kwamba tunapata viwanda ambavyo vinakwenda kuongeza thamani kwa maana ya kupata pembejeo na madawa pamoja na viuadudu katika mazingira yetu hapahapa, lakini pia sambamba na uzalishaji wa mbegu. Tatizo la mbegu limekuwa ni tatizo kubwa sana kwa sababu mbegu zetu nyingi zinatafitiwa kutoka nje. Kwa hiyo niombe sana Serikali iongeze pesa katika vituo vyetu vya utafiti ili kutokana na mabadiliko haya ya tabianchi ambayo yameendelea kuikumba nchi yetu wananchi waendelee kubadilisha aina ya mazao kwa sababu bado mpaka sasa hivi wananchi wengi wanapanda mazao mengi kwa mazoea lakini kiuhalisia kwa kweli hayana ubora ule ambao unaweza ukashindana katika soko.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo nataka kulizungumzia ni la madawa; juzi Kamati ya *PAC* tulitembelea Bohari Kuu ya Madawa (*MSD*) na tukakutana na wenzetu wa Nchi za Kusini mwa Afrika (*SADC*), karibu nchi 16 walikuja pale kufunga mkataba na *MSD* ili iweze kuagiza madawa kwa niaba ya hizo nchi 16 na kufanya *deliveries*.

Hata hivyo, changamoto kubwa ni kwamba hapa ndani uwezo wa viwanda vya ndani katika soko la madawa ni asilimia nne peke yake na bado napo kuna tatizo la kwamba hatuna viwanda vya kutosha vya madawa, hata dripu tunaagiza nadhani kutoka Uganda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nimwombe sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana hii ya uwekezaji kwamba sasa tujaribu kupata *incentive* nzuri kwa ajili ya kuhamasisha viwanda vya madawa vijengwe hapa nchini ili tuweze sasa kupata hili soko la Kusini mwa Afrika. Kama nchi 16 leo zinachukua madawa kutoka Bohari Kuu ya Madawa maana yake ni kwamba hayo madawa yanegkuwa yanazalishwa hapa nchini moja kwa moja hii ingekuwa ni faida kwetu, lakini leo *MSD* anageuka tu kama *agent* wa kuagiza kwa makampuni mengine ya nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, la mwisho kabisa ni kwa Bandari ya Dar es Salaam; bado Bandari yetu na Mamlaka ya Mapato Tanzania sio rafiki sana kwa uwekezaji, kuna mambo mengi ambayo yanafanyika pale kila siku tunarudi nyuma, kila siku wanaanzisha mambo mapya. Kwa hiyo tunapozungumza suala zima la uwekezaji ni lazima Serikali nzima iwe inazungumza, Wizara zote zizungumze na kuwe na *connection* kwamba mizigo inapotoka nje inapofika katika bandari zetu ichukue muda mfupi na iweze kwenda kule ambako inakusudiwa. Kama tutakuwa tuna bandari ambayo inachelewesha mizigo, basi hata ile dhana nzima ya kwamba nchi yetu inavutia wawekezaji itakuwa haifanyi kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa muda wako. (*Makof*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, atafuatiwa na Mheshimiwa Sungura na Mheshimiwa Hussein Mohammed Bashe ajiandae.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nami jioni ya leo niweze kuchangia hotuba iliyo mbele yetu. Awali ya yote niseme namshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai wa kuweza kusimama jioni hii na kutoa mchango wangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila kuchelea nataka nitoe vilevile pongezi zangu za dhati kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na wateule wote kwa kazi nzuri inayofanywa na vilevile niwaombee dua kwa Mwenyezi Mungu awape umri mrefu ili waweze kuitumikia nchi yetu twende kule ambako Tanzania inataka kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nianze na kwa nini watu kila wakisimama hapa wanamsifia sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa kweli kama kuna mtu anachelea kumsifia Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, anafanya dhambi. Yapo mambo ambayo Mheshimiwa huyu Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yanafanya katika nchi hii hayakutegemewa kwa miaka mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata mimi nilivyokuwa upande wa pili alivyokuwa anaanzisha hii miradi mikubwa nilikuwa na wasiwasi hizi fedha zitapatikana wapi lakini kitu cha ajabu kilichotokea sasa hivi, tuna miradi mikubwa mingi inayofanywa na inafanya kwa pesa zetu. Kama miradi hii ingeweza kutekelezwa kwenye awamu zilizopita leo Tanzania tusingekuwa hapa tulipo. Sasa kwa nini huyu mtu ambaye ana maono ya namna hii tusimpe sifa, tusimtie moyo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna miradi, kwa mfano kuna kuna huo mradi wa *Stiegler's Gorge*, kuna ununuzi wa ndege, kuna ujenzi wa reli (*SGR*), kuna ujenzi wa viwanja vya ndege, tunajenga hospitali wilayani, tunajenga vituo vya afya kwenye kata zetu. Nani ambaye anaweza akasimama

kwenye Bunge hili ambaye kwenye wilaya yake hakuna kituo cha afya kinachojengwa? Kwa spidi hii ya ujenzi wa vituo vya afya kama huko miaka ya nyuma tungekuwa tunajenga namna hii, kwa spidi hii leo hii kuna kata ambayo ingebaki haina kituo cha afya?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tunapokwenda namna hii, tunajenga *flyover*, Dar es Salaam sasa hivi kunakwenda kujengwa *flyovers* zaidi ya tatu. Jamani, kwa nini tuache kusifia? Ni lazima tutasifia, ni lazima tutam-*support* na lazima tutamwombea dua Mwenyezi Mungu ampe umri mrefu.

Mheshimiwa Naibu Spika, dhana ya Mheshimiwa Rais kutokutoka nje ya nchi hii sasa tunakwenda kuona faida yake. Kwa nini Mheshimiwa Rais alikuwa amesema kwamba hataki kusafiri nchi za nje; yuko tayari kulinda rasilimali za nchi hii ili ziweze kuwanufaisha watu wote na ulinzi wa rasilimali za nchi hii tumeuona kwa sababu katika hali ya kawaida watu walikuwa wanasema kwamba Mheshimiwa Rais hasafiri, tutapataje misaada? Yuko ndani na tunafanya mambo yetu, *big up* sana Mheshimiwa Rais. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nichangie kwenye uwekezaji; kwenye uwekezaji nchi yetu inafanya vizuri, ni kwa sababu kubwa mbili. Kwanza ni kwa ajili ya amani yetu tuliyonayo na usalama, wawekezaji wanahakikishiwa usalama, kwa sababu wanakuwa salama na amani, mali zao zitakuwa salama. Hata hivyo, tunapwaya upande mmoja kwenye uwekezaji, Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji naomba anisikilize hapo; bado tuna tatizo la njoo kesho, njoo keshokutwa, hapa ndipo tunapokwama. Leo hii mwekezaji, nitoe mfano mmoja, jana nimemsikia Mheshimiwa Rais akiwa Mtwara, kuna mwekezaji mmoja pale amewekeza kiwanda, transfoma za umeme kanunua mwenyewe, amekwenda Idara ya Maji wanamwambia atoe milioni 100 wamletee maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa msingi huu hata kama tuna sifa nzuri kwamba bwana Tanzania ukiwekeza mali zako zitakuwa salama, ni nchi yenye utulivu, lakini bado akija

ndani hapa anakutana na vikwazo vya njoo kesho, njoo keshokutwa, hili Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana naomba aliangalie kwa makini sana, bado kuna watu kwenye ofisi yake wana tabia ya njoo kesho, njoo keshokutwa. Inawezekana haohao ndio wapinzani wa Mheshimiwa Rais, kwa sababu haiwezekani mpaka leo hii kuna mteule wa Rais hajui mwelekeo wa nchi inapokwenda, hajui Mheshimiwa Rais anataka nini. Wapo watu wanashindwa kufanya maamuzi, wanashindwa kujua kwamba wamebekwa pale kwa sababu gani; Mheshimiwa Waziri naomba alichukue hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nielekee kwenye kilimo; kwenye kilimo kuna matatizo makubwa mawili, kwanza upatikanaji wa pembejeo kwa wakati na masoko. Suala la pembejeo kwangu mimi linachukua nafasi ya pili ukilinganisha na suala la masoko. Tunalo tatizo kubwa sana la wakulima wetu wanahangaika na masoko na ndiyo maana sasa hivi wakulima wanabadilisha mazao kila mwaka. Mwaka juzi korosho Kusini zimefanya vizuri, watu wameacha kulima mpunga, wameacha kulima mazao mengine wamekwenda Kusini kulima korosho, mwaka huu korosho zimeyumba bado wakulima wetu wanahangaika. Kwa hiyo, naomba kwenye upande wa kilimo tujikite sana kwenye kutafuta masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kwenye upande wa maliasili; upande huu naomba sana Serikali ije na marekebisho ya Sheria ya Kifuta Machozi. Sisi tunaopakana na hifadhi tunapata shida sana mazao yetu kuliwa na wanyama, lakini hakuna sheria ambayo mkulima yule anapata fidia, kuna Sheria ile ya Kifuta Machozi. Naomba Serikali ije na marekebisho ya sheria, angalau sasa tuanze kufikiria kuwafidia wale ambao mazao yao yataliwa na wanyama wakali.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la umeme, *REA*; upande wa *REA* hapa hatujafanya vizuri. Ipo mikoa ambayo imefanya vizuri, ile tu ambayo imepata wakandarasi wanaojielewa, lakini kuna mikoa mingine ambayo imepata wakandarasi wa hovyo, mikoa ile bado *REA* haijafanya vizuri.

Sielewi ni kwa sababu gani, Serikali ilikuwa na vigezo gani mkandarasi mmoja anapewa mikoa zaidi ya mitatu, matokeo yake anafanya mkoja mmoja mingine anasahau. Kwa hiyo, naomba Serikali iangalie upya suala la *REA*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano katika Wilaya yangu ya Liwale, katika *REA* awamu ya tatu, Sehemu ya Kwanza ambayo ilikuwa na vijiji 14 mpaka leo kumewashwa vijiji viwili tu na mkandarasi yule amepotea. Tena kibaya zaidi mkandarasi yule anatuchonganisha sisi na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa sababu tangu alipopewa Mkoa wa Lindi, alikwenda Ruangwa akamaliza alipomaliza vijiji vya Ruangwa amekimbia. Sasa sjui kama aliambiwa kwamba Mkoa wa Lindi una wilaya moja, hatujui. Kwa hiyo naomba sana, suala la *REA* hawa wakandarasi waangaliwe upya, wale wakandarasi ambao wanaonekana kabisa wanaikwamisha Serikali kufikisha malengo yake waondolewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba, asilimia kubwa sisi tunazungukwa na hifadhi, lakini vilevile kuna Sheria ya Misitu. Naiomba sana Serikali, hebu twende turekebishe Sheria ya Misitu, asilimia tano kwa uvunaji wa mazao ya misitu inayopata halmashauri ni fedha ndogo sana ambazo hazilingani na jangwa au na uharibifu mkubwa wa misitu unaofanywa kwenye halmashauri zile.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna fedha ambayo imetengwa kwa ajili ya kupanda miti, kwamba baada ya uvunaji wa miti panakuwa na fedha zimetengwa, asilimia mbili, kitu kama hicho kwa ajili ya kupanda miti, mimi kwenye Halmashauri yangu ya Liwale sijawahi kuona kijiji hata kimoja kimepanda miti zaidi ya kukuta kwenye shule tu, ile miti ambayo inapandwa kwenye bustani za shule. Kwa hiyo, naomba kifungu hiki sasa kiondolewe kipelekwe kwenye halmashauri, ile asilimia inayokwenda hamashauri ifike angalau asilimia 10.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala hili la wazee, leo ni mara ya tatu naliongelea suala hili. Wazee wanatamkwa sana, ukienda kwenye hospitali zetu utakuta kuna *labels*

zimeandikwa pisha wazee, watangulize wazee, lakini bado Serikali haijatuletea sheria ya kuwatambua hawa wazee, hawa wazee tunaokwenda kuwakusudia ni wazee wa aina gani. Ni bora sasa Serikali ikaharakisha mchakato wa kuleta sheria ambayo sasa hawa wazee tunaokwenda kuwatungia sheria wanatambulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye suala la elimu maana mimi nadondosha sehemu mojamoja tu. Suala la elimu; suala hili bado hatujafanya vizuri. Tumefanya vizuri kwa kufanikiwa kupeleka watoto wengi shuleni, hili jambo tumefanya vizuri, lakini kwenye ubora wa elimu bado tuna tatizo. Tunacho kitengo chenye kazi ya kukagua, wanaita Kitengo cha Ukaguzi wa Ubora wa Elimu, kile kitengo hakina vitendeakazi, hata magari hawana, mafuta hawana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeweza kufanya ziara, unakwenda kwenye shule unauliza shule hii imekaguliwa kwa mara ya mwisho lini, watakwambia ni miaka miwili, miaka mitatu shule haijakaguliwa. Jambo hili ni jambo ambalo linatakiwa litiliwe maanani, kwamba hiki Kitengo cha Ukaguzi wa Ubora wa Elimu sasa ni wakati kinatakiwa kijengewe uwezo kupewa magari na fedha za mafuta ili kuweza kukagua maeneo yetu haya na hapo ndipo elimu yetu itakapoweza kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio ukaguzi peke yake, bado tumuangalie Mwalimu. Jambo kubwa kwenye elimu, mtu wa kwanza kumwangalia ni Mwalimu; je, Serikali imeshafanya tathmini kwamba madeni ya Walimu yamefikia kiwango gani, mpaka leo hii ni walimu wangapi wanaidai Serikali na mpaka leo hii kiasi gani walimu hawa wanadai? Wengine wanadai likizo, wengine wanadai kupandishwa vyeo, wengine madaraja, bado kuna tatizo kubwa kwa upande wa walimu. Kama tukiamua kucheza na walimu maana yake tunakwenda kucheza na elimu. Mimi jambo hili kwa upande wa elimu naomba sana kwamba litiliwe mkazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho, naiomba Serikali ifanye tathmini kuangalia majengo au mahitaji ya wilaya, kata na vijiji vyetu. Kwa sababu Mheshimiwa Rais amesema hana mpango wa kuongeza sehemu za tawala kwa maana kwamba hawezi kuongeza wilaya, mkoa, kata wala tarafa ni mpaka mahitaji kwenye maeneo hayo yamekamilika. Je, Serikali imeshafanya utafiti?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye Halmashauri au Wilaya yangu ya Liwale haina jengo la mahakama, jengo la polisi, Hospitali ya Wilaya wala nyumba ya Mkuu wa Wilaya na ina miaka 43. Kwa hiyo, ni lazima Serikali ije na mpango na takwimu ijue kuna wilaya ngapi zimekosa majengo ambayo yanaitambulisha wilaya, mikoa au kata zetu. Haiwezekani unakwenda kwenye kata hukuti jengo linaloitambulisha kata, hakuna zahanati, kituo cha afya, kituo cha polisi au mahakama ya mwanzo, sasa unasemaje pale ni kata? Ni vitu gani vinavyokwenda kutambulisha maeneo haya? Kwa jambo hili naiomba Serikali iwe makini sana na ije na takwimu sahihi kuhakikisha kwamba haya yote tunakwenda kuyasimamia.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa  
Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana na napenda kuunga mkono hoja kwa asilimia mia kwa mia. *(Makof)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Sabreena Sungura atafuatiwa na Mheshimiwa Hussen Mohamed Bashe, Mheshimiwa Deo Ngalawa ajiandae.

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika bajeti iliypopo mbele yetu. Kwanza kabisa, napenda

kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa uhai na afya bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuchukua fursa hii kuwapa pole viongozi wangu tukiongozwa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni kwa kufungwa takribani miezi minne wakiwa mahabusu na kukosa dhamana hali iliyopelekea kwa kweli Kambi yetu kuyumba na wanachama kuhuzunika takribani nchi nzima kwa kitendo kama hicho. Nawapa pole sana nawaombea Mwenyezi Mungu aweze kuwapa subira. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kukishukuru Kiti chako, nikianza na Mheshimiwa Spika lakini na wewe mwenyewe na Mawaziri na Wabunge mbalimbali ambao kwa namna moja au nyngine walipata kunijulia hali pale nilipopata hitlafu ya kiafya. Nawashukuru sana na Mwenyezi Mungu awabariki. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye mchango wangu. Wananchi wa Mkoa wa Kigoma wamenituma na wanahoji kwamba katika Mpango wa Maendeleo kulikuwa na suala zima la ununuzi wa meli ya uvuvi katika Ziwa Tanganyika lakini wameshangaa miaka inaenda meli hii bado hajawenza kununuliwa wakati ni kitu ambacho kipo kwenye mpango. Kwa hiyo, wanaomba kwenye bajeti ya mwaka huu basi meli hii iweze kupatikana ili sasa wananchi waweze kupata fursa mbalimbali kutokana na suala zima la uvuvi. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ambalo napenda kuzungumzia na napenda kutoa shukrani kwani kwenye ziara ya Waziri Mkuu alivyokuja Kigoma kwa kuendeleza zao letu la mchikichi na kuanzisha Kituo cha Utafiti katika Mji Mdogo pale Kihinga na kuwezesha kupandikiza miti takribani 4,000 ikiwa na lengo la kwenda mpaka miche 5,000,00. Tunaomba Serikali isiishie hapo iweze kutusaidia kutafuta wawekezaji ili waweze kuwekeza hususani katika Bonde la Mto Luiche kwa kuwa watu wengi sana wana nia ya kuendeleza kilimo hicho lakini *issue* ni masuala ya kifedha.

Pia watusaidie kwa Benki yetu ya Kilimo iwawezeshe wananchi kwa masharti nafuu kabisa waweze kupata mikopo na waweze kuitumia fursa hii adhimu ambayo imeletwa katika mkoa wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tungeomba wawekezaji wa zao la mhogo. Nimesikia China ni wanunuzi wazuri sana wa zao mihogo na Mkoa wa Kigoma tumekuwa tukilima sana zao hili. Tunaomba Serikali itusaidie na sisi kupata wawekezaji na wanunuzi kwenye zao hili ili angalau wananchi wetu waweze kuendeleza kilimo hiki ambacho kitakuja kuwa na tija kwa mkoa na kwa taifa kwa jumla. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wafanyabiashara wa Mkoa wa Kigoma na Tanzania kwa ujumla wamekuwa na malalamiko mengi kuhusiana na masuala mazima ya biashara. Wanasema biashara imekuwa na mlolongo mrefu. Ili mtu aweze kufungua biashara yake na *ku-establish* na ikakaa kwenye mstari mlolongo wa vitu vingi sana vinahitajika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, mtu anataka kutoa ajira kwa vijana, anataka kufungua ofisi, anahitajika ali pe *Pay As You Earn, Income Tax, OSHA*, kwenye Manispaa katika Halmashauri zetu, *Workers Compensation Fund*, bado kuna mifuko mingi, *NSSF* na kadhalika atoe michango na *Withholding Tax*. Kwa hiyo, kumekuwa kuna mlolongo wa vitu vingi, mambo ya *fire* na kadhalika, ambapo ni mtu anajitahidi kutengeneza ajira mambo yote haya anatakiwa alipie. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili kwa namna moja ama nyingine ni kikwazo kwa wafanyabiashara wetu. Kwa wale wanaotoka nje pia, wanatakiwa *wa-obtain Certificate of Incentive* kuititia pale *TIC*, tumekuwa na mlolongo wa vitu vingi. Nashauri Watanzania wa kawaida na wenyewe wasaidiwe, kama ilivyowekwa *One Stop Center* basi na Watanzania wa kawaida wanapotaka kuanzisha biashara zao mazingira yaye rahisi mtu akienda sehemu moja aweze kupata vitu vyote kwa wakati na aweze kufanya biashara

zake ili aweze kupata kitu ambacho kitasaidia Taifa na yeye mwenyewe na familia yake kwa ujumla. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuzungumzia suala zima la dhamana lakini pia na mlundikano wa mahabusu katika magereza yetu. Tumekuwa na mlundikano wa mahabusu wengi kwenye magereza zetu bila sababu za msingi. *Police bail* imekuwa ni shida katika nchi hii na kumekuwa kuna mchezo watu hawapewi dhamana kwa makusudi tu wakisingizia kwamba haya ni maagizo kutoka juu lakini wakati mwininge hakuna maagizo yoyote kutoka juu, huko juu ni wapi, ni mbinguni? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, urasimu tu unafanyika huku chini mtu anaamua kusema kwamba ni maagizo kutoka juu. Mimi siamini kama kuna sehemu yoyote ambayo ni juu kuna watu wapo kwa ajili ya kuwakandamiza watu wengine. Nashauri Serikali iweze kuingilia katilili haki za dhamana ziweze kupatikana na mahabusu waweze kupungua katika magereza zetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, unaweza kushangaa mtu kama Kiongozi wa Upinzani Bungeni ni Mbunge ana dhamana ya wananchi, ana familia, ana mali, amewekeza katika nchi hii, unamnyima dhamana mtu huyu akikimbia atakwenda wapi? Kwa hiyo, tuwawezeshe watu wetu basi ili Watanzania angalau na wenyewe wawe mionganoni mwa watu wanaoishi katika nchi za watu wenyewe furaha. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni kuhusu Wakuu wetu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya, hii amri ya kuwafunga watu saa 24 mpaka 48 ni mbaya na inaingilia mamlaka ya vyombo vingine ambavyo vimewekwa kwa mujibu wa Katiba. Unaweza kukuta baadhi ya maeneo Daktari amefanya tu jambo la kawaida ambalo lingeweza kuzungumzwa ama hatua zikachukuliwa kwa mujibu wa sheria lakini unakuta kosa limefanyika na Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa anatoa amri ya kumfunga Daktari ndani saa 48 lakini kumbe kule *theater* kulikuwa na wagonjwa hata 5, 6, 7, 8 ambao wanatakiwa wafanyiwe upasuaji. Kwa hiyo,

unakuta ni *administrative decision* ndogo imefanyika lakini ukienda kuangalia huko ndani zaidi inaathiri watu wengi sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mzee wangu Mheshimiwa Mkuchika hapa alisema, Serikali haiwezi kuwa kama nyumba ya kambale kila mtu awe na sharubu, kwamba kila mtu awe na haki ya kamata, funga, fanya hivi fanya hivi. Kama tumepeana maeneo ya kusimamia, wewe simamia haki, simamia kufungwa, simamia ulinzi, simamia hiki; basi kila mtu afanye kazi ambayo inamhusu. Kwa kweli hili suala la kuwapa mamlaka wenzetu kufunga watu saa 24 - 48, nafikiri siyo sahihi na ikiwezekana Serikali iweze kuleta sheria hapa tufanye *amendmentili* kuondoa hiki kipengele kwa sababu wananchi wamekuwa wakikilamikia sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo napenda kuchangia ni posho za Madiwani. Halmashauri yangu ya Buhigwe wamekuwa wakilalamika takribani zaidi ya mwaka hawalipwi posho zao. Sisi hapa ni Wabunge hata tukifanya semina tu mtu akakosa kulipwa nafsi inahaha kama vile sijui amekosa kitu gani katika ulimwengu. Sasa tuwaangalie wenzetu hawa ambao mtu anafanya kazi miezi sita, mwaka mzima, ni Diwani na hawana shughuli za maana za kufanya huko lakini wanakosa hela ndogo ambayo ingewasaidia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi sishangai hii hama hama ya watu kutoka chama kimoja kwenda chama kingine ni kwa sababu ya ukata. Hakuna shujaa wa njaa, mtu ye yote akipata njaa ikamzidua lazima atasalimu amri. Kwa hiyo, unaweza kukuta kuna wimbi la watu kuhama kumbe njaa na yenye we imekuwa ni sababu. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri Serikali iweze kuwasaidia basi Madiwani wetu ambao sehemu mbalimbali nchini wanadai waweze kupatiwa...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

## TAARIFA

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waitara, muda wake ulikuwa umeisha tayari, utapata fursa ya kujibu. (*Makofi/ Kicheko*)

**MHE. SABREENA H. SUNGURA:** Mheshimiwa Naibu Spika...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sabreena, muda wako ulikuwa umekwisha, kengele ilishagonga, kwa hiyo, umeshamaliza muda wako. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Hussein Mohamed Bashe, atafuatiwa na Mheshimiwa Deo Ngala na Mheshimiwa Jitu Soni ajiandae.

**MHE. HUSSEIN M. BASHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa fursa. Awali ya yote, nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia sote kukutana katika Bunge hili la bajeti na kutimiza wajibu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, nitumie nafasi hii tena kumpongeza Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kauli ambazo wamekuwa wakitoa zaidi ya mara moja, mara mbili juu ya namna ambavyo watendaji wa Serikali na Serikali nzima inatakiwa ku-*act*na ku-*behave* katika suala zima la uwekezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaongelea mambo mawili. La kwanza nitaongelea suala la *investment*. Suala la pili nitakaloliongelea ni la kilimo. Ukitazama takwimu za *World Bank, The Economic Update No.11* iliyotolewa mwaka huu, inaonesha kwamba idadi ya Watanzania walioongezeka katika umaskini toka mwaka 2012 mpaka leo ni Watanzania

millioni mbili. Watanzania milioni mbili wameongezeka kwenda kwenye umaskini. Kwa nini? Nitaeleza baadaye.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia asilimia 60 ya *population* ya nchi yetu au mpaka 70 ipo katika sekta ya kilimo. Mipango yetu yote tunayofanya kama nchi na *financing program* zetu zote tunazozifanya kama nchi ni lazima ziangalie ni namna gani zina-*improve productivity* na kuhakikisha kunakuwa na masoko ya uhakika ya wakulima ili tuweze kuondoa watu wetu katika umaskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukitazama *financing* ya sekta ya kilimo kwa miaka mitatu mfululizo, tunachowekeza katika sekta ya kilimo kinazidi kupungua kila mwaka. Tunachowekeza na kile tunachoki-*disburse against* bajeti yetu ya maendeleo, haviwiani. Sekta yetu ya kilimo inachangia asilimia 29 ya *GDP* ya taifa letu lakini inatengewa *less than 5% ya development budget*. Wakati huo huo *population* yetu inaongezeka kwa wastani wa asilimia 3, hili ni tatizo, ni lazima watu wataendelea kuongezeka kwenye umasikini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nini ushauri wangu katika hili? Hakuna njia tunayoweza kuondoa watu kutoka katika umaskini kama hatutofanya mambo matatu. La kwanza, ni lazima tuanzishe *Price Stabilization Fund* kwenye eneo la kilimo ili wakulima wanapokutana na mtikisiko wowote wa soko la dunia ama *unpredictability* kwenye bei za dunia tuna njia ya kuwaokoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kunapotokea hili tatizo, mimi ninazo takwimu za toka mwaka 2014 – 2017, zao la pamba msimu wa mwaka 2013 kwenda mwaka 2014 *production* ilishuka kwa asilimia 30; mwaka 2015 ilishuka kwa asilimia 17; mwaka 2016 ilishuka kwa asilimia 16; mwaka 2017 ilishuka kwa asilimia 18 na mwaka huu lime-grow kwa *initiative* iliyofanywa na Serikali. Zao la korosho ukiangalia toka mwaka 2014 lilikuwa lina *negative trend* lakini mwaka 2017/2018 zao hili lime-grow ni kwa sababu tuliwekeza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu, moja, kama nchi ni lazima tuanzishe *Price Stabilization Fund* kwa ajili ya mazao ya kilimo. Mbili, ni lazima tuanzishe mfuko wa ku-subsidize *inputs* kwa sababu mazao tunayoyazalisha kwa ajili ya kwenda kwenye *export* sisi hatuna uwezo wa ku-control bei nje, tuna uwezo wa ku-control uzalishaji na *quality*. Sasa mzalishaji mfano wa mahindi, kama tutakapompa mbolea, viuatilifi hatutotoa ruzuku katika maeneo haya maana yake gharama ya uzalishaji itakuwa kubwa, soko halipo au halipo la uhakiki, matokeo yake mkulima huyu atakata tamaa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesoma mpango ambao umesomwa na Wizara ya Fedha ambao tutaujadili, ningeshauri katika misingi na maeneo makuu matano ambayo Wizara ya Fedha wamesema, eneo la kufungamanisha ukuaji wa uchumi na maendeleo ya watu, hapa wametaja suala la elimu, maji na afya ni lazima tuweke wazi (*precisely*) *component* ya kilimo, kwamba ni eneo muhimu la kufungamanisha uchumi na maendeleo ya watu ili liweze kupata *priority*. Kwa sababu tukianza kulijadili kwa staili hii tuaanza kulitengea fedha tunapokuwa na uwezo. Hili ni eneo la kwanza. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ni la masoko, nini ushauri wangu? Tumeanzisha *Tanzania Agricultural Development Bank*. *TADB* kuna tatizo la *structure* kwa sababu *TADB* iko chini ya Wizara ya Fedha, Bodi ya Mazao mchanganyiko, *NFRA* na Bodi zingine ziko chini ya Wizara ya Kilimo, kuna suala la *marketing* ambalo liko chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara na kuna suala la *investment* ambalo liko chini ya Wizara ya Waziri Mkuu. Ushauri wangu ni lazima kutafutwe njia ya kutengeneza *a strategic alliance* kati ya hizi Wizara zote kwenye suala la *marketing* ya mazao ya wakulima ili Bodi ya Mazao Mchanganyiko kama tunaenda kwenye msimu waweze ku-*plan* nje kuna mahitaji ya mahindi kiasi gani, masoko yako wapi, Serikali isihitaji ku-*finance*, *TADB* awa-*finance* wanapokuwa wamepata *contract* za kuuza mazao nje. Hii itasaidia *predictability* ya mazao tunayozalisha. Tusipofanya namna hii, aje kiwanda cha magari na kadhalika,

viwanda hivi havita-*break even*, havitaweza kuzalisha kwa sababu sehemu kubwa ya watu haina *purchasing power*. Hili ni jambo la pili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la tatu ambalo nataka nishauri na mimi niipongeze Wizara ya Fedha nimeona kwenye mpango wameongelea uboreshaji wa mazingira wezeshi kwa uendeshaji wa biashara na uwekezaji. Lazima Serikalini watu wafahamu kwamba suala la mtu kuchukua shilingi mia moja yake kwenda kuiwekeza kwenye nchi au mji *number one* ni *perception* kwamba naamini shilingi mia yangu nayoenda kuiweka pale iko salama.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo Kariakoo *is dead* na mimi nimpongeze Waziri Mkuu alienda kukutana na wafanyabiashara wa Kariakoo. Nawaomba suala la *Blue-print* kama linahitaji mabadiliko ya sheria leteni tubadilishe. Suala la *Blue-print* kama linahitaji *harmonization* ndani ya Serikali ifanyike. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *World Bank* wametoa ripoti, wamesema *key areas* ambazo zinatumbua sisi Tanzania kwenye suala la *investment* ni kwamba moja, kuna utitiri wa kodi ndogo ndogo. Mbili, hakuna *simplicity* kwenye suala la ulipaji wa kodi na tozo. Tatu, wanashauri kuwe kuna *simplified system and predictable tax regime*. Haya yatatusaidia watu kuja kuwekeza. Jamani, ambalo nataka nishauri na hapa Waheshimiwa Wabunge wengine wamesema, leo inaanizishwa *Task Force* inaenda Kariakoo pale inasimama, eti ile *Task Force* ina Polisi, haijui kukusanya kodi. Polisi kasomea wapi ukusanyaji wa kodi? Ina TAKUKURU; TAKUKURU kasomea wapi ukusanyaji wa kodi? Ina watu wanasmewa kutoka Idara nyeti za Serikali, ina watu wa *TRA*, na kadhalika. Kundu la watu limekaa pale Kariakoo, mtu kanunua mfuko wake anaambiwa leta *TRA* aah, hii ni feki huyu.

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu mtu katoka Kongo anajuaje kama ile karatasi ya *EFD* mashine yake ni feki? Hawezi kujua, atabebwa, anawekwa Msimbazi Kituo cha Polisi. *Next time* haji, anaenda Uganda; anaenda nchi

nyingine. Hii ni shida. Ni lazima suala la ukusanyaji kodi liachwe mkononi kwa watu waliosomea ukusanyaji wa kodi. Polisi wakafanye kazi yao, TAKUKURU wakafanye kazi yao. Hii ni *dis-incentive*.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo ukienda kwenye soko letu la hisa, *trade volume* imeshuka sana, *share prices* za share zilizoko kwenye soko la hisa zimeshuka. Kwa sababu gani? Sababu ni chache tu. Moja, *there is no investors* wanaoenda kununua na kuuza *shares*; wanaoenda kununua *shares*, watu wameshikilia share zao. Pili, maana yake hakuna *surplus*, hakuna fedha za ziada ambazo watu wanataka kuwekeza. Tatuhii, kuna kuwa na *unpredictability*. Kwa hiyo, tusipofanya haya mambo kuwa na sera ambazo ziko *predictable* katika suala la *investment*, hatuwezi kuondoka hapa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la mwisho ambalo nataka nishauri, leo tumewekeza sana kwenye ndege, *It is very good*. Nami nataka niseme, uwekezaji wa ndege *is not for itself*, lakini uwekezaji wa ndege ni *means to drive other sectors*. Tumewekeza kwenye ndege, tumejenga viwanja vya ndege, nami nimshauri Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Waziri wa Fedha ni lazima uwasainishe Wizara wa *Tourism Performance Agreement*, kwamba wanakuongezea *tourists* kiasi gani kurudisha *investment* uliyoifanya kwenye ndege? Ni lazima kwa sababu hizi ndege ambazo tumewekeza, tunajenga viwanja vya ndege kwa kasi sana, tunafungua nchi yetu, ni lazima tuweze kupata *return* kutokana na hii *investment*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *investment* hii, hatutaki tuone *ATCL*; nami kwanza niseme tu wanasiasa, hebu nitajieni *Africa Airline* gani *ina-make profit?* Hakuna! *They are making loss. It is not true.* *African Development Bank* wame-predict *Airline sector Africa globally ita-make 3 million US dollar loss*, zote! Sasa hizi *Airline* zinafanya nini? Zinakuwa ni *feeders* za *sector* nyingine. Kwa hiyo, ni lazima sekta nyingine tuzitengenezee utaratibu wa kujua kwamba tumewekeza shilingi 100 kwenye ndege, wao wanaleta shilingi ngapi?

Tusiseme tu tuna *Bombardier* tuna *Dreamliner*, tuna nini; ni lazima hizi ndege zitusaidie kukuza sekta nytingine. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, tunajenga reli. Mimi niseme hapa, nilisikitika sana. Tanzania imewekeza sana Kongo kwenye usalama. Tumewekeza sana. Askari wetu wamepoteza maisha yao. Sisi Rais wa Kongo kaapishwa, nilikuwa nafuatilia, wawakilishi wetu kama nchi wametua, wameenda kwenye kuapisha, wamegeuza.

Mheshimiwa Spika, Kenya katua Rais wa pale na *delegation* ya wafanyabiashara 60, wamekaa kusaini mikataba, kesho yake kaondoka. *The first visit* ya Rais wa Kongo *is Kenya; and you know what?* Wamesaini makubaliano ya Kenya itaenda ku-train civil servant wa Kongo. *This is a forex.* Katoka pale *CEO round table* zilliofanyakwa Rwanda, kaenda Kigali *three days*. Naishauri Serikali, ni lazima tuwe *business oriented.* *This is very important.* Bila hivyo, Waziri wa Fedha hapa atakuja kudondoka na *pressure.* Tunaomba maji, tunaomba nini, *he cannot do anything.*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, nashukuru. (*Makofî*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Jitu Soni, atafuatiwa na Mheshimiwa Asha Abdallah Juma. Mheshimiwa Mussa Rashid Ntimizi, ajiandae.

**MHE. JITU V. SONI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote naomba nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa siku ya leo, lakini pia nichukue fursa hii kumpongeza Rais wetu kwa kazi kubwa na nzuri anayofanya, lakini pia Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kazi kubwa na nzuri na Wizara yake inavyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kuanzisha Wizara ya Uwekezaji, lakini pia kuhamisha Kituo cha Uwekezaji (*TIC*) katika Ofisi ya Waziri Mkuu. Jambo hili tulikuwa tumelisemea

kwa muda mrefu sana kwamba lazima pawe na chombo Serikalini ambacho kitakuwa kinaratibu, kinaunganisha Wizara mbalimbali na ndiyo kinaelekeza ili Serikali iweze kufanya kazi kama Serikali moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, siku zote tulikuwa tunasema huko nyuma hakuna uratibu ndani ya Serikali, kila Wizara ilikuwa inajitahidi ifanye mema katika sekta yake, lakini bila kuwa na uratibu na kufanya kazi kwa pamoja, Serikali kama Serikali isingefanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na ninawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote katika Ofisi ya Waziri Mkuu, tena ni akina mama wote wawili, Mheshimiwa Jenister na Mheshimiwa Kairuki. Ni akina mama ambao wanajiamini na wanaweza kuchukua maamuzi magumu. Pia Manaibu Waziri, Makatibu Wakuu na timu nzima kwa kazi nzuri wanayofanya. Mimi ombi langu ni moja, naomba Waziri wa Uwekezaji ndio awe mratibu mkuu kwa shughuli zote hasa katika biashara inayofanyika hapa nchini katika sekta zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa sababu hili suala tunalozungumza kuhusu urahisi wa kufanya biashara Tanzania, umekuwa mgumu kutokana na kodi, tozo, ada na urasimu mwingi. Hiyo inaweza kuondolewa na Wizara ya Uwekezaji; siyo kwa wawekezaji wa nje tu, lakini pia kwa uwekezaji wa ndani uwe mkubwa au mdogo. Wizara hii inaweza kufanya kazi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipitia bajeti yao lakini bado naona bajeti waliyopewa ni ndogo. Nilikuwa naomba kama inawezekana Wizara hii iongezewe bajeti ili wawe na fedha ya kutosha kufanya utafiti lakini pia waweze kufanya kazi ambazo zinaweza kuunganisha Wizara nyingine zote. Ni vizuri sasa Mawaziri wengine kupitia Wizara zao watoe ushirikiano wa karibu sana na Waziri wa Uwekezaji ili mambo yetu yaweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu kwenye suala hili, ili pawe na urahisi wa kufanya biashara, tunahitaji kuwa na

*One Stop Center.* Sheria inasema, kutokujua sheria siyo kinga. Hivi kila Mtanzania, kama wako milioni 20 wanafanyabiashara, hivi kila mmoja atajua sheria zote? Leo hii tunakwama kwa sababu sekta ambayo ni rasmi inazidi kupungua na sekta isiyokuwa rasmi inazidi kuongezeka kutokana na urasimu na utaratibu ambao ni mbovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sekta isiyokuwa rasmi inazidi kukua kutokana na tozo, ada, kodi mbalimbali ambazo zinatokana na taasisiza udhibiti (*Regulatory Boardies*) charges zao zimekuwa kubwa. Leo hii wote sasa wanashindana kukusanya mapato kwa kuptitia *fine* au tozo mbalimbali ili kuonekana Wizara zao zinakusanya mapato makubwa. Mapato yalitakiwa yatokane na faida inayopatikana na kodi ya hiari watu walipe, hapo ndiyo utaona uchumi umekua na watu wanafanya biashara na wanaridhika kulipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zile tozo ni kubwa mno. Mheshimiwa Rais juzi alisema kwamba liangaliwe na kama ni sheria ziletwe. Huu ndiyo wakati wa kubadilisha hizo sheria na tozo mbalimbali ili ziendane na viwango. *Cost of production* ikiwa kubwa hata tukiwekeza; kama sukari yetu au mafuta gharama ya kuzalisha ndani ya nchi ikiwa kubwa, hatuwezi kushindana na ile inayotoka nje. Mitu akitoka nje, akilipa kodi zote hata ukiweka mara mbili, bado ni rahisi kuliko ile ya ndani. Ni vizuri sasa ile *blueprint* tuifanyie kazi; na siyo kuifanyia kazi kwa kuleta tu Bungeni kwa kuturidhisha sisi, lakini ifanyiwe kazi ili iwe na mafanikio makubwa, ili biashara zetu zikue, viwanda vikue na hali ya ufanyaji wa biashara uwe mzuri hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, muhimu ni kuangalia namna ya kupunguza zile tozo na kodi mbalimbali. Sasa tukija kwenye kila sekta, tutaleta hasa kwenye *Finance Bill* kwamba hivi ni vitu ambavyo vinatakiwa viondolewe au vipunguzwe ili tuweze kuzalisha bidhaa zetu kwa gharama nafuu, bidhaa ambazo tunaweza kuzalisha humu humu nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuptitia Wizara ya Uwekezaji, sisi tuna bidhaa kama nne au tano, tungeweka

muda kwamba ndani ya miaka mitatu tunataka tuwe tunazalisha nchini na tusiagize kutoka nje, tutakuwa na mafanikio makubwa, moja ni mbegu ambayo kwa asilimia 76 tunaagiza kutoka nje ya nchi ambayo hata usalama wa chakula hakuna; lakini pia mafuta ya kula, sukari, maziwa, nyama, samaki lakini pia mboga mboga na matunda. Ni vitu hivyo tu ambavyo tunaweza kuzalisha hapa nchini, hivyo ni vizuri kwa kupitia Wizara ya Uwekezaji tufanye hiyo kazi na Serikali iwekeze katika hayo maeneo tuweze kufanikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali isipowekeza kwenye utafiti, bado hatutafanikiwa kwa sababu bila utafiti hatutakuwa na maendeleo. Ni vizuri tuwekeze kwenye suala la utafiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia asilimia kubwa ya Watanzania wako kwenye Sekta ya Kilimo, zaidi ya asilimia 75. Vijana wetu wanaosoma, wengi sasa hivi ajira hakuna kutokana na fani walizosomea ajira hizo hakuna. Ni vizuri Serikali sasa ikubali maombi yetu ya muda mrefu kwamba huko nyuma tuliondoa *Skill Development Levy*, ile 4% tukaipungua 2% kwenda kwenye *Loans Board*. Naomba asilimia mbili ile ambayo tumeipeleka kwenye *Loans Board* sasa irudi kwenye *Skills Development Levy* iende *VETA* ili tuwekeze kwenye shule zetu hizi za ufundi ili watu wengi waweze kusoma ufundi kwa kuwa ajira zao zipo na hizo kazi uhitaji wao ni mwinci.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo namna ya kuongeza ajira ni kuwekeza kwenye shule zetu za ufundi ili tupate vijana wengi ambao wanaweza wakapata ajira za kawaida ambao uhitaji ni mkubwa; iwe kwenye sekta yoyote, iwe kilimo, mifugo, hata kwenye Sekta ya Madini, tukitaka *value addition* bila kuwekeza kwenye *Vocational Training* watu ambao watajua kusanifu na kuchonga madini yetu ili tuzalishe bidhaa hapa hapa, hatutafanikiwa.

Mheshimiwa Nailbu Spika, kwa hiyo, naomba ile 2% ambayo tuliipeleka katika kipindi tulichokuwa na dharura, hatukuwa na fedha ya mikopo, basi turudishe irudi kwenye

VETA. Mbali na hiyo, ni vizuri pia tukaangalia namna ya kuhakikisha kuwa hiyo *One Stop Center* iwe na mafanikio makubwa kwa biashara kubwa na ndogo, lakini pia Ofisi ya Uwekezaji iweze kukaa na Wizara mbalimbali. Leo hii ili waonekane wanafanya kazi kubwa, wanaanza kudai tozo na ada ya miaka kumi nyuma. Unakuta mtu wa *TFDA* anakuja anakudai vitu vya miaka kumi nyuma. Unakuta *OSHA, Regulatory Boardies*, yaani Taasisi za Udhibiti, zinakuja kukudai vitu vya miaka 10 nyuma. Je, siku zote walikuwa wapi? Sasa ni vizuri tukafutilia mbali madeni ya nyuma, wakaanza leo kwa sababu waliolala usingizi walikuwa ni wao, sio wafanyabiashara. Mfanyabiashara kutokujua sheria, siyo kosa lake. Sasa ni vizuri haya yakafanyiwa kazi na ninaamini kabisa kwamba hali ya ufanyaji biashara itakuwa na unafuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na hiyo, ni vizuri pia sekte binafsi kwa kupitia Baraza la Uwezeshaaji lakini pia kwa kupitia Baraza la Biashara Taifa ambalo iko chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu, liweze kufanya kazi kubwa na kuunganisha na kuangalia kwamba nini kinahitajika ili kazi iweze kwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika watu wamezungumzia urasimu, namshukuru Waziri wa Uwekezaji, juzi kulikuwa na vibali ambavyo vilitakiwa vitolewa ili mtu aanze kuwekeza kwenye Kiwanda cha Sukari. Aliweza kupiga simu mbili na ndani ya wiki moja kibali kikatoka, lakini yule mtu alihangaika zaidi ya miezi sita, ilikuwa hapati. Sasa ni vizuri pawe na mfumo au *website* ili hata kama mtu anaomba katika Wizara nyingine aweze kutoa taarifa hiyo kwa Waziri wa Uwekezaji ili Ofisi yake iweze kufanya kazi ya uratibu kwamba kwa nini hiki kitu hakijatoka kwa muda maalum? Kwa sababu watu wakipata vibali kwa muda maalum, nina uhakika watu watawekeza na mambo yetu yataenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna jambo lingine ambalo ni muhimu sana, kwamba tukija kwenye *Finance Bill* kwa kupitia Waziri wa Uwekezaji na Waziri wa Kazi, ni vizuri tukaangalia hizi kodi mbalimbali ambazo ni kubwa, tuzipunguze lakini tukizipunguza hatutapata tatizo lolote kwenye ukusanyaji kwa sababu *compliance* itakuwa kubwa.

Leo hii kama kodi ni kubwa watu wengi wanaendelea kukwepa, juzi Mheshimiwa Rais amezungumza vizuri sana, naamini muda huu ni muafaka, amezungumzia kipindi cha Bunge la Bajeti, tutaweza kufanikiwa kwa sehemu kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na hiyo, wengi wamezungumzia suala la vibali; upatikanaji wa *permit*. Kwa watu ambao wanawekeza, kuna aina mbili; kuna wale ambalo ni *skilled labour* ambao wana vyeti vyao vyote, lakini pia kuna *unskilled labour*, lakini ana uzoefu mkubwa. Vile vile mwangalie wale ambao ni *unskilled* lakini wana uzoefu, vibali hivyo viwe vinatoka kwa urahisi zaidi ili biashara hizo ziweze kufanyiwa kazi na Serikali itapata kodi kubwa na watu wetu wa humu ndani pia wataweza kujifunza kutokana na suala hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, mbali na hayo, napongeza tu kwa kuanzishwa kwa Wizara hii ya Uwekezaji na ninaamini kabisa kwamba kwa kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu, Wizara zote hizi zikifanya kazi vizuri kwa ushirikiano, tutakuwa na mafanikio makubwa na tutaweza kuhakikisha kwamba nchi yetu inapata viwanda vingi, biashara inakua na uchumi wetu unakua. Wananchi wa...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa, muda wako umekwisha. Ahsante sana. Mheshimiwa Asha Abdallah Juma, atafuatiwa na Mheshimiwa Mussa Rashid Ntimizi na Mheshimiwa Faharia Shomari ajiandae.

**MHE. ASHA ABDALLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Naomba nianze na kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uwezo na nguvu za kuweza kusimama katika Bunge hili leo, na kuweza kuchangia Hotuba hii ya Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana kutoa pongezi za dhati kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa

Jenister, Mheshimiwa Antony Mavunde, Mheshimiwa Stella, Katibu Mkuu na Watendaji wote wanaoshirikiana katika ofisi hii ya Waziri Mkuu, kwa jinsi walivyoilandaa Bajeti hii na jinsi walivyokuwa wanafanya kazi zao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naanza kwa kuunga mkono hoja hii ya bajeti. Napenda kutumia nafasi hii katika Bunge lako hili Tukufu kuandikisha masikitiko yangu ya moyoni na ya dhati kabisa kuhusiana na kwamba, ninavyofahamu hili Bunge ni sehemu ya mhimili mkubwa sana na muhimu sana katika ujenzi wa nchi yetu. Ni mahali pa heshima, tunapotakiwa tufanye kazi zetu kwa taratibu na kwa mujibu wa kanuni na sheria zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha sana, kuna Mheshimiwa aliamua kwa kupitia kwenye Bunge hili kwa kinywa kipana kabisa kusema kwamba Rais analalamika lalamika. Nasikitika sana kwamba Mbunge huyu alivyofanya siyo sawa. Mheshimiwa Rais halalamiki, ameapa kusimamia maendeleo na ustawi wa nchi hii kwa kiapo. Kwa hiyo, ni kazi yake kukosoa, kukemea, kuelekeza na kufuatilia. Ndiyo maana unaona mambo yamechukua sura hii yaliyochukua. Sasa napenda jambo hilo lisije likajirudia hapa kusema kiongozi wetu mkubwa, Amiri Jeshi kwamba yeeye kazi yake ni kulalamika. Hiyo siyo kazi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile namwomba sana Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Magufuli azidishe na aendelee kuwashughulikia wezi, wabadhirifu, wala rushwa na wale wote wanaokwenda kinyume na maagizo ya maadili ya maelekezo ya Chama chetu na misingi yetu. Chama chetu kwa wale wasiokijua ni Chama cha Mapinduzi, ndiyo ninachokikusudia, ninachokisemea hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zinazofanyika kwa usimamizi wa Rais wetu huyu zinatambuliwa hata nje ya mipaka yetu. Sasa kama huku ndani kuna mtu hatambui, huyu ndio anapanda mgomba changaraweni hauwezi ukamea. Tabia na dhamira inayooneshwa baadhi ya wenzenetu humu kwa lengo la kutoka walikotoka kwamba nia

ya kuivuruga Serikali na kuitifua humu sio mahali pake, kama wanataka kuitifua waende wakatifue malundo ya mchanga huko nje na ndio maana Spika juzi aliwaona akawaambia, wakafanye mambo ya huko nje Bunge. Nipende kusisitiza kwamba tukitunze chombo chetu hiki Bunge kama inavyostahili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nijielekeze kwenye mchango na napenda kuchangia kwenye Tume ya Uchaguzi. Tume ipo imara na imepangika vizuri na kama mlivyoona kwenye hotuba hapo, imefanya kazi zake kwa vizuri na imeweza kuongeza vituo na kuboresha madaftari ya kupiga kura, kwa hiyo suala kusimamia demokrasia ya uchaguzi limekaa vizuri. Tumeona hapo kuna ongezeko la vituo 27 kwa upande wa Zanzibar, jambo ambalo ni zuri na nahakikisha kwamba Tume yetu hii pia kwa upande wa Zanzibar iko vizuri vile hakuna tatizo na demokrasia ya vyama itakwenda vizuri na uchaguzi utasimamiwa vizuri na ni matumaini yangu pia uchaguzi unaokuja wa Serikali za Mitaa utakwenda vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunataka kutoa idhari kweli Tume yetu ya Uchaguzi ipo vizuri na ipo imara kwa sababu mimi ni moja kati ya wale waliobahatika kwenda changuzi zinavyofanyika nchi zingine, huko inakuwa hali si hali. Tume ya ya Uchaguzi ni mashaka, tume si tume kwa mujibu wa maadili na itifaki hatuwezi kusema ni wapi na nini, lakini sisi tushukuru tume yetu ipo vizuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba nijielekeze kwenye Ofisi ya Msajili, Ofisi hii ya Msajili kwa sasa badala ya kupitisha ile Sheria Na.5 kuifanyia marekebisho ile ya mwaka 95, naona hali itakuwa nzuri zaidi kwa sababu itapata meno ya kudhibiti wa hivyo wale ambao wamekusudia kufanya vurugu ya aina yoyote, ofisi hii ya msajili ipo tayari kwa ajili yao. Dhamira ya kuhakikisha kwamba hesabu za chama zinaangaliwa vizuri masuala yote yanayohusiana na demokrasia ya vyama vingi kwa msajili kwa imara hizo alizopata itakuwa vizuri. Kwa hiyo napenda kusema kwamba

fungu alilopewa Msajili kama kuna namna yoyote ya kuweza kumwongezea, basi aongezewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ninalotaka kuzungumzia ni mahakama, kama tunavyojuu huu mhimili ni muhimu sana na unahitaji kuimarishwa zaidi kwa kuwekewa nyenzo za kufanya kazi. Kuimarisha mfumo wa utoaji haki ni jambo la lazima. Tumeona katika hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu mashauri kadhaa yameweza kufanyiwa kazi na vile vile tumeweza kuelezwaa na kuona kwamba kuna ongezeko la Majaji wa Mahakama ya Rufaa na kuweza vile vile kuweka haya mabadiliko yote. Sasa unapoweza kupata Majaji ushauri wangu ni kwamba lazima uende sambamba na uboreshwaji wa majengo ya mahakama yenye.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kadri mahitaji yanapoongezeka majengo vile vile ya mahakama inabidi yaongezeke. Napongeza sana kazi zinazofanywa na hasa Kitengo cha Kusimamia Majengo ya Mahakama, hiki kitengo kimefanya kazi nzuri sana, sisi tulipata bahati ya kukagua majengo haya tumeweza kuona majengo ya kileo kabisa ya Mahakama ya Rufaa kule Mara na kule Kigoma, kwa kweli Kitengo hiki kinafanya kazi nzuri sana. Kuna sehemu nyingi ambazo bado majengo ya mahakama hayajafikia, lakini tunaamini kwamba fungu likiwekwa hawa watapata spidi ya kumaliza kazi ambayo imepangwa na nyingine ambayo itaweza kuzuka. Kwa hiyo upande wa mahakama kwa kweli umejiweka vizuri sana. Naomba kama kuna ziada ya fedha hapo waweze kuongezewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka sasa kuzungumzia kilimo cha mchikichi, japokuwa kilipata msito kidogo, kilisita kwa sababu kilianzishwa siku nyingi, lakini kama watu wengine walivyosema kuchelewa sio tatizo, nia ni ile kuhakikisha unataka kufika kule unakokwenda. Kwa hali tulioionya ya Kigoma na sehemu nyingine na sehemu nyingi za Tanzania, hii miche inaweza kustawi sana na tukapata mazao mazuri sana. Vile vile lazima twende sambamba na viwanda vya kuchakata hizi chikichi. Tumeweza kuona wananchi kule Kigoma wanajitahidi sana kutumia matunda haya ya chikichi

katika kujipatia kipato zaidi kwa kutengeneza sabuni na vitu vingine. Lakini vifaa wanavyotumia bado duni. Kwa hiyo Serikali ingefaa kuwaona watu hawa ambao wengi ni wanawake wanaojishughulisha kwa ujasiliamali kwa kutumia zao hili ili waweze kufanya shughuli zao kitaalam zaidi na kuleta tija zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na zao hilo la chikichi kwa mikoa kama Kigoma lakini naweza hapa kuingizia tu kwamba bado barabara kule haijaka vizuri, inabidi litupwe jicho la ziada kuweka barabara kule.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nalipenda na linanikosha sana ni hili la wazo la kuanzisha *SGR - Standard Gauge Railway* na ninapoona kwamba itakapofika 2019 itakuwa imeshafika Morogoro, basi inanipa matumaini kwamba inaweza kufika Kigoma hatimaye Mwanza na kwingine na kwa kupitia kwenye reli hiyo ndio pale ambapo uchumi wa maeneo ya pembezoni utaweza kukua kwa sababu watu watasafirisha huku na huku bidhaa zao. Kwa hiyo, hili wazo ambalo *champion* wetu Rais Jemedari Mkuu amelivalia njuga, napenda nimpongeze linakwenda vizuri sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa, kengele ya pili imegonga.

**MHE. ASHA ABDULLAH JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mussa Ntimizi atafutiwa na Mheshimiwa Faharia Shomari, Mheshimiwa Mashauri Ndaki ajiandae.

**MHE. MUSSA R. NTIMIZI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuchangia hotuba ya bajeti ya Ofisi ya Waziri Mkuu. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri Mkuu kwa kazi kubwa anayoifanya na Watanzania wanaiona. Anafanya kazi anajitoa sana, anatembelea kwenye majimbo yetu,

anahakikisha kabisa kwamba utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi inakwenda sawasawa. Hata hivyo, kwa kufanya kwake kazi vizuri ana wasaidizi wake lazima na wenyewe tuwapongeze, hawalali usiku na mchana kuhakikisha kwamba kazi zinakwenda sawasawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mhagama, dada yangu anafanya kazi nzuri sana; Mheshimiwa Kairuki, anafanya kazi nzuri sana; Mheshimiwa mdogo wangu Mavunde, *big up* anafanya kazi nzuri sana, hatuangushi vijana wenzake; Mheshimiwa Stella Ikupa anafanya kazi nzuri nzuri sana. Kwa ujumla Ofisi ya Waziri Mkuu inaratibu mambo vizuri na mambo yanakwenda sawasawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, miaka minne iliyopita tulikuwa tunaiomba Serikali kutekeleza ahadi ambazo tuliziahidi wakati wa uchaguzi. Leo katika kipindi cha miaka minne tuna haki leo Wabunge kusimama hapa na kuipongeza Serikali kwa kazi kubwa ilioifanya kwa kutekeleza llani ya Uchaguzi ambayo tulikuwa tumeahidi. Kwa hiyo sisi Wabunge wa CCM tunajivunia, tunakwenda kwenye uchaguzi mambo yetu yakiwa yako juu sana na kazi hii imefanywa vizuri kwa uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tunasema kwamba tunakwenda vizuri. Naomba niseme maneno machache, hasa mimi natoa mfano kwenye Jimbo langu la Igalula na nchi yetu kwa ujumla, kuna watu wanazungumza ujenzi wa *standard gauge* hauna faida kwa nchi yetu. Tulikuwa tunalalamika mizigo, sisi ambao tunatoa mikoa ambayo reli ya kati inapita, reli iliyokuwepo ilikuwa ni tatizo kubwa kwa usafiri wa wananchi wa mikoa hiyo, usafirishaji wa mizigo ulishuka kwa asilimia kubwa sana kwa sababu ya reli yenyewe kutobudu uzito wa mizigo inayosafirishwa kwa reli hiyo, leo tunajenga reli ambayo itabeba mizigo mizito na mizigo mingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, si hivyo tu, pia tunazungumzia muda wa usafiri utakuwa mchache, maana yake kutoka Dar es Salaam kwenda Tabora unakwenda kwa

saa tano, wakati tulikuwa tunakwenda kwa siku tatu, tunaadhirika sana njia. Kwa hiyo sisi tunaotoka katika maeneo yale tunaona umuhimu wa *standard gauge* kwa maana reli ya kisasa inayokuja, tutakuwa na uhakika wa ghamama za usafiri zitakuwa ndogo, tutakuwa na uhakika wa safari yetu kwa sababu zamani treni ilikuwa inadondoka sana, sasa hivi tutakuwa uhakika wa usalama wa safari yetu. Kwa hiyo unapozungumzia *standard gauge* kwa wananchi wa Igalula tunatarajia itasafirisha tumbaku yetu toka Igalula kwenda sokoni kwa ghamama nzuri na kwa muda ambao unategemewa kuwa mdogo sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi katika Igalula tunashukuru, tulikuja tukazungumza kwamba kuna maboma mengi wananchi wamejenga kwa nguvu zao yanatakiwa Serikali itenye fedha kuyakamilisha. Nataka kusema tumepekea milioni 500 kukamilisha ujenzi wa madarasa ya shule za misingi na shule za sekondari katika Jimbo la Igalula ambazo zilizishwa na nguvu za wananchi. Kwa hiyo katika bajeti hii ya Waziri Mkuu, naomba nifikishe salamu za wananchi wa Igalula zile nguvu zao walizozieweka katika kujenga maboma yale Serikali imeona uwezekano wa kuwasaidia na imetuletea zaidi ya shilingi milioni 500. Ambacho tunakiomba, tuna maboma mengi zaidi, tunaomba tuendelee kuangaliwa ili tuweze kusaidia nguvu za wananchi ambazo wameziwekeza katika maeneo mbalimbali ikiwemo pia kwenye eneo la afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo upungufu mchache ambao tunaomba Serikali iendelee kuuangalia ili wananchi wa Igalula waendelee kuwa juu kama vile ambavyo Serikali yetu ipo juu katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Katika Mkoa wetu wa Tabora tuna takribani kilomita 8,000 za barabara, lakini tunaletewa shilingi bilioni nane kutengeneza zile kilomita 8,000, hazitoshi, mtandao wa barabara ni mkubwa na fedha tunazoletewa ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, niombe Serikali iungalie Mkoa wetu wa Tabora, tuongezewe fedha ili ziweze kusaidia huu mtandao mkubwa wa barabara uliopo katika Mkoa wetu

wa Tabora. Hata hivyo, nishauri katika eneo letu la kilimo, miaka yote tunashauri kilimo cha umwagiliaji ndio kitakuwa mkombozi wa wananchi wetu ambao wanalima huko vijijiini, tusipowekeza katika kilimo cha umwagiliaji, hatutowasaidia wananchi wetu. Naomba Serikali iliangular hili ili tuongeze tija katika kilimo, tuweze kupata pato la wananchi wetu na tuweze kupata pato la nchi kwa ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nataka niishukuru sana Serikali kwa kazi kubwa inayoifanya, lakini niombe katika Mkoa wetu wa Tabora, Wilaya yetu ya Uyui ni Wilaya kubwa sana, *DC* wetu aangaliwe sana. Mwaka wa nne sasa hana gari na wilaya ni kubwa, anahitaji kufanya kazi ya ziada kusimamia miradi mingi ambayo inakuja katika Mkoa wetu wa Tabara. Niombe sana tuweze kuangular namna ya kusaidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, bado inahitajika nguvu kubwa katika eneo la afya. Sisi katika Jimbo la Igalula tumejenga vituo zaidi ya vitano lakini tumepata fedha za kituo kimoja cha afya. Nina hakika katika bajeti hii inayokuja tutaendelea kuangular nguvu hizi za wananchi na kuongeza fedha na zaidi ili ziweze kusaidia kuondoa tatizo la afya kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimalizie, kwa miradi ambayo inafanyika katika maeneo yetu, mimi nitoe mfano wa mwisho, katika barabara tumepokea zaidi ya bilioni mbili za barabara zetu za ndani katika Jimbo la Igalula, kwa nini tusiishukuru Serikali yetu ya Awamu ya Tano kwa kazi kubwa ambayo inaifanya. Tumepata zaidi ya bilioni 149 za kujenga barabara ya lami ya Chaya - Nyahua ya kilomita 189 ambayo inakaribia kwisha, ni lazima tuendelee kuishukuru Serikali kwa kazi nzuri ambayo inaifanya na tunazidi kuwapa moyo kwamba Wabunge wenu wa CCM tunaona kazi ambayo inafanyika na tunazidi kuwatia moyo kwamba wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niunge mkono hoja na ahsante sana. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Fakharia Shomari atafuatiwa na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud ajiandae.

**MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza sina budi kumshukuru Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa hotuba yake nzuri aliyotoa na ambayo imetoa mwanga kwa Watanzania na wengi walioisikia hotuba yake wanaiunga mkono kama tunavyounga mkono sisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, najua ameweza kufanya hivi kwa sababu ana Mawaziri walio mahiri, ana Manaibu Waziri walio mahiri na watendaji wake katika Wizara yake pia ni watendaji walio bora na waliotukukuka na ndio maana akaweza kufanya kitu kizuri kama hiki. Vilevile sina budi kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Makamu wake wa Rais kwa maelekezo yao mema wanayoyatoa na kwa shughuli zao njema za kazi wanazozifanya, inakuwa dira kwa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuzungumzia huu ukurasa wa 56 unaozungumzia mambo ya afya. Kwa kweli nampongeza Mheshimiwa Waziri Mkuu pale alipoeleza kwamba vituo vya afya vilikuwepo 7,678 na sana vimefika 8,119. Hili ni jambo jema kwa sababu tunaongeza vituo ili kuwasaidia Watanzania kupata afya bora. Hata hivyo, tukae tukijua kuna vituo vinavyotoa dawa hovyo mitaani *pharmacy*. Vituo hivi unakwenda unasema unataka dawa au unamwambia nini shida yako unayoumwa na unapewa dawa bila kuangalia una cheti ya Daktari au hauna. Unajua kuna dawa nyingine kama akina *panadol* unaweza ukapewa, hasa hizi za maumivu, ukaeenda kule kwenye hospital *pharmacy* zao na unaweza ukapewa bila hata kuwa na cheti, lakini kuna zingine lazima uwe na cheti cha Daktari, sio unakwenda unamwambia naumwa kitu fulani na baadaye anakupa dawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa hapa panataka elimu itolewe, watupe elimu sisi wananchi, wawape elimu na wale

wenye vituo, maana wao wanajali fedha kuliko afya ya mtu. Sasa na hivyo tutawapa matatizo Watanzania ambao wengine hawajui, ye ye anajua nikienda hospitali itabidi Daktari nimlipe na nani nimlipe, lakini nikienda *pharmacy* nitanunua dawa tu, wakati dawa atakayonunua siku nyiningine haitamtibu, itampa madhara. Sasa hapa kitu kikubwa ni elimu kutolewa kwetu zote na vilevile kufanya ziara mara kwa mara kuvamia hivi vituo ili wapate uhakika wa hao wanayoyatenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna msemo unatumia sana, tunaweza au naweza. Huu unamtaka mama mjamzito na baba mwenye mjamzito nyumbani awe anamsaidia mama mjamzito kwenda kliniki na hii lazima pia iwe inapigiwa debe. Mama mjamzito anapokwenda kliniki kupima akienda na baba toka kuanzia mwanzo mpaka atakapojifungua, itasaidia sana baba kujua upungufu wa mama yule. Sasa unaambiwa utumie neno naweza, sasa mnaweza mkikaa baba anasema na mama anasema ili kumfanya kiumbe aliyeo tumboni kupata uhai uliokuwa mwema. Hivyo, hili linataka elimu ili kwa mama inambidi lazima aende lakini kwa baba inakuwa kidogo mbinde kumsindikiza mama, hata *handbag* yake baba inabidi ambebee maana imeshakuwa mama ana mzigo. Sasa na ye ye akienda naye na kambebea ki-*handbag* chake mapenzi yanazidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikija ukurasa wa 29 uzalishaji wa mazoa ya biashara, suala hili nampongeza Mheshimiwa Rais kwa ziara yake aliyoifanya juzi Mtwara, kaupata ukweli kuondosha upotoshwaji, maana vyombo vyahabari vilikuwa vinasema kwamba watu hawajalipwa, Serikali hajjawalipa watu inawasumbua kumbe katikati kuna watu walipita njia za mkato wakazinunua korosho wakajifanya wao ndiyo wenye korosho wakauze Serikali ili wao wapate faida. Baada ya kujulikana Mheshimiwa kawasemehe, kawaambia wapite kwenye sheria, wawaone, wawalipe lakini lisiendee. Namshukuru Rais wangu mweledi, ana ufahamu mpana na anatizama tatizo na akalipatia ufumbuzi ili kuwasaidia Watanzania kuondokana na matatizo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuongelea ukurasa wa 81 kuhusu Muungano. Kwanza niipongeze Serikali ya Muungano na lazima nipongeze kwa kufuta malimbikizo ya deni ya kodi ya VATyalifofikia shilingi bilioni 2.8, hili ni jambo jema, hapa ndiyo Muungano tunapouona. Muungano unazungumza pande zote mbili msaidiane, hii ilikuwa si kusaidia ni wajibu wake umefanya kwa sababu ilikuwa kelele ikipigwa muda mrefu, wameliangalia, wakaona tatizo hakuna, ni haki yao na kuweza kulitekeleza. Kwa hili natoa pongezi kwa Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kushirikiana hili suala likamalizika kwa amani na usalama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sikitiko langu liko mwisho hapa, baadhi ya Ofisi za Muungano Zanzibar zina majengo ya Muungano lakini Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje kuanzia mwaka 1964 hadi leo mwaka 2019 halina jengo lake *officially* walilojenga, jengo wanalonumia ni nyumba iliyokuwa ya Kiongozi wa Upinzani kabla ya Mapinduzi. Jengo la nyumba ukaligeuza ofisi unatupa pesa zako bure kwa sababu halitokubali. Suala hili nimeshalizungumza mara nyingi, naomba Mheshimiwa Waziri alichukue, tunataka jengo la Wizara ya Mambo ya Nchi za Nje Zanzibar kama ilivyojenga Muungano, Polisi, Jeshi, Uhamiaji na Wizara nyingine na wao ni Wizara kubwa...

*(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fakharia, kengele ya pili.

**MHE. FAKHARIA SHOMARI KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Mashimba Mashauri Ndaki, atafuatiwa na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud, tutamalizia na Mheshimiwa Augustino Manyanda Masele.

**MHE. MASHIMBA M. NDAKI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili nami niweze kuchangia kwenye hotuba hii ya Mheshimiwa Waziri Mkuu. Nichukue nafasi hii kwanza kabisa kumshukuru sana Mheshimiwa Waziri Mkuu kwa kushughulikia kwa sehemu kubwa sana suala la ushirika kwenye maeneo yetu kwa sababu wakati huo ushirika ulikuwa umekufa kabisa. Mwaka jana wakati anasisitiza mimi binafsi nilikuwa na wasiwasi kama unaweza ukafanya jambo lolote lakini kwa kweli alijitahidi sana na watu walielewa ushirika umefanya jambo zuri kwa mwaka huu ulioisha na naamini mwaka huu tunaouanza utafanya vizuri zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimpongeze sana Mheshimiwa Waziri katika Ofisi ya Waziri ya Mkuu, Mheshimiwa Jenista kwa kutusaidia kwenye Wilaya yangu na kwenye Jimbo langu alitupa pesa tukaanzisha Kiwanda cha Kuchambua Mpunga pamoja na ku-grade. Tumefanikiwa na tumeweza, vijana wanaendelea, wamepata ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nimshukuru kwa sababu aliweka mbegu kwenye Kiwanda cha Chaki na chenyewe sasa kimeota, kimekuwa kiwanda kikubwa, tume pata mabilioni kutoka Serikalini, mjenzi tayari amekwishaanza kujenga. Kwa hiyo, nawashukuru sana Ofisi ya Waziri Mkuu kwa uwezesho mkubwa ili vijana wetu waweze kupata ajira, kujiongezea kipato na kuendesha maisha yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze mambo mawili tu. Jambo la kwanza nataka kuzungumza juu ya ajira hizo hizo za vijana. Uchumi wetu kwa sehemu kubwa unaendeshwa na sekta isiyo rasmi. Sekta isiyo rasmi ina utawala uchumi wetu kwa asilimia kama 60 hivi. Katika sekta hii isiyo rasmi sehemu kubwa wanaofanya kazi huko ni vijana maana nguvu kazi ya vijana kwenye Taifa hili ni kama asilimia 56 na asilimia 70 wako kwenye sekta isiyo rasmi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sekta hii inapoendelea kuwa kubwa namna hii siyo afya sana kwa uchumi wetu kwa sababu wataalam wa mambo ya uchumi wanasema sekta isiyo rasmi kama ni kubwa tuhesabu kwamba nchi hiyo

itaendelea kuwa katika hali ya umaskini kwa sababu sekta isiyo rasmi haina mchango mkubwa unaoweza kueleweka kwa Serikali na hata kwa uchumi wa nchi hiyo. Kwa hiyo, sekta hii isiyo rasmi lazima tuendelee kufanya juhudui kuipunguza.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa juhudui kubwa zinazofanywa na Serikali ili kurasi misha biashara za baadhi ya watu lakini pia kujenga ujuzi kwa vijana ili waweze kujajiri watoke kwenye sekta hii isiyo rasmi wawe rasmi zaidi. Pia nashukuru pia kwa mpango wa Serikali ambao sasa umekwishaanza wa kugawa vitambulisho vya Sh.20,000 ili wafanyabiashara na wajasiriamali wadogo wadogo waweze kusajiliwa lakini hii ni hatua ya kwanza tu ili waweze kwenda hatua ya pili ambayo sasa itawafanya wajulikane na waweze kutoa mchango mkubwa kwenye uchumi wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye sekta hii isiyo rasmi, sasa wanaingia vijana ambao wamemaliza vyuo vikuu na vyuo mbalimbali kwa sababu ya kukosa nafasi za ajira maeneo mengine. Sekta hii inapoingiliwa na watu waliosoma namna hii, lazima sasa kama Taifa tuanze kuangalia ni kwa namna gani tunafanya kwa kasi kuipunguza sekta hii ili iwe rasmi watu hawa ambao Taifa limewasomesha waweze kuchangia sawasawa kwenye uchumi wa nchi yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, vinginevyo tukiendelea kuiacha ikaendelea kuwa kubwa kwa wimbi kubwa la wasomi wanaoingia kwenye sekta hii, kwanza wakiingia huko kwa sababu mambo yake mengi hayajaeleweka vizuri watachanganyikiwa na kwa hiyo itakuwa ni chanzo cha vurugu au cha kukosesha amani nchi yetu kwa sababu wao wana-*higher expectation*. Tunaposoma chuoni tunaamini kwamba ukitoka hapo basi utakuwa umeukata sasa wakikutana na sekta isiyo rasmi ambayo hajaeleweka vizuri inaweza ikwapunguzia amani zaidi na hivyo kuwaongezea msongo wa mawazo na hatimaye kipelekeea kutupeleka kwenye mahali ambapo hatutaki kwenda. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka kushauri pia vijana wetu wengi wanaomaliza vyuo vikuu hata kama

ajira zipo wanashindwa kuajiriwa kwa sababu ya kukosa uzoefu. Suala hili limekuwa tatizo kubwa kweli. Nashauri Serikali kwa nini isije na mpango wa kujengea uwezo vijana wetu wanaomaliza vyuo wote wapate uzoefu wa mambo waliyoyasomea huko chuoni kuititia programu ambayo itakuwa ni ya kujenga uzoefu ya kiserikali. Siyo hii ambayo mtu anakuwa chuoni anaenda *practical* sijui miezi miwili, mitatu, *no*, akimaliza chuo kikuu aende *Internship Programme* ya muda wa mwaka mmoja au miwili ajenge uzoefu, aweze kuajiriwa nafasi za ajira zinapotokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunakutana na watu mbalimbali, mashirika mbalimbali ya kimataifa na taasisi zingine zisizo za kiserikali zinasema tunashindwa kuwaajiri vijana wanaotoka chuoni kwa sababu kwanza uzoefu hana lakini pia ujuzi wa kazi ile ambayo wangeweza kumpa hana, sasa atapataje uzoefu na ujuzi huo? Serikali ikija na mpango wa kila mwanafunzi anapomaliza chuo aende kwa Afisa Utumishi wa Wilaya, Idara au wa chombo chochote cha Serikali akae hapo, gharama zinaweza kuwa za mzazi au mlezi ili ajengewe uwezo awe na uzoefu na ujuzi wa lutosha ili aweze kuajirika nafasi za ajira zinapopatikana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tukiendelea na utaratibu tulio nao sasa mtu amalize chuo kikuu, ana matarajio makubwa, anafikiri atapata kazi, akienda kwenye *interview* anaonekana hana uzoefu, anarudishwa aende nyumbani akafanye nini? Kwa hiyo, nashauri Serikali kwamba ni muhimu sasa ije na *Internship Programme* ambayo itawawezesha vijana hawa wapate uzoefu na ujuzi wa mambo waliyoyasomea na hasa kazini ili waweze kuajirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo nataka nizungumze na pengine litakuwa jambo la mwisho, ni suala la viwanda. Ni hivi, wawekezaji wa nje tunawahitaji sana lakini pia wawekezaji wa ndani nao tunawahitaji sana. Nadhani hawa wa ndani tunawahitaji zaidi kwa sababu wao pia wanatuona sisi kama Watanzania wenzao. Najua wawekezaji wa nje ni wazuri lakini wanatuona sisi kama soko lakini pia kama chanzo cha malighafi ili kutengeneza *semi-processed*

commodity waweze kwenda kumalizia kwenye viwanda vyao kule nyumbani.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nizungumze tu juu ya viwanda vya nguo. Ni kweli tuna kauli mbiu inayosema 'pamba hadi nguo' lakini ni kauli mbiu tu inaungwa mkono na Sera ipi ya Viwanda vya Nguo? Hatuna Sera ya Viwanda vya Nguo! Naelewa tuna Sera ya Viwanda lakini Sera mahsusii kwa ajili ya Viwanda vya Nguo haipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, amesema Mheshimiwa mama Kilango jana hapa, nchi hii ina uwezo mkubwa wa kuzalisha pamba nyingi na hivyo kwa pamba hii tungeweza kuajiri watu wengi zaidi kama tungeangalia kwa ndani kwanza badala ya kuangalia soko la nje. Habari ya pamba ingeweza kujenga uchumi wetu vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa mama Malecela jana ametuambia Bangladesh ambayo ilikuwa nchi maskini sana hailimi pamba lakini imeajiri watu wake asilimia 85 kupitia pamba ambayo inazalishwa sehemu nyingine. Sasa sisi ni zaidi maana tuna watu milioni sita ambaa wameajiriwa kwa kulima pamba kwenye nchi hii ambapo pamba yao inaweza ikatengeneza ajira zingine milioni tatu na kitu au mpaka nne. Kwa hiyo, pamba inaweza ikaajiri watu milioni kumi katika nchi hii ikiwa tutafanya juhudzi za makusudi kuwaunga mkono wale waliowekeza kwenye viwanda vya pamba. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nini tusiwe na mpango kama ule tulionao kwenye sukari? Mbona viwanda vya sukari vimeweza kutu-*sustain*. Viwanda vya sukari vinazalisha sukari kwa nchi hii, hatuzalishi sukari kwa kuuza nje lakini tunazalisha sukari kwa ajili yetu Watanzania na tumevilinda kwa namna mbalimbali kwa kuzuia sukari isiingie hapa. Viwanda vya pamba hatujavilinda kwa namna hiyo, tumeacha soko huria hata kwa vitu ambavyo vinaweza vikatengenezwa hapa kwa kutumia pamba yetu na viwanda hivyo vikatengeneza ajira kwa ajili ya watu wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana tutafute ni kwa namna gani tunaweza kuongeza uzalishaji wa pamba lakini kuongeza viwanda vinavyochambua na kutengeneza nguo zinazotokana na pamba kutoka kwenye pamba yetu badala ya kuangalia tu kuuza pamba iliyo ghafi kwenda nje. *After all* tunapoiuza kule nje kilo moja kwa wenzetu inazalisha mashati matatu sisi hapa mkulima wa kwangu kule Maswa anapata Sh.1,200 tu lakini yule tuliymuuzia pamba kule nje ananilettea shati, shati moja hapa nitanunua kwa Sh.40,000 mara tatu ni Sh.120,000. Tumetengeneza ajira kwake, tumemuongezea kipato yeye, sisi ambao tumezalisha tumeachwa hatuna kitu. Kwa hiyo, nafikiri Serikali ianzesasa kuwa na mkakati na mazao haya ambayo hasa ni ya Kimkakati tuone ni kwa namna gani tunaweza kuyalinda yakaajiri watu wetu wengi baadaye yakatupa kipato cha kutosha kwenye nchi yetu na watu wetu wakapata ajira wakafurahia matunda ya uhuru wa nchi yao. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka niseme hayo mambo mawili tu kwa leo, nitazungumza mambo mengine nitakapopata nafasi nyngine hasa kuhusiana na viwanda vya nguo hapa nchini. Viwanda vya nguo vya hapa nchini kwa kweli hatujavitendea haki kwa sababu hatuvilindi, vinajipigania vyenyewe lakini ukijaribu kuangalia waliowekeza ni wazawa, ni Watanzania ambao wanaajiri Watanzania, wanatupatia kipato na tunapata namna ya kuendesha maisha yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi, naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tunaendelea na Mheshimiwa Khadija Hassan Aboud.

**MHE. KADIJA HASSAN ABOUD:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote na mimi napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeniweka hadi leo kuwa nina afya na uzima. Kwanza, naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii adhimu kuipongeza Serikali ya Chama cha Mapinduzi, inayoongozwa na jemedari wetu Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli; Makamu wa Rais Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan; Waziri Mkuu pamoja na Mawaziri wote walimo ndani ya Wizara hii ya Ofisi ya Waziri ya Waziri Mkuu, Mheshimiwa Dada yangu Jenista Mhagama na Mheshimiwa Angellah Kairuki, pamoja na Naibu Mawaziri wote kwa nzuri wanayoifanya katika kutekeleza majukumu yao na kuwaletea wananchi wetu maendeleo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, bajeti ya mwaka jana nilichangia kuhusu kusamehewa VAT kwa umeme tunaouziwa kutoka *TANESCO* kwenda *ZECO* Zanzibar. Napenda nichukue nafasi hii kwa heshima kubwa kwa niaba ya Wazanzibar kuipongeza kwa dhati Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Marais wetu wawill kwa kutafakari na kufikiria hili kwa lengo la kuimarisha Muungano kwa vitendo na kuudumisha kwa kutusamehe deni la umeme la shilingi bilioni 22.9 na pia katuondelea VAT kwenye umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala hili litaongeza ari ya pamoja kwamba Tanzania tuna dhamira ya dhati kuelekea kwenye uchumi wa viwanda kwa sababu viwanda vingi vinategemea umeme. Kwa hiyo, kupungua kwa bei ya umeme kutaongeza chachu ya wawekezaji Zanzibar, ajira itapatikana na uchumi utakua kwa pande zote mbili za Muungano. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchangia na kuipongeza Wizara hii ya Uwekezaji kwa kuendelea kuandaa mazingira wezeshi kwa wafanyabiashara na wawekezaji ndani ya nchi. Naomba juhudhi hizo ziendelee kwa kupunguza changamoto mbalimbali zinazowakabili wawekezaji wetu ili kuongeza uwekezaji katika sekta mbalimbali na hatimaye kuongeza ajira, kukuza uchumi na kufikia hatua ya uchumi wa kati. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili naipongeza sana Wizara ya Kilimo lakini pia naipongeza Wizara ya Mifugo

kwamba tayari wameshaanza kuanzisha viwanda vy  
nyama pamoja na usindikaji wa ngozi. Kama tunavyofahamu  
ngozi yetu ili kuwa haina soko lakini sasa ngozi yetu itapata  
masoko kwa kusindikwa hapa nchini na pia kuanzisha  
vivanda vy nyama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza Rais  
wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuleta  
vitambulisho vy waafanyabiashara au wajasiriamali wadogo  
ili waweze kufanya biashara zao bila ya kubughudhiwa.  
Pamoja na hilo napenda tuendelee kuzishauri Halmashauri  
zetu ambazo baadhi yao zinawabughudhi hawa  
wafanyabiashara na wajasiriamali wadogowadogo kwa  
kuwatoza kodi ndogo ndogo. Mheshimiwa Rais amelikemea  
hilo, kwa hivyo na sisi tumuunge mkono kwa kulikemea ili  
wafanyabiashara na wazalishaji wetu wadogowadogo  
waweze kufanya biashara zao bila kubughudhiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uwekezaji tuhakikishe  
malighafi za ndani zinapata masoko na yataanzia kwenye  
vivanda vinawekezwa hapa nchini. Nashauri tuhakikishe  
vivanda vyetu vinavyowekezwa hapa nchini vinatumia  
malighafi zetu za ndani ili kuwapa wakulima wetu masoko,  
masoko yetu yaanzie humu ndani ya nchi kwanza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hilo, ili tupate  
masoko na bidhaa bora ambazo zitahitajika katika vivanda  
vitakavyoanzishwa ni lazima tuwekeze vizuri kwenye sekta ya  
kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuendeleza utafiti ili tupate  
mbegu bora za mifugo na kilimo ili bidhaa zetu kwenye  
vivanda hivyo ziwe na tija. Tuwe na bidhaa chache  
tunazozalisha lakini tunapata tija kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye suala la uvuvi,  
naomba Serikali iendelee na harakati za kuwekeza kwenye  
uvuvi wa bahari kuu. Nashauri iwekeze kwa kujenga gati za  
uvuvi na kununua meli uvuvi kwa ajili ya kujipanga sasa  
kuingia kwenye soko la kimataifa kwa uvuvi wa bahari kuu.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuipongeza Serikali kwa juhudini mbalimbali inayochukua katika kuwalettea wananchi wetu maendeleo ikiwemo kupunguza kodi na tozo mbalimbali kwa bidhaa mbalimbali za kilimo na ufugaji. Serikali imepunguza tozo na naomba iendelee kuangalia tozo mbalimbali ambazo zinakwamisha wawekezaji na wazalishaji wetu wadogo wadogo. Nashauri Serikali iendelee kukaa na wawekezaji na wazalishaji wadogowadogo ili kubadilishana mawazo na kutatua na kuzivumbua changamoto mbalimbali zinazokwamisha shughuli za maendeleo katika nchi yetu ili uwekezaji wetu uwe mzuri na wenye tija. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, namalizia kwa kuipongeza Serikali kwa kuwa nchi yetu sasa iko salama, mipaka ya nchi iko salama, shughuli za maendeleo na kiuchumi zinafanyika kwa sababu nchi iko salama, kuna utawala bora, maendeleo yanapatikana, juhudini zinaonekana, wananchi wanafurahila maendeleo, reli zinajengwa, miundombinu inaimarishwa, barabara zinajengwa na ndege watu wanakosa nafasi. Sasa hivi watu wanapotaka kusafiri kwenda nje wanaambishi ndege ya *Air Tanzania* imejaa wanaanza kuhangaika kutafuta ndege maeneo mengine ili waweze kusafiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana kwa michango yenu kwa siku ya leo. Naamini upande wa Serikali umesikiliza na kama utaratibu wetu ulivyo wao wataitazama michago ile ambayo imelenga kuboresha yale ambayo Waziri wa Fedha aliyaleta mbele yetu.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kusema hayo, niahirishe shughuli za Bunge mpaka Siku ya Jumatatu, saa tatu asubuhi.

*(Saa 1:45 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Jumatatu,  
Tarehe 8 Aprili, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*